BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Mbili – Tarehe 28 Juni, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

DUA

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu!

NDG. CHARLES J. MLOKA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

Na. 443

Hospitali ya Wilaya ya Maswa

MHE. DKT. RAPHAEL M.CHEGENI (K.n.y. MHE. STANSLAUS H. NYONGO) aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Maswa ina uwezo mkubwa wa kuhudumia wananchi wa Mkoa wa Simiyu:-

Je, ni lini hospitali hiyo itapandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Rufaa?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hospitali ya Wilaya ya Maswa inatoa huduma za afya kwa wagonjwa wa Wilaya ya Maswa na miundombinu yake haitoshelezi kuwa hospitali ya mkoa. Mkoa wa Simiyu umeandaa makubaliano

(memorundum of understanding) ya kuifanya Hospitali ya Wilaya ya Bariadi kuwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu kwa muda ambapo inatarajiwa kuanza kutoa huduma zenye hadhi hiyo kuanzia tarehe 1/7/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu, mkoa umeshaanza kujenga Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa kufuata vigezo vinavyostahili ambapo hadi sasa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* limeanza kujengwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi bilioni 1.4 ili kuendelea na ujenzi huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M.CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa Mkoa wa Simiyu ni moja ya mikoa mipya, tuna tatizo kubwa sana la kutokuwa na Hospitali ya Rufaa. Kwa vile Mheshimiwa Nyongo alikuwa ameomba kwamba, Hospitali ya Maswa ipewe hadhi hiyo ya kuwa hospitali ya rufaa, lakini Mkoa wa Simiyu tuliamua kwamba Bariadi ndiyo inafaa kuwa Hospitali ya Rufaa. Sasa kwa kuwa Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, ni lini ujenzi huu wa kukamilisha Hospitali ya Rufaa kwa Mkoa wa Simiyu na mikoa mingine mipya ikiwemo Mikoa ya Songwe, Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Geita pamoja na Simiyu yenyewe, lini hii mikoa mipya itasaidiwa kupata hospitali za rufaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa katika Wilaya mpya vilevile ndani ya mikoa hii mipya ikiwemo na Wilaya ya Usega, tuna tatizo la kutokuwa na Hospitali za Wilaya na sisi katika Wilaya ya Busega tumeiteua Hospitali ya Mkula kwa mkataba wa miaka miwili kuwa hospitali teule ili iweze kutoa huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Busega waweze kupata huduma za Kiwilaya. Lini mchakato huu wa Serikali utakamilika? Tumeshapeleka maombi Wizarani sasa ni muda mrefu lakini hatujapata majibu. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kukiri wazi kwamba, kwa mtazamo wake wa Hospitali ya Bariadi ambayo Serikali mwaka huu tunajielekeza kupeleka 1.4 *billion* kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mkoa. Hapa maana yake, ule ujenzi uendelee na ni mtazamo mzuri, hata wao kule wanaona kwamba inastahili iwe Hospitali ya Kanda. Kwa hiyo, kikubwa zaidi tutaendelea kuipa nguvu hiyo Hospitali ya Bariadi, lengo kubwa ni kuwa hospitali inaweza kuhudumia ukanda wote ule. Pia suala zima la ujenzi wa Hospitali ya Mkoa, huu ni mpango mkakati wa Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa sababu tunajua tuna mikoa mipya ambayo, tumeianzisha kama alivyosema kuna Songwe na mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kinachohitajika kufanyika? Ni kwamba katika mwaka wa fedha, kwa sababu huu ndiyo mwaka wa kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano, imani yangu ni kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja niwaombe sasa Waheshimiwa Wabunge, kwa umoja wetu na katika vikao vyetu vile vya kisheria, vikao vyetu vya Madiwani, hali kadhalika vikao vyetu vya *RCC,* jambo hili liwe kipaumbele ili mradi mwisho wa siku na sisi Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutakuwa tunakusanya mikakati yote ya mikoa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali za mikoa. Hata hivyo, katika hili hatutosita kwa sababu lengo letu kubwa ni kuhakikisha kwamba, kila mkoa unakuwa na hospitali yake ya mkoa na baadaye tunakuwa na hospitali za Kanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo katika swali la pili kwamba Busega hamna hospitali ya Wilaya, ni kweli na kwamba wanatumia hospitali ya Mkula kama ni hospitali teule, lakini bahati mbaya kibali bado hakijapatikana. Hivyo, tutawasiliana na wenzetu wa Wizara ya Afya, lengo kubwa ni kupata kibali, lakini hata hivyo mpango mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba kila wilaya inapata hospitali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekwenda mbali zaidi, kwa sababu sehemu zingine *coverage* ya Wilaya ndani yake kuna Halmashauri kadhaa. Sasa tunasema kwamba, ikiwezekana kila Halmashauri iwe na hospitali yake, kwa hiyo huo ndio mpango wa Serikali. Imani yangu kubwa ni kwamba, tutaungana na mpango huu wote kwa pamoja kusukuma juhudi za ukusanyaji wa kodi ili tupate fedha za kutosha, mwisho wa siku maamuzi yetu ya ujenzi wa Hospitali za Wilaya na Mikoa yaweze kufikiwa. Hivyo, Mheshimiwa Chegeni endelea na spidi hiyo hiyo, nadhani kila kitu kitakuwa sawasawa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazeee na Watoto.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda tu kuongezea majibu ya nyongeza kuhusu swali la pili la kibali cha Hospitali ya Mkula, kuwa *district designated* hospital, kwa ajili ya Wilaya ya Busega. Tayari Mheshimiwa Raphael Chegeni, Mbunge wa Jimbo hilo amewasilisha jambo hili Wizarani kwetu na amenikabidhi barua zake mimi mwenyewe hapa Bungeni juzi tu, hata siku tatu hazijapita, ili niweze kufuatilia suala hili. Namwahidi kwamba nitawakabidhi wataalam suala hili, ili waweze kufika maeneo ya pale Mkula, bahati nzuri napafahamu vizuri, wakafanye ukaguzi, wajiridhishe kama inakidhi vigezo na hatimaye Wizara ya Afya iweze kuipa kibali cha kuwa Hospitali Teule ya Wilaya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Maswa linafanana kwa ukaribu kabisa na tatizo la Wilaya ya Momba, kwa sababu Wilaya ya Momba haina hospitali ya Wilaya. Kipindi cha kampeni Mheshimiwa Rais alituahidi kutupatia majengo ya pale Chipaka yatumike kama hospitali ya Wilaya. Nataka kujua, je, Serikali ina mpango gani wa kutupatia majengo yale ili yatumike kama Hospitali ya Wilaya ya Momba? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Momba hatuna hospitali ya wilaya pale na siyo hospitali ya wilaya hata zile *infrastructure* za wilaya yenyewe, halmashauri hatujakaa vizuri. Momba kwa sababu ni eneo jipya, mkakati wetu ni kuweza kuimarisha, lakini kwa sababu kuna majengo tayari, kikubwa zaidi ni kwamba wataalam watatakiwa kufika pale kufanya *assessment* ya hayo majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri katika ziara yangu ambayo nitaanzia Mkoa wa Iringa kuanzia tarehe 17 vilevile nitafika na maeneo ya Momba. Nikifika Momba, nitaomba wanifikishe katika yale majengo. Lengo letu ni nini? Tubainishe jinsi gani wananchi wataweza kupata huduma hizi. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Juliana Shonza kwa juhudi kubwa anayofanya kwa ajili ya wananchi wa Momba. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Maswa ina majengo mazuri na yamekamilika, mojawapo ni jengo la upasuaji, lakini hakuna vifaa kwa ajili ya kazi hiyo ya upasuaji na wataalam; na kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne alifika hapo akaahidi kwamba vifaa vitakuja na wataalam Madaktari wawili wataletwa kwenye Wilaya ya Maswa. Sasa Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ahadi hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, baba mwenye nyumba akisema maana yake hiyo hoja imekwisha. Kama Rais amekuja ameshatoa ahadi hiyo, ndiyo maana nimesema jukumu kubwa ni kwa jinsi gani tutafanya katika utekelezaji. Sasa katika hili, nini tunachotaka kufanya? Tunataka kuangalia jinsi gani tutatumia fursa zote kwamba hospitali hii iweze kupata huduma. Hata hivyo, naomba niwaambie ndugu Watanzania kwa ujumla kwamba, sasa hivi Wizara ya Afya

tuna mradi mmoja mkubwa sana, ambao sisi Watanzania tunashirikiana na wenzetu wa Uholanzi, mradi wa shilingi bilioni zisizopungua 44.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu kazi yake kubwa itakuwa kuweka vifaa tiba katika hospitali zetu za kanda na hospitali za mikoa na kwa sababu Maswa kuna kipaumbele maalum, tutaangalia jinsi gani tutafanya eneo hili lipate vifaa tiba. Sambamba na kuweka kwamba wataalam waweze kupatikana ili mradi wananchi wapate huduma za upasuaji katika Hospitali ya Maswa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Doto Biteko, swali la nyongeza.

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru. Kiu ya wananchi wa Maswa ya kupandishiwa hadhi hospitali yao, kiu hiyo hiyo iko kwa wananchi wa Bukombe hasa wa Kata ya Uyovu, ambao kituo chao cha afya ni kikubwa sana na kinahudumia watu kutoka Wilaya za Chato, Biharamulo pamoja na Bukombe. Kinahudumia watu wengi zaidi kuliko hata Hospitali ya wilaya, kwa sababu chenyewe kinahudumia watu zaidi ya 82,000 wakati hospitali ya wilaya inahudumia watu 68,000 tu. Namwomba Mheshimiwa Naibu Waziri atusaidie wananchi wa Bukombe, atuambie tuna uwezo wa kupandisha Kituo cha Afya cha Uyovu ili kiwe hospitali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Biteko anafahamu, tulikuwa pamoja pale Geita katika uzinduzi wa hospitali na kuweka vifaa katika Hospitali ya Geita pale. Bahati nzuri nilipita katika eneo lake, jiografia yake kweli ina changamoto kubwa na wananchi lazima wapate huduma na kituo hiki cha afya anachokizungumzia amesema kinahudumia watu wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge sasa kwa uhodari wake uleule wa kutetea wananchi wake katika suala zima la maliasili ambapo namsikia mara nyingi zaidi na uhodari wake wa kutetea wananchi katika sekta ya afya na nakumbuka kwamba alileta malalamiko mpaka wataalam wake walihamishwa katika eneo la Jimbo lako na akasema Madaktari wamehama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe kupitia vile vikao husika vya mchakato wa upandishaji vituo vya afya kuwa hospitali ya Wilaya kuanzia katika *Ward C*, Baraza la Madiwani, halafu mwisho wa siku naamini ikienda katika Wizara ya Afya ambao wao kazi yao ni kuangalai, kama vigezo vikikidhi, hospitali hiyo inapandishwa. Nadhani hawatosita, namwamini Mheshimiwa Dkt. Kigwangala na dada yangu Ummy Mwalimu watakuwa tayari kuhakikisha kwamba, watu wa Bukombe wanapata hospitali yao kwa mujibu wa vigezo vitakavyokuwa vimefikiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini sasa aulize swali lake.

Na. 444

Mpango wa Kupandisha Hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere

MHE. DESDERIUS J. MIPATA aliuliza:-

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Namanyere imetimiza vigezo vyote vya kuwa Halmashauri ya Mji.

Je, ni lini Serikali itaipa hadhi ya kuwa Halmashauri ya Mji Mamlaka hiyo ya Mji mdogo wa Namanyere?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya kupandishwa hadhi Mamlaka ya Mji mdogo Namanyere kuwa Halmashauri ya Mji yameshapelekwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI baada ya kukamilika kwa vikao vya kisheria. Baada ya hatua hiyo, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itakwenda kuhakiki vigezo vinavyozingatiwa katika uanzishwaji wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati tunakamilisha taratibu za kisheria zinazotakiwa na kufanya uhakiki kabla ya maamuzi ya kuanzisha Halmashauri ya Mji kufikiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mipata, swali la nyongeza.

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Tunaposukuma uanzishwaji wa mamlaka hizi, tunataka kuharakisha maendeleo kwa wananchi. Mji wa Namanyere umekuwa na maombi haya muda mrefu na majibu yamekuwa ya namna hii hii, tangu Bunge lililopita majibu yamekuwa ni haya ya kusema kuna timu ya wataalam watakwenda kuhakiki ili majibu ya kuanzisha yapatikane. Nataka kujua kama Serikali inaweza ikatoa hasa tarehe maalum au *time frame* ili wananchi wajue hasa ni lini zoezi hili litakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, miji midogo mingi hapa nchini inaendelea kukuwa ikiwepo ile ya Chala, Kate ambako ni Makao Makuu ya Jimbo, Wampembe, Kipande na kwingineko, lakini mpangilio wake umekuwa si mzuri sana kutokana na Halmashauri kukosa fedha za kufanya utaratibu wa mipango ya uendelezaji wa miji hiyo. Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya ukuaji huu wa miji usioridhisha hapa nchini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mipata, anataka *time frame* ya lini jambo hili litakamilika. Mheshimiwa Mipata amekuja ofisini kwangu si chini ya mara mbili katika jambo hili na siyo Mipata peke yake na wadau mbalimbali wengine kutoka Lushoto, wengine kutoka maeneo mbalimbali kwa ajili ya jambo hili. Ndiyo maana nilisema hapa siku zilizopita kwamba, jambo hili kwa sababu limekuwa ni kilio cha Wabunge wengi, mpaka Waziri wangu akaagiza kwamba tulete *database* ya *status* ya kila maombi haya yamefikia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze, naweza nika-*table* hii *status* ya *database* mpaka kwa kaka yangu pale Ilula, mpaka kwa kaka yangu Profesa Majimarefu wote maombi yao yapo katika hili na hii chati yote iko hapa wataalam wetu tumewaagiza sasa jinsi gani watakwenda kufanya *assessment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba niseme, hapa katikati tumepata matatizo, kuna Halmashauri zingine zinaanzishwa kwa presha hata zile *GN* namba zinapotajwa zile *code* zinakosewa, zinapokosewa maana yake unaingilia katika mipaka ya Halmashauri nyingine. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mipata avute subira, sitaki kusema ni lini inaanza, lakini lengo letu kubwa ni kwamba, ndani ya kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha tunapoanza, imani yangu kwamba, hii kazi itakwenda kwa kasi kwa sababu hata mimi sipendi kila siku kusimama hapa kujibu swali hilo hilo. Kwa hiyo, imani yangu ni kwamba, jambo hili tutafikia mwisho, wenye kukidhi vigezo watakidhi na wale ambao watakuwa na upungufu wataambiwa wapi warekebishe ili mradi wapate mamlaka. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mipata avute subira.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine alizungumzia suala zima la mipangilio mibaya ya miji. Ni kweli sasa hivi ukiangalia hasa miji mingi inayokua, maeneo mbalimbali yanajengwa kiholela sana. Hata hii miji midogo, kwa mfano, ukienda hata pale Kibaigwa, eneo la karibu tu hapa, ukienda kuna ujenzi kama unatengeneza kachumbari vile, kitunguu, nyanya kila kitu yaani miji imekuwa hovyo hovyo kabisa. Ndiyo maana tunapopita katika Halmashauri zetu tumewaelekeza Maafisa wa Mipango Miji na Maafisa Ardhi, jukumu lao kubwa sio kuchukua mshahara wa Serikali tu na kukaa ofisini, japokuwa *resource* ni ndogo lakini wakitumia taaluma zao, tutafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani Afisa Mipango Miji au Afisa Ardhi yuko ofisini pale, nje ya Halmashauri palepale, lakini watu wanaendelea kujenga kiholela katika maeneo yasiyokuwa sawasawa. Tumetoa maelekezo kwamba Maafisa Mipango Miji na Maafisa Ardhi watumie *own source* zilizokuwepo, kuona jinsi gani watatumia taaluma yao kufanya mipango rafiki ya kijamii, angalau wananchi wetu waishi katika mipango bora. Kwa sababu ukitegemea kwamba utapata bilioni mbili (2) kwa wakati mmoja kupanga mipango miji, inawezekana itakuwa changamoto kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba nimwambie Mheshimiwa Mipata kwamba, tumeliona hili na tumeendelea kutoa maelekezo na kwa kutumia *platform* hii ya leo naomba niwaagize Maafisa Mipango Miji wote na nilishawaagiza Afisa Mipango Miji wa Bahi na Magu nilikopita kwamba, wahakikishe maeneo yao yote wanapokuwa Ofisini, yanakuwa maeneo rafiki yaliyopangwa vizuri kwa kutumia taaluma zao.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo Mji Mdogo wa Namanyere, katika Wilaya ya Geita kuna Mji Mdogo wa Katoro ambao una hadhi na umetimiza vigezo vyote. Napenda kujua sasa ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo huu wa Katoro utapandishwa kuwa Mamlaka ya Mji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kweli Mji wa Katoro unakua sana hasa katika eneo lile la Mkoa wa Geita. Kutokana na suala la Sekta ya Madini, hali ya miji imekuwa ikikua kwa kasi sana ukiwemo na mji wa Katoro. Kwa hiyo, nipendekeze tu kwa sababu katika *database* yangu hapa nikiangalia Mji wa Katoro siuoni, kwa hiyo Mheshimiwa Lolesia, kama walishaleta Ofisi ya Rais, TAMISEMI nitakwenda ku-*cross check,* lakini kama bado hawajaanza huo mchakato, naomba nielekeze sasa jinsi gani tutafanya katika eneo la Halmashauri yao, wahakikishe kwamba wanaanza mchakato wa kawaida kwanza katika Vijiji, katika u-*DC*, Baraza la Madiwani na baadaye *RCC,* yale maombi yaje Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tutayatathmini, mwisho wa siku ni kwamba, eneo hili litapandishwa kwa vigezo vitakavyokuwa vimefikiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Keissy, swali la nyongeza.

MHE. ALLY M. KEISSY: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri katika swali lake la kwanza alisema kwamba ana ziara ya Iringa, Mbeya na Songwe. Je, yuko tayari sasa katika hiyo ziara kuunganisha mpaka Wilaya ya Nkasi akajionee mwenyewe matatizo ya Afya, Elimu na Barabara katika Wilaya yetu ya Nkasi? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ziara yangu inaanzia Mkoa wa Iringa, nitakwenda Mkoa wa Njombe, Mbeya, Rukwa, nikitoka hapo nitakwenda Mkoa wa Kigoma halafu namalizia Mkoa wa Tabora, hiyo ni *phase* namba moja. Baadaye nitakwenda Mkoa wa Mara, Geita, Mwanza, Kagera, halafu nitarudia katika Kanda ya Mashariki. Kwa hiyo, Mheshimiwa Keissy mpo katika awamu ya kwanza ya ziara yetu kubaini changamoto ili kuona jinsi gani Ofisi ya Rais TAMISEMI, tutafanya kuwahudumia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dunstan Kitandula, swali la nyongeza.

MHE. DUNSTAN L. KITANDULA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa hali ya kukamilika kwa vigezo vya kupandisha hadhi miji yetu kule Namanyere iko sawa sawa na kule Maramba ambapo tumetimiza vigezo vya kupata mji mdogo tangu kabla Mkinga haijawa Wilaya. Je, ni lini Mji wa Maramba utapewa hadhi ya kuwa Mji Mdogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hawa wenzetu walikuwa na maombi yanayogusa sehemu mbili; walikuwa wanaomba hii Maramba iwe mji mdogo, lakini walikuwa wanaomba eneo hili la Mkinga. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge, nadhani maombi haya yamepita muda mrefu sana. Sasa nimwombe na nimwagize Mkurugenzi na timu yake kule Halmashauri wakishirikiana naye kwa sababu kulikuwa na maombi haya na muda mrefu sana umepita, waanze huu mchakato vizuri ilimradi itufikie Ofisi ya Rais, TAMISEMI, mwisho wa siku vile vigezo vikiwa vimefikiwa hatutosita kuhakikisha eneo hili linapandishwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimwagize Mheshimiwa Mbunge na wengine wote, maana yeye ni rafiki yangu tupo humu ndani. Namwambia Mkurugenzi na timu yake yote waanze huu mchakato sasa vizuri ilimradi hili jambo lifike Ofisi ya Rais, TAMISEMI na wataalam wetu waende kuhakiki kwa ajili ya vigezo hivyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala sasa aulize swali lake, kwa niaba yake Mheshimiwa Subira Mgalu.

Na. 445

Fedha za Maendeleo Kutotolewa kwa Wakati

MHE. SUBIRA K. MGALU (K.n.y. MHE. EZEKIEL M. MAIGE) aliuliza:-

Moja kati ya vikwazo vya utekelezaji wa Ilani ya CCM ni kutotolewa kwa fedha kwa ukamilifu na kwa wakati:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilikasimiwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala kwa mwaka wa fedha 2015/2016?

(b) Je, Serikali imetoa kiasi gani cha fedha za Miradi ya Maendeleo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Msalala hadi kufikia Desemba, 2015?

(c) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuhakikisha fedha za maendeleo zinapatikana kwa wakati na kupelekwa kwenye miradi husika?

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Masalala, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2015/2016, kiasi cha shilingi bilioni 4.1 kilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Desemba, 2015 Serikali imeshatoa kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Wilaya ya Msalala. Aidha, wahisani wametoa jumla ya shilingi bilioni 1.6 nje ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti ya Halmashauri hiyo kwa ajili ya miradi ya *TASAF*, *SEDP* na *AGPHAI* na kufanya fedha zote zilizopokelewa hadi Desemba, 2015 kufikia bilioni 3.1.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za miradi ya maendeleo zinapelekwa katika Halmashauri zote kulingana na makusanyo yanayofanyika. Mkakati uliowekwa na Serikali ni kuimarisha makusanyo ya mapato ya Serikali na kudhibiti upotevu wa mapato katika vyanzo mbalimbali ili kuhakikisha fedha zinapelekwa kama zilivyopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa kwa mujibu wa jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, ameonesha kuna bakaa ya fedha ambazo zimebaki hazijawasilishwa kwenye Halmshauri ya Wilaya ya Msalala, kiasi kwamba itapelekea miradi kutokamilika kwa wakati. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, anaweza kulihakikishia Bunge hili kabla ya mwaka wa fedha mpya haujaanza miradi ile itakamilika na Serikali itapeleka fedha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa swali la msingi limeelekeza changamoto ya upelekaji wa fedha za maendeleo ambalo ni changamoto inayoikabili karibu nchi nzima kwa mwaka huu wa fedha, hususani, Halmashauri zetu za Mkoa wa Pwani. Je, Naibu Waziri yupo tayari kutoa maelekezo kwa Wakurugenzi kwa miradi ambayo ni viporo hasa ya Sekta ya Afya, wawasilishe taarifa haraka ili Serikali iweze kuikalimisha katika Halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Pwani? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, bajeti pale mpaka mwezi Desemba, nimesema zilikuwa hazijafikia shilingi bilioni 3.1 zilizokuwa zimepelekwa, lakini mpaka mwezi Mei, hivi sasa fedha ambazo zimepelekwa katika ile bajeti imefika bilioni mbili (2), lakini fedha zingine za nje zimeongezeka na zimefikia karibu bilioni 1.9 mwezi uliopita. Kwa hiyo, jukumu kubwa ni nini? Tunaona kwamba kuanzia mwezi Desemba, mpaka hivi sasa kuna fedha nyingine za Serikali zimezidi kupelekwa na hapa maana yake Serikali itajitahidi kwa kadiri iwezekanavyo ili miradi iliyokusudiwa iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, isipokuwa katika hili, ni lazima wataalam wetu, wakati mwingine ule uwezo wa utumiaji wa fedha za miradi kwa watendaji wetu umekuwa ni udhaifu zaidi. Kwa mfano, hapa tunapozungumza fedha nyingi zimeshapelekwa kule Msalala, basi nawaomba watendaji wetu waweze kuhakikisha kwamba, fedha zilizofika za maendeleo zitumike ilimradi wananchi waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ni jinsi gani tutafanya kwa Mkoa wa Pwani. Kikubwa zaidi naomba niwaagize kama nilivyosema, ni kwamba Wakurugenzi wote wa Mkoa wa Pwani na mikoa mingine yote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wahakikishe kwambam kwanza wanaandaa zile changamoto zilizokuwepo katika Sekta ya Afya na miradi mingine, lakini tubainishe kwamba hata hizo fedha zilizofika ziweze kutumika kwa ajili ya maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba nitoe onyo kwa Wakurugenzi mbalimbali, kipindi cha mwaka unapofika siku hizi za mwisho, watu wamekuwa wakifanya mambo ya ajabu sana katika matumizi ya fedha za Serikali, wakijua kwamba mwaka unakwisha. Wakati mwingine fedha zinapelekwa sehemu ambazo hata zisizohusika, ambazo haziendi kuwagusa wananchi. Kwa mwaka huu naomba nikiri wazi kwamba, Mkurugenzi yeyote ambaye atacheza na fedha za Serikali, naamini Waziri wangu ataamua kuchukua fimbo kubwa sana kuhakikisha kwamba watu hawa wanawajibishwa. Lengo kubwa kuhakikisha wananchi wetu wanapata huduma kutokana na kazi kubwa inayofanywa na Serikali yao ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri, kumekuwana kisingizio kikubwa cha sababu ya ucheleweshaji wa fedha kwa kutokukamilika kwa miradi mingi na kupelekea wakandarasi kudai kwamba wanalipwa kidogo kidogo. Kwa mfano, miradi ya maji ambayo iko katika Kijiji cha Ipalamwa, Kitoho, Ilamba na sehemu nyingine. Sasa Serikali inasemaje, nani wa kuchukuliwa hatua, ni Halmashauri husika au Mkandarasi ambaye ameshindwa kumaliza mradi kwa wakati na ubora? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zinapelekwa kulingana na *certificate* ambayo mkandarasi ameiwasilisha Halmashauri na imefanyiwa tathmini na imewasilishwa Wizara ya Maji ndiyo tunapeleka fedha kulingana na kiwango cha uzalishaji ambacho Mkandarasi amezalisha. Kwa hiyo hapo, Wakurugenzi wanaagizwa kuwasukuma wakandarasi waweze kuzalisha zaidi ili Serikali iweze kutoa fedha zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kange Lugola, swali la nyongeza.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ucheleweshaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo limejitokeza kwenye Jimbo la Mwibara ambako Miradi ya Maji ya Bulamba, Kibara pamoja na maji ya Mji wa Bunda kutoka Nyabehu, zaidi sasa ya miaka saba, fedha bado zinacheleweshwa kwenda. Hili ambalo analisema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, lazima *certificate* zile ziandaliwe na zihakikiwe, sisi Halmashauri ya Wilaya ya Bunda kwa kushirikiana na *Engineer* ya Maji wa Wilaya, tulishasukuma sana hizi *certificate* na kuna mabarua mengi Wizara ya maji. Sasa je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataliambia vipi Bunge hili kwamba hata zile *certificate* ambazo zilishahakikiwa bado fedha haziendi, ni uzembe wa Wizara au ni uzembe wa mtu gani? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane moja kwa moja, aje ofisini kwa sababu sina taarifa kwamba kuna *certificate* ambayo haijalipwa. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametoa bilioni 15 na *certificate* zote zimelipwa, sina *pending certificate* ambayo imebaki kwenye ofisi ambayo haijalipwa. Kwa hiyo, kurahisisha kazi Mheshimiwa Mbunge, naomba awasiliane na mimi ili tuweze kuangalia ni nini kimetokea.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, sasa aulize swali lake.

Na. 446

Miradi ya Maji ya Manga na Mutulingara

MHE. DEO K. SANGA aliuliza:-

Miradi ya Maji Manga pamoja na Kijiji cha Mutulingara inasuasua tu mpaka sasa.

Je, ni lini miradi hii itapatiwa fedha ili iweze kukamilika?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Jimbo la Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maji ya Manga na Mutulingara, ni miongoni mwa miradi ya Vijiji 10 inayotekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Makambako. Kazi ya ujenzi wa Mradi wa Maji katika Kijiji cha Manga inaendelea na hadi kufikia mwezi Machi, 2016, utekelezaji wake ulifikia asilimia 90. Serikali tayari imemlipa mkandarasi kiasi cha shilingi milioni 235.08 kati ya shilingi milioni 491.9 anazodai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ujenzi wa Mradi wa Mutulingara, bado haujaanza kutokana na changamoto ya upatikanaji wa fedha. Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi huu katika awamu ya pili ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 992.8 kwa ajili ya miradi ya maji katika Halmashauri ya Mji wa Makambako.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sanga, swali la nyongeza.

MHE. DEO K. SANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwanza nianze sana kwa kumpongeza Rais John Pombe Magufuli, Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, pamoja na wataalam wa Wizara hii, kwa namna walivyotutengea bajeti ya Wizara ya Maji katika Halmashauri yetu ya Makambako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu wametutengea fedha nzuri, hasa ukizingatia za mradi mkubwa ule wa Makambako ambao kwa muda mrefu wananchi wa Makambako wamekuwa wakipata tabu sana juu ya kupatikana kwa maji. Anawaambia nini wananchi wangu wa Halmashauri ya Makambako, kwamba baada ya kutenga bajeti ile mwaka wa fedha unaanza keshokutwa, ili fedha zile ziweze kwenda kujenga mradi ule mkubwa lakini ukiwepo pamoja na Kijiji cha Kiumba, Mutulingara yenyewe pamoja na Ikelu na vijiji vingine ambavyo vimekosa maji. Ni lini sasa fedha hizi tulizozitenga zitakwenda? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, Makambako tuna Bodi ya Maji, kwa muda mrefu Halmashauri ilishapitisha majina ya kuja katika Wizara, mwaka mmoja na nusu sasa Bodi ya Makambako haijateuliwa katika vyombo vinavyohusika. Sijajua ni TAMISEMI au ni Wizara ya Maji. Je, ni lini sasa mtateua ili watu hawa waendelee kufanya kazi katika Bodi ya Mji wa Makambako?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge Sanga, ameshukukuru kwamba tumemtengea milioni 992.8, lakini anasema sasa nini kinafuata. Kinachofuata ni utekelezaji wa hiyo bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia mafaili, mwaka 2013 Wizara ilitoa mwongozo na ikatoa kibali kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri kwamba, baada ya kupata bajeti wanatakiwa kufanya taratibu za manunuzi na kusaini mikataba, lakini nakala ya mikataba walete Halmashauri. Hapo katikati kulitokea tatizo kidogo, tayari nimeshamwagiza Katibu Mkuu, aweze kutoa mwongozo mwingine, tutashirikiana pamoja na Hazina ili sasa utekelezaji wa hii bajeti ambayo imepitishwa, Waheshimiwa Wabunge, Wakurugenzi wa Halmsahauri wapewe mwongozo jinsi ya kufanya. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, kwamba suala hili tunalifanyia kazi, kwa ajili ya kutoa mwongozo kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la la uteuzi wa Bodi, tunatumia sheria namba 12 ya mwaka 2009. Zipo Bodi ambazo zinateuliwa na Wizara ya Maji, lakini zipo Bodi ambazo zinateuliwa na TAMISEMI. Kwa hiyo, hili

nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitalifuatilia ili tuweze kujua sasa nini kinafanyika na tuweze kuona ni wapi pamekwama Bodi yake haijateuliwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Ningependa sasa kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, katika Mji wa Lindi Manispaa, kumetokea tatizo la dharura kubwa sana katika wiki hii. Wananchi wamekosa maji, wanahangaika na visima ambavyo vilikuwa vinatoa maji pale Kitunda kuleta mjini, visima viwili pampu zimekufa na kisima kimoja kimebomoka. Wananchi wanahangaika sana, ningependa kujua Serikali itatusaidiaje ili ku-*solve* tatizo hili la maji, wananchi waweze kupata maji? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli muda mrefu tumekuwa tunapata matatizo kwa wananchi wa Mji wa Lindi kupata shida ya maji kutokana na *setup* ya miundombinu jinsi ilivyo. Kwa sababu visima viko ng'ambo ya pili vinazalisha maji, mabomba yanapita chini ya bahari, halafu yanaleta maji kwenye Mji wa Lindi, yakitokea mawimbi, yale mabomba yanakatika. Kwa hiyo, Mji wa Lindi unakosa maji na ndiyo maana Serikali ilikuja na mradi mkubwa ule wa Ng'apa ambao ukikamilika sasa matatizo katika Mji wa Lindi yatakuwa yamekwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa sina taarifa, lakini kwa taarifa hii, leo baada ya saa saba nitafuatilia ili kujua tunafanya nini na nitampatia majibu Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Tatizo la maji la Halmashauri ya Makambako linafanana kabisa na tatizo lililoko Halmashauri ya Nyang'hwale. Kumekuwa na miradi mingi ya usambazaji wa maji kutoka Ziwa Victoria, leo takribani miaka minne, miradi hiyo haisongi mbele kwa sababu ya ukosekanaji wa pesa. Je, Waziri anatuambia nini wananchi wa Nyang'hwale, kuhusu miradi hiyo kwamba itaendelea kwa kasi ili tuweze kupunguza tatizo la maji?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, ndiye ambaye amekuwa ananipa nyaraka nyingi kutoka kwenye Halmashauri yake na ndiye ambaye

alinikabidhi hata ile barua ambayo nilikuja kugundua kwamba mwaka 2013, Wizara ilitoa waraka kuhusu utekelezaji wa bajeti katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili tatizo la Nyang'hwale linafanana na maeneo mengine pia, inawezekana kuna matatizo pia katika Halmashauri ya Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa utaratibu tuliouweka sasa kama miradi ipo na uzalishaji upo, wakileta *certificate* tunalipa pesa; lakini tumegundua kuna maeneo ambayo uzalishaji umekwama kwa matatizo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Wizara ya Maji, tukishirikiana na Mheshimiwa Mbunge tutapeana taarifa, ili tuweze kuona ni nini kimekwamisha na kwa bahati nzuri tuko humu humu ndani kwenye Bunge. Nakumbuka Mheshimiwa Mbunge Lusinde kwake kulikuwa na shida, lakini tumeitatua na sasa hivi mradi unaendelea vizuri. Kwa hiyo, tupeane tu taarifa kuna tatizo gani ili tuweze kuiangalia Halmashauri. Pengine ndani ya Halmashauri kuna uzembe, tutauondoa ili kuhakikisha hii miradi inatekelezeka na hasa kwa kuzingatia kwamba sasa fedha inatolewa. Kwa hiyo, hakuna sababu kabisa kwa nini mradi usitekelezwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swali la nyongeza.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika Jimbo langu la Ulanga kuna mradi mkubwa wa maji wa Mahenge Mjini ambao tayari umeshakamilika. Tatizo la huo mradi umeshindwa kuanza kwa kuwa tu, Idara ya Maji haina mita za kuwafungia wateja, kwa kisingizio cha fedha zikipatikana, fedha zikipatikana. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa ili Idara ya Maji iwafungie mita wananchi wa Mahenge Mjini ili waanze kufaidi matunda ya Mbunge wao kijana machachari? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imetekeleza mradi na mradi ule umekamilika; kilichobaki ni mita. Sasa naomba anisaidie awasiliane na Halmashauri kuna tatizo gani, hatuna taarifa kwamba wana hilo tatizo la mita, watuletee taarifa. Hata hivyo, katika Mwaka huu wa Fedha tumemwekea bajeti, kwa nini wasiangalie hiyo bajeti ili wakaweza kufunga mita, halafu waendelee kupata mapato. Kwa sababu najua kwamba wananchi watakuwa wanapata maji, lakini tatizo Halmashauri haipati mapato. Kwa hiyo, kwanza Mheshimiwa Mbunge aangalie bajeti ambayo tumempatia, kama haitatosha, basi tuwasiliane ili tuweze kuliondoa hili tatizo la mita. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Franz Mwalongo.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niulize kwamba, kuna vijiji katika Kata ya Matola na Kata ya Uwemba katika Jimbo la Njombe Mjini; Kijiji cha Mtila na Kijiji cha Kilenzi. Vijiji hivi vinazalisha maji kwa ajili ya vijiji vya jirani kwa sababu vyenyewe viko juu ya mwinuko lakini vyenyewe kama vijiji havina maji kabisa. Je, Serikali iko tayari kutuchimbia visima virefu katika vijiji hivi viwili ili kusudi wananchi hawa wanaozalisha maji na kutunza mazingira waweze na wao kufaidi maji hayo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJ: Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu tu kwamba, Serikali ipo tayari, ndiyo maana imemtengea bajeti, ni suala la yeye Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri yake kuweka kipaumbele ili waweze kuhakikisha kwamba yale maeneo ambayo maji yanatoka, basi wao wawe wa kwanza kupata maji, waweke vipaumbele, wachimbe visima, watakapokuwa wamefikia, bajeti mwakani inaanza; huu ndio mwaka wa kwanza tunaanza na tutaendelea kutenga bajeti, kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Halima Bulembo.

Na. 447

Mradi wa Maji Wilayani Longido

MHE. HALIMA A. BULEMBO (K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE) aliuliza:-

Je ni lini mradi mkubwa wa maji Wilayani Longido utaanza rasmi, ambao utakuwa ni mkombozi kwa wananchi wote wa Wilaya ya Longido.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi mkubwa wa Maji Wilayani Longido ambao chanzo chake ni Mto Simba uliopo ndani ya hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, ulifanyiwa usanifu wa kina na kazi hiyo ilikamilika mwezi Machi mwaka 2015. Mradi umekisiwa kugharimu sh. 13,998,791,270.40 na utaweza kuhudumia watu 21,666. Serikali imepanga kujenga mradi huu na kuukamilisha katika awamu ya pili ya Program ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2016/2017, imetenga kiasi cha shilingi bilioni 4.61 kwa ajili ya kuendelea kukamilisha miradi ya Vijiji 10 katika Halmashauri ya Longido. Pia imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Longido.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Bulembo, swali la nyongeza.

MHE. HALIMA A. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa matatizo yaliyoko Longido yanafanana kabisa na ya mkoani kwangu Mkoa wa Kagera Wilaya ya Bukoba Vijijini, Kata ya Maruku na Kanyangeleko ambapo kumekuwa na mradi mkubwa wa maji uliojengwa tangu miaka ya 60 mpaka 70 na mradi huu uliweza kufanya kazi kwa miaka 10 na uliwahudumia wananchi wengi. Mradi huu tayari una vyanzo, una matenki, kinachohitajika katika mradi huu ni ukarabati. Je ni lini mtaukarabati mradi huu ili uweze kuwahudumia wananchi wa Bukoba Vijijini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze anasoma historia, mama huyu anawapenda wananchi wa Kagera na kwa sababu ni mama anahusika na kuchota maji, kwa hiyo uchungu wake anaujua. Amesoma historia miaka ya 60 na 70 kwamba mradi huu ulijengwa na kuwahudumia wananchi kwa muda wa miaka 10, lakini sasa hivi ni kwamba umechakaa unataka ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa hii na nimwagize Mkurugenzi wa Maji wa Kagera aweze kuangalia na Mheshimiwa Rweikiza ameshaniambia kuhusu mradi huu na nimeshawaagiza Wakurugenzi wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, waende wakauangalie mradi huu kuona unahitaji nini ili tuweze kuufanyia ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba katika awamu ya pili ya maendeleo ya sekta ya maji, tunataka kuhakikisha kwamba miradi yote ya zamani inafanyiwa utafiti na tunaikarabati ili iendelee kutoa huduma kwa wananchi kama ilivyokuwa inatarajiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

WAZIRI OFISI YA RAIS TAMISEMI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa majibu mazuri sana, yanayohusiana na masuala ya maji. Hata hivyo, nataka niongezee tu kwenye jibu hilo juu ya swali liloulizwa na Mheshimiwa Bulembo, ambaye amezungumzia juu ya miradi ya maji iliyojengwa miaka mingi na ilikuwa imefanya kazi kwa

ufanisi, lakini leo hii ama imechakaa, ama miundombinu yake haitoshelezi idadi ya watu iliyoongezeka ama vijiji vilivyoongezeka na kwa hivyo inashindwa kumudu na watu wanapata shida ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, kwa ujumla wetu, sisi ndio wenye Majimbo na tunatoka kwenye maeneo haya, kama miradi hii haitabainishwa na kuorodheshwa kwenye mipango ya Halmashauri ya kila mwaka, siyo rahisi sana Serikali ikaweza kuitekeleza. Serikali inaamua mambo yake na kupanga na kuyatekeleza kupitia kwenye bajeti. Sasa kama haisomeki kwenye bajeti siyo rahisi kuiona na hata mimi ambaye kwa kushirikiana na Wizara ya Maji tunatekeleza miradi mbalimbali, kwa namna ambavyo tunaletewa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, jambo la kwanza ni kuiweka kwenye mipango ya maendeleo au ya kwenye bajeti, ikisomeka hivyo inakuwa rahisi kuiona, lakini pia kuitengea fedha na kuikarabati miradi hii. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, kwenye bajeti inayokuja, miradi yote ile iliyochakaa muiweke kama kipaumbele cha miradi ya kukarabatiwa, siyo miradi mipya, miradi ya kukarabatiwa, ili Wizara ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Maji tuweze kukaa na kuona kama tuje na mpango gani, au *program* gani ili tuweze kuitekeleza miradi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na kwa kuwa natoka pia katika Mkoa wa Arusha, pamoja na Mkoa huu wa Arusha kuwa na vyanzo vingi vya maji, vinavyotoka katika Mlima Meru, lakini maji haya yameonekana kuwa na madini ya *fluoride* na madini haya ya *fluoride* siyo mazuri sana. Je, Serikali inafanya jitihada gani, kuhakikisha kwamba inapunguza madini haya ya *fluoride? (Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Mji wa Arusha katika vile visima ambavyo vinatumika kutoa maji katika Mji wa Arusha, kuna visima ambavyo vimeonekana vina kiwango kikubwa cha maji ya *fluoride* na visima hivyo viko Mianzini viko viwili. Tulipunguza kiwango cha utoaji maji katika hivyo visima na tukachimba visima vingine viwili ili ku-*balance* ile *fluoride* isiwe kwa kiwango kikubwa; ni kwamba *fluoride* inatakiwa katika mwili wa binadamu lakini kiwango kisiwe juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hilo suala tayari tumeshalifanyia kazi kwa ku-*balance*, *fluoride* yake siyo nyingi sana kiasi ambacho ukiichanganya na maji mengine, basi inaingia katika viwango vile vinavyokubalika. Pia

naomba kumweleza Mheshimiwa Mbunge Mollel ni kwamba sasa hivi Arusha tuna mradi mkubwa, tunatarajia kuchimba visima 30 ili kuhakikisha kwamba kiwango cha maji katika Mji wa Arusha baada ya miaka miwili kukamilisha huo mradi, ambao tumepata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na *financial agreement* imeshasainiwa, tatizo la maji tutakuwa tumelimaliza kabisa katika Mji wa Arusha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Juma Nkamia, swali la nyongeza.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja tu la nyongeza. Mji wa Dodoma ni Mji unaokua kwa haraka sana na leo tunategemea asilimia mia moja ya maji kutoka katika visima vilivyoko pale Mzakwe. Moja kati ya juhudi zilizokuwa zimebuniwa na Serikali ni pamoja na kutengeneza bwawa la Farkwa, ambalo litaleta maji hapa Dodoma kupeleka Bahi, Chemba na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri awahakikishie Watanzania na wananchi wote wa Dodoma, kwamba ni lini mradi huu wa bwawa la Farkwa utaanza kujengwa kwa sababu sasa hivi tayari wananchi wameshaambiwa wasiendeleze nyumba zao na miradi yao mingine wakisubiri ujenzi uanze. Naomba Mheshimiwa Waziri atuhakikishie ni lini bwawa hili litaanza kujengwa na lini wananchi wataanza kulipwa fidia?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nkamia, kwanza umeuliza swali mara mbili lakini naona kama kuna maswali matatu.

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Naibu Spika, basi unisamehe tu kwa leo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Nkamia.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba sasa hivi maji tunayoyapata tunayapata kutoka visima vya Mzakwe, lakini Serikali tayari imeishafanya upembuzi yakinifu, na usanifu wa kina kuhusiana na ujenzi wa bwawa la Farkwa. Sasa hivi Serikali inachofanya ni kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili ili kuhakikisha kwamba Mji wa Dodoma sasa hautakuwa na matatizo ya maji. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala hili tunalitekeleza katika *Program* ya pili ya Maendeleo ya Sekta ya Maji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Emanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mamlaka ya Maji ya

Tabora Mjini *(TUWASA)* ina matatizo makubwa ya malimbikizo ya madeni zaidi ya bilioni mbili ambayo inawadai Taasisi za Serikali na hasa majeshi yetu na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema katika majibu yake ya msingi kuna pesa zimetengwa kulipa katika miradi mbalimbali. Je, ni lini Mamlaka ya Maji Tabora watalipwa pesa zao ambazo zinawafanya sasa wasifanye kazi kwa ufanisi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, madeni ya maji ambayo Taasisi za Serikali zinadaiwa katika mwaka wa fedha zitalipwa moja kwa moja kwenye Fungu la Hazina. Kwa hiyo, tutakapoanza kutekeleza Bajeti hii ambayo mmeipitisha tutaangalia tuweze ku-*manage* fedha zile, tuweze kulipa kwenye mamlaka husika ili waweze kuendelea kutoa huduma za maji. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Mmasi, swali fupi la nyongeza.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa upande wa Dar es Salaam na hususani kwa Jimbo la Kawe, ni dhahiri kwamba tumekuwa na changamoto za maji. Changamoto hizi zinatokana na kodi kubwa inayowekwa kwenye madawa ya kutibu maji, pamoja na kuhifadhi maji.

Pia tumekuwa na tatizo la miundombinu chakavu kwa upande wa *DAWASA* na vile vile tumekuwa na bajeti isiyokidhi mahitaji ya suala zima la upatikanaji wa maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Je, Serikali imejipangaje katika kutatua changamoto za maji, kwa Jimbo la Kawe zaidi sana pale Boko, Tegeta na Bunju. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, mradi wa mkubwa wa maji kutoka Ruvu Chini umekamilika na sasa hivi maji yameongezeka sana katikaJiji la Dar es Salaam. Tatizo tulilokuwa nalo ni ule mtandao. Tunao ule mtandao wa zamani ambao ni chakavu, kazi ya ukarabati inaendelea. Pia tayari tuna mkandarasi ambaye anafanya mtandao mpya maeneo hayo ya Kawe kwenda Bunju mpaka Bagamoyo, baada ya muda siyo mrefu maeneo yale upatikanaji wa maji utaongezeka sana. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge na suala la kodi ya *VAT* kwenye madawa ya maji, Serikali imeshakubali kuondoa kodi ya *VAT* kwa hiyo, tunatarajia bei ya maji itapunguzwa kwa sababu itakuwa ni kigezo cha kupunguza bei maji wakati gharama za kununua madawa yale zimepunguzwa.

Mheshimiwa Mbunge uwe na imani kwamba baada ya muda siyo mrefu bei ya maji itapungua, lakini pia upatikanaji wa maji utaongezeka katika Jiji la Dar es Salaam.

NAIBU SPIKA: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Hassan Elias Masala Mbunge wa Nachingwea, sasa aulize swali lake.

Na. 448

Umuhimu wa Kuendeleza Kambi ya Ukombozi *Farm* 17

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Nachingwea ni miongoni mwa Wilaya chache zilizo na historia ndefu katika kusaidia nchi nyingi za Afrika kupata uhuru; kwani wapiganaji wengi wa nchi hizo walihifadhiwa kwenye Kambi ya Ukombozi *Farm* 17 iliyopo Nachingwea:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhifadhi na kuendeleza maeneo ya Kambi ya *Farm* 17 hata kama yamegeuzwa kuwa Sekondari ili kuwa maeneo ya kihistoria na kuweza kuwavutia watalii?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzishawishi nchi zilizonufaika na Kambi ya *Farm* 17 kama Msumbiji na Zimbabwe ili ziangalie kwa karibu kambi hiyo kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu muhimu zilizopo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO – (K.n.y WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala Mbunge wa Jimbo la Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa *Farm17* ni miongoni mwa maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika katika harakati za ukombozi. Serikali kwa kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo Sanaa na Vijana imeanzisha mradi ujulikanao kama *Road to Independence* kwa lengo la kutunza kumbukumbu za historia ya ukombozi wa Bara la Afrika ikiwemo *Farm* 17. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa itashirikiana na Wizara hiyo katika kuhakikisha kuwa eneo hili linatunzwa ipasavyo ili kuvutia watalii

wakaolitembelea. Aidha, tunapenda kuushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kusaidia shule ya sekondari *Farm* 17 kuendeleza uhifadhi wa miundombinu ya kihistoria iliyopo shuleni hapo ili kutunza historia hiyo muhimu ya ukombozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haina mpango wa kuzishawishi nchi zilizopata hifadhi ya wapigania uhuru hapa nchini, kusaidia juhudi za uhifadhi wa maeneo hayo kwani nchi zenyewe zina hiari ya kuona umuhimu huo kwani lengo la Serikali ilikuwa ni kusaidia harakati za ukombozi kwa nchi husika.

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza;

Swali langu la kwanza ninataka tu nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, hii *project* ya *Road to Independence,* nimepitia bajeti zote za Wizara ya Ulinzi, nimepitia bajeti ya Wizara ya Utamaduni, sijajua kama anaweza akaweleza wananchi wa Nachingwea ni kipindi gani haswa inaenda kutekelezwa hii *program* ili tuweze kujua kwa sababu miundombinu ya eneo lile bado inaendelea kuharibika mpaka sasa hivi tunavyozungumza, ikiwemo eneo ambalo ameisha Mheshimiwa Samora Machel.

Swali la pili ambalo ninapenda kuuliza, ni nini kazi za Mabalozi wetu katika nchi hizi ambazo zilinufaika na maeneo haya, ukienda Msumbiji leo hii kuna Chuo Kikuu kinaitwa Nachingwea University kinapatikana pale Msumbiji. Je, hawaoni umuhimu wa kushirikisha Balozi zetu na nchi zilizohusika kuweza kusaidia maeneo haya ili kuweza kuweka kumbukumbu za Viongozi ambao waliishi katika maeneo haya? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri maswali ni matatu naomba ujibu mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Masala.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nitatoa utangulizi kwamba historia ya ukombozi wa Bara la Afrika haiwezi kutenganishwa na ushiriki mahiri na wa kujitoa wa nchi yetu Tanzania. Haiwezi kutenganishwa na uwepo wa Viongozi mashuhuri kama Mwalimu Julius Kambarage Nyerere lakini pia na Viongozi wengine wa Bara la Afrika kama kina Nkwame Nkurumah na hao wapiganaji wenyewe wakina Samora Machel wakina Robert Mugabe na wengine. Kwa maana hiyo, hii historia japokuwa ni chungu na japokuwa ni ngumu hatuna sababu ya kusema tunaweza tukadharau kutunza maeneo ambayo historia hiyo inayathamini, kwa maana hiyo eneo hili la Nachingwea ambalo Mheshimiwa Mbunge analizungumzia litapewa kipaumbele kwenye *program* hiyo ya *Road to Independence* ambayo nimeizungumzia hapa. *Program* hii kama anavyosema kwenye bajeti haionekani, naomba mimi na

yeye tushirikiane kwa pamoja baada ya kikao hiki cha Bunge kufanya utafiti kwenye vitabu vya bajeti ili tuone ni wapi haswa bajeti hii ya *Road to Independence* inapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana usiwe mradi ambao unatokana na bajeti ya ndani ukawa ni mradi ambao pengine una ushirika wa hawa wabia anaowasema wakiwemo wafadhili wa maendeleo ama Vyuo Vikuu ambavyo vinapenda kufuatilia historia ya ukombozi wa Bara la Afrika.

Swali la pili, kwamba hatuoni kama Balozi zetu zinaweza zikashirika nchi hizo, Tanzania tulikuwa na jukumu kubwa tu ambao tulijitolea kulibeba la kutafuta ukombozi wa Bara la Afrika na kuwapa nyumba na makazi, mafunzo, chakula na malazi zaidi ya wapiganaji kutoka nchi zaidi ya 12 za Afrika zilizokuwa zinapambana na ukoloni na kwa maana hiyo, hiyo ni heshima ya kipekee ambayo sisi tuliipata kupata wapiganaji wa ukombozi kwenye nchi zao kuja kukaa katika nchi yetu. Heshima hiyo tunaendelea kuipata leo na mwaka jana Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitunukiwa heshima ya kipekee pale AU kwa kupewa jengo la *Peace and Security* katika Mkutano wa Marais wa Afrika na hivi tunavyoongea hapa katika watu watatu mashuhuri wa Bara la Afrika ambao wanatambuliwa na wamewekewa alama za kipekee pale Addis Abba kwenye Makao Makuu ya AU ni pamoja na Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, wengine wakiwa ni Nkwame Nkurumah na mwingine akiwa ni Nelson Mandela.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Tanzania itaendelea kuwapokea na kuwapa ushirikiano wapiganaji wote ambao wanapenda kuja Tanzania kwenye maeneo waliyowahi kuishi kama vile kufanya hija na kukumbukia siku ambazo walikuwepo hapa nchini wakipigania uhuru wa nchi zao, ambazo sasa zimekuwa huru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anajibu kwa niaba kwa hiyo, tusijetukajikuta kwenye miongozo wa majibu kwa mujibu wa Kanuni ya 46 nadhani tukubaliane kuendelea Waheshimiwa. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe sasa aulize swali lake.

Na. 449

Utaratibu wa Kusambaza Mbolea ya Ruzuku

MHE. JORAM I. HONGOLI aliuliza:-

Serikali Awamu ya Nne ilianzisha utaratibu wa mbolea za ruzuku ili kuwasaidia wakulima wasio na uwezo wa kununua pembejeo waweze kuzipata na kuboresha kilimo:-

(a) Je, Serikali haioni kama inapoteza fedha nyingi kusambaza pembejeo hizo kupitia mawakala ambao mahali pengine hupeleka mbolea kidogo au wanawasainisha wakulima vocha bila kuwapa mbolea kwa kuwapatia shilingi 5,000 - Shilingi 10,000 na baadaye kurejesha mbolea mahali pengine;

(b) Je, kwa nini Serikali isisambaze mbolea hizo kupitia Kamati za Ulinzi na Uslama kuliko hao Mawakala ambao siyo waaminifu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joram Ismael Hongoli, Mbunge wa Lupembe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa wako baadhi ya mawakala na watumishi wa Serikali wasiowaaminifu ambao huwarubuni wakulima ili kukiuka utaratibu wa utoaji wa ruzuku uliowekwa kwa manufaa ya mawakala na watumishi wao. Wizara yangu inafanya ufuatiliaji wa karibu na kuwachukulia hatua za kisheria wahusika hao kwani huwakosesha wakulima pembejeo na hivyo kudumaza maendeleo ya sekta kilimo nchini. Aidha, ili kuondoka na mfumo huu Wizara yangu imeunda kikosi kazi cha kupitia gharama za uzalishaji na uagizaji wa pembejeo nchini ili kama kuna uwezekano kuondoa baadhi ya tozo na kodi ili kufanya pembejeo hizo zipatikane kwa bei nafuu. Sambamba na hilo viwanda vya kuzalisha mbolea vinatarajiwa kujengwa hapa nchini katika Wilaya za Kilwa na Kibaha, mategemeo yetu ni kuwa uzalishaji utakapoanza bei ya mbolea itakuwa nafuu kwa wakulima wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa mbolea za ruzuku umekuwa ukifanywa kwa ushirikiano wa sekta binafsi na Serikali. Makampuni ndiyo yenye mitaji na dhamana ya kuuza pembejeo hizo kwenye mpango wa ruzuku. Serikali inatoa vocha kwa mkulima ambayo ni hati punguzo ya kupunguzia mkulima makali ya bei ya pembejeo. Kwa utaratibu wa sasa Kamati za Pembejeo za Wilaya chini ya Uenyekiti wa Wakuu wa Wilaya, zimepewa jukumu la kusimamia

mgawo na usambazaji wa pembejeo katika maeneo yao. Hata hivyo, uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wamekuwa wakialikwa katika vikao vya Kamati ya Pembejeo za Wilaya ili kusaidia katika mikakati ya kudhibiti upotevu na ubadhirifu wa vocha za pembejeo.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na maswali mawili.

Swali la kwanza, kwa kuwa vocha hizi zimekuwa zikichelewa kuwafikia wakulima na wakati mwingine zimefika wakati wakulima wameshapanda mazao yao au wameshakuzia mazao yao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba mbolea hizi zinafika mapema ili kabla hawajaanza maandalizi ya mashamba haya ikiwezekana ziwe zimeshafika?

La pili, kwa kuwa mbolea hizi za ruzuku zimekuwa zikitolewa kwa wakulima wa mazao ya chakula pekee, Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa mbolea za ruzuku kwa wakulima wadogo hasa wa mazao ya biashara kama vile chai ili waweze kuongeza uzalishaji na hatimaye waweze kuongeza kipato chao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema kwamba kwa utaratibu wa sasa pembejeo zinachelewa sana kwa wakulima, nimfahamishe tu Mheshimiwa mbunge kwamba katika mwaka ujao wa fedha Wizara yangu inaubadilisha utaratibu mzima wa kupeleka ruzuku kwa wananchi. Kwa hiyo, tunategemea kwamba changamoto kama hizi kuhusu ucheleweshaji wa pembejeo hautatokea tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusu mpango wa Serikali wa kutoa ruzuku kwa pembejeo kwa ajili ya wakulima wote zaidi tu ya wale wanaofanya kilimo cha mazao ya chakula hususan mahindi na mpunga. Nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba ruzuku ya pembejeo hutolewa vilevile katika mazao mengine ikiwemo kwa mfano Korosho, Pamba, Kahawa, kwa kutumia taratibu za mifuko kwa ajili ya mazao hayo na vilevile kuna utaratibu wa kuhakikisha kwamba pembejeo vilevile zinatolewa katika zao la chai. Kwa hiyo, utaratibu huu vilevile unatayarishwa na Mheshimiwa Mbunge atapata taarifa pindi itakapokamilika.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Katika maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba ruzuku ya pembejeo pia inapelekwa kwenye zao la pamba. Mheshimiwa Waziri unajua kwamba mpaka leo hakuna ruzuku yoyote inayopelekwa kwenye zao la pamba, kwenye mbolea pamoja na mbegu?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia ruzuku katika zao la pamba linatolewa kwa utaratibu tofauti na ule unaotolewa katika mahindi na mpunga. Kwenye zao la pamba ruzuku inatolewa katika mbegu, kwa hiyo, niko tayari kuongea na Mheshimiwa Mbunge tujaribu kupitia yale ambayo yeye anayafahamu kuhusu hili lakini nimfahamishe tu kwamba kuna ruzuku inatolewa lakini ni katika utaratibu ambao ni tofauti kidogo. Kama nilivyosema mazao mengine kama kahawa, korosho vilevile ruzuku inatolewa lakini mara nyingi ni kwa kupitia mifuko maalum ambayo imeundwa kwa ajili ya mazao hayo. Lakini niko tayari kuongea naye tuangalie kuhusu hili.

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Kwa kuwa, Wilaya ya Lushoto ni ya wakulima wa mbogamboga na matunda hasa maeneo ya Mkuzi, Kishangai, Boeloi, Ubili, Lukozi, Baga na Mazumbai na wakulima hawa hawapati ruzuku za pembejeo. Je, Serikali ina mpango gani sasa kuwapatia wakulima hawa pembejeo ili na wao waweze kunufaika kama wakulima wengine wa nafaka?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kama tulivyosema kwamba siyo mazao yote hupata ruzuku, nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba mpango wa kutoa ruzuku ambao umeanza kwa muda sasa kuanzia mwaka 2003 umekuja kwa sababu ya kufanya mambo makuu matatu:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa chakula, lakini vilevile kujaribu kuwafanya na kuwahamasisha wakulima waweze kutumia mbolea na mbegu bora.

(ii) Kuwasaidia wakulima ambao wana kipato cha chini kuweza kuongeza tija. Tumeanza na baadhi ya mazao kama nilivyosema kwa sasa Serikali inatoa ruzuku na pembejeo kwenye mazao makuu mawili katika maana ya Mpunga na mahindi lakini vilevile kwenye yale ya biashara kupitia bodi zao lakini pale tutakapoona kwamba inafaa tutaendelea kuongeza utaratibu wa kupatikana kwa ruzuku kwa mazao yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba nilieze Bunge lako Tukufu kwamba lengo la kutoa ruzuku siyo kufanya wakulima wawe wategemezi lengo ni kuwafanya wao waone umuhimu wa kutumia pembejeo. Kwa hiyo, kama wakulima wenyewe wanauwezo wa kujinunulia pembejeo bila kupata ruzuku

ingefaa zaidi kwa sababu ni utaratibu ambao ni endelevu. Hata hivyo, tuko tayari kuangalia kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge kuangalie uwezekano wa baadhi ya mazao hasa haya amesema ya mbogamboga kama kuna umuhimu wa kutoa ruzuku.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mnapiga kelele sana na Waheshimiwa Wabunge ambao mmesimama hamuulizi maswali tafadhali kaeni kwenye *seat,* zenu ama ukienda kwenye kiti cha jirani yako kaa kwenye kiti cha jirani ndiyo uongee naye msimame mnaongea kwa muda mrefu. Tunaendelea Mheshimiwa Margaret Sitta.

MHE. MARGARET S. SITTA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo;

Kati ya kero zinazowakabili wakulima, mojawapo ni hii ya upatikanaji wa mbolea na bei yake wakiwemo wakulima wa tumbaku. Je, ni lini Serikali itaondoa kodi na tozo mbalimbali zinazoifanya mbolea ipatikane kwa gharama kubwa, tukiamini kwamba zikiondolewa kodi hizo na tozo mbalimbali mkulima atapata nafuu ya mbolea na pembejeo zingine na kwa msingi huo ataweza kulima zaidi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba tozo na kodi mbalimbali zinachangia gharama ya pembejeo hususan mbolea kuwa kubwa. Nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali imefanyia marekebisho baadhi ya tozo hizo na kodi kama mlivyosikia wakati Waziri wa Fedha anawasilisha bajeti, tayari kuna marekebisho kwenye baadhi ya tozo za zao la korosho lakini vilevile pamba na tunaendelea taratibu kuboresha katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwafahamishe tu Waheshimiwa suala la kodi haliwezi kuwa ni suala la siku moja kwa sababu ni lazima mijadala ifanyike miongoni mwa wadau wa setka mbalimbali vilevile kodi ni suala la uchumi huwezi kuondoa zote kwa siku moja, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaendelea kuzifanyia kazi taratibu ili hatimaye kuwe na mazingira ya kikodi ambayo hayamuumizi mzalishaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, tatizo lingine linalosababisha bei ya mbolea kuwa kubwa ni kwa sababu tunaagiza kutoka nje, nimpe habari njema kwamba kwa sasa kuna mikakati ya kujenga viwanda viwili vikubwa vya mbolea nchini; moja kitajengwa Kibaha na kingine kitajengwa Kilwa. Tunaamini kwamba uzalishaji wa mbolea ukifanyika nchini kwetu itakuwa ni rahisi zaidi wakulima kupata mbolea kwa bei ambayo ni nafuu.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Fedha na Mipango; Mheshimiwa Susan Chogisasi Mgonokulima Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya.

Na. 450

Mfumo wa *EFDs*

MHE. NEEMA W. MGAYA (K.n.y. MHE. SUSAN C. MGONOKULIMA) aliuliza:-

Mfumo wa mashine za *EFDs* hauchanganui kwa uwazi fedha ipi ni mapato ya kodi na ipi ni faini au ni gharama za uendeshaji:-

Je, ni lini kutakuwepo ushirikishwaji kati ya waandaaji mfumo wa *TRA* na viongozi wa wafanyabiashara ili kodi inayotozwa iwe halali na isiwe inayoua mitaji ya wafanyabiashara?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Chogisasi Mgonokulima, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa matumizi ya mashine za kutunza hesabu za kodi za kielektroniki ulianzishwa kwa lengo la kurahisisha na kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za biashara za walipa kodi. Mfumo wa *EFD* ulianzishwa ili kupata ufumbuzi wa matatizo ya utunzaji kumbukumbu za mauzo na utoaji wa risiti za mauzo zinazoandikwa kwa mkono. Mfumo huu umerahisisha usimamizi na ukadiriaji wa kodi kwa kuwa kumbukumbu zote za mauzo na manunuzi huhifadhiwa na kutunzwa kirahisi kwenye mashine za *EFD* na taarifa za mauzo ya mlipa kodi hutumwa kwenye *saver* ya Mamlaka ya Mapato moja kwa moja kwa njia ya mtandao kupitia mashine husika ya *EFD* kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa *EFD* haukuundwa kwa ajili ya kutoa mchanganuo wa fedha kwa mapato ya kodi, faini au gharama za uendeshaji wa biashara. Mfumo wa *EFD* ni kwa ajili ya kutunza kumbukumbu sahihi za mauzo na manunuzi ya mfanyabiashara pamoja na kutoa risiti. Mchanganuo wa mapato ya kodi na gharama za uendeshaji hufanywa kwa njia ya kawaida ya kiuhasibu kwa kutumia kumbukumbu za mauzo na manunuzi ya biashara zinazotunzwa katika mashine za *EFD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ina jukumu la kukadiria, kukusanya na kuhasibu mapato ya Serikali yanayotokana na kodi, ada, na tozo mbalimbali pamoja na kusimamia sheria zote za kodi zilizotungwa

na kupitishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango ina utaratibu wa kushirikisha wadau mbalimbali wakati wa maandalizi ya bajeti ambao hutoa michango yao na ushauri kwa kupitia kikosi kazi yaani *task force* kilicho chini ya Idara ya Sera ambacho kazi yake ni kuchanganua maoni na ushauri uliotolewa na kuainisha mambo muhimu ya kuingiza katika bajeti ya Taifa. Utaratibu huu hutoa fursa kwa viongozi wa wafanyabiashara na wengine kutoa maoni na ushauri ili ufanyiwe kazi na kuingizwa katika mipango ya Serikali. Hakuna kodi inayotozwa kwa nia ya kuua mitaji ya wafanyabiashara wetu, kwani kiwango cha juu cha kodi ya mapato ni asilimia 30 ya mapato baada ya kuondoa gharama za biashara yaani *net profit*. Pale ambapo mfanyabiashara hakupata faida, hakuna kodi ya mapato itakayotozwa. Hivyo basi, kodi zinazotozwa na Mamlaka ya Mapato ni halali na haziui mitaji ya wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka kujua ni lini Serikali itasambaza mashine za *EFD* katika Mikoa yote ya Tanzania, ili mwananchi aweze kulipa kodi kihalali na kuweza kulipatia Taifa mapato? *(Makofi)*

Swali la pili; kuna changamoto katika mtandao, changamoto hii ya mtandao inapelekea kukatika kwa mawasiliano kati ya mashine hizi na *TRA*. Mfano mnunuzi yupo kituo cha mafuta X akiwa safarini kuelekea Mkoa Y na ikatokea kuna changamoto hiyo, je, mnunuzi anatakiwa afanyeje ikiwa juzi tu tumepitisha sheria kwamba lazima mtu achukue risiti? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nilithibitishie Bunge lako Tukufu kwamba nia ya Serikali yetu ni kusambaza mashine hizi nchi nzima. Kama tunavyofahamu jambo lolote lina gharama na mashine hizi pia zina gharama, kwa sasa Serikali imeanza kugawa mashine hizi za *EFD* katika Mkoa wa Dar es salaam kwa wafanyabiashara wadogo wenye mauzo ghafi kati ya shilingi milioni 14 hadi milioni 20. Katika awamu ya kwanza Wizara yangu imepanga kugawa mashine za *EFD* 5,703 na mpaka leo tayari wafanyabiashara 118 wameshachukua mashine zao. Naomba pia niwashajihishe wafanyabiashara wote wa Dar es salaam ambao waliainishwa kuchukua mashine hizi sasa waende wakachukue mashine, kama ambavyo tumesikia kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwamba mashine hizi zipo lakini wafanyabiashara hawataki kujitokeza kwenda kuchukua mashine

hizi. Nawaomba wafanyabiashara wafike na wachukue mashine hizi katika Mamlaka yetu ya Mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili la Mheshimiwa Neema ameuliza changamoto katika mtandao. Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba Serikali yetu pia imefanya jitihada ya kusambaza mkongo wa Taifa nchi nzima. Kwa hiyo, changamoto hii ya mtandao naamini haina muda mrefu itafika mwisho na pia naomba niseme na niwaombe wafanyabiashara, wamekuwa wakisingizia changamoto ya mtandao kumbe hakuna tatizo la mtandao. Naomba niwaambie ni vizuri wakaweza kutumia sasa fursa hii ya kuenezwa kwa mkongo wa Taifa na kuweza kutumia mashine hizi katika kutoa risiti pale ambapo wanauza au wanatoa huduma yoyote kwa wananchi. Nimekuwa nikiongea na wafanyabiashara nikiwauliza swali na Waheshimiwa Wabunge naamini ninyi ni mashahidi nani amewahi kufika katika mabenki ya biashara akaambiwa mtandao upo chini, hakuna. Kwa hiyo, hii pia ni danganya toto ya wafanyabiashara, naomba niwaambie sasa Serikali tumeingia vizuri na tunaanza kazi kila mmoja aweze kutoa risiti hizi za mashine ya *EFD*.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Richard Mbogo

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kupata taarifa za wafanyabiashara ili waweze kulinganisha na maandalizi ya kumbukumbu zao za hesabu. Sasa katika uhasibu kuna marekebisho ya kiuhasibu, inatokea mtu anatoa kitu kinaitwa *credit note* au *debit note* ili kufanya masahihisho. Lakini kwa sasa mfumo huu wa *electronic signature device* hauchukui marekebisho ya kiuhasibu. Je, ili kuondoa hali ya sintofahamu na kulinganisha kumbukumbu za *TRA* na wafanyabiashara, Serikali ipo tayari kubadilisha mfumo wake na kuingiza hizi *credit note* au *debit note* katika marekebisho ya kiuhasibu ili ziweze kusomeka katika mtambo wa *TRA* na kurahisisha kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi; lengo la mashine hizi ilikuwa ni kupata taarifa na kumbukumbu sahihi za wafanyabiashara na mauzo yao, lakini kama kuna jambo lolote ambalo litaweza kuboreshwa zaidi Serikali yetu iko wazi kabisa, naomba tushirikiane ili tuweze kuhakikisha kumbukumbu zote zinaingia katika mfumo huo. Kwa sasa, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba tumeanza na hizo kumbukumbu za mauzo na mapato ya wafanyabiashara ila haya mengine yote pia tunaendelea kuboresha mfumo wetu, nina imani kubwa yote yataingizwa kwenye mfumo huu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kandege.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo.

Kwa kuwa, katika swali la msingi suala zima linaloongelewa ni juu ya elimu na faida inayotokana na faida na ulipaji wa kodi. Kwa kuwa tumekuwa mashuhuda katika baadhi ya miradi ambayo inatekelezwa tukipata fedha kutoka kwa wafadhili nikitolea mfano wa barabara iliyojengwa kutoka Tunduma kwenda Sumbawanga unakuta kuna vibao ambavyo vimeandikwa kwamba pesa hii imetokana na walipa kodi wa Marekani.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kwa ile miradi ambayo inakamilishwa kwa pesa ya ndani, vikawekwa vibao ili kuhamasisha ulipaji wa kodi kwamba miradi hii inatokana na ulipaji kodi ya Watanzania? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, nilidhani Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi anasimama lakini naona hana mpango. Vile vibao ni ninyi mnahusika au ni watu wa *TANROADS*? Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, tafadhali.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazo zuri na tutalichukua na tutalifanyia kazi. Hili ni jambo jema nafikiri. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Sawa, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii, ninapenda kuuliza swali dogo la nyongeza.

TRA wanafanya kazi nzuri, lakini katika baadhi ya maeneo *TRA* hawa hawana ofisi; kwa mfano katika Wilaya ya Kasulu, Wilaya kubwa ya kibiashara, Wilaya ya mpakani *TRA* haina ofisi. Sasa ningependa kujua kupitia kwako je, wenzetu wa Wizara ya Fedha mna sera ipi ya kujenga ofisi za *TRA* katika maeneo hasa yale ya kibiashara ili mapato ya Serikali yaendelee kuongezeka.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, *TRA* imekuwa ikifanya uchambuzi wa mwenendo wa biashara na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika Wilaya na Mikoa ya nchi yetu ili kuweza kuamua mahali ambapo panatakiwa patangulie katika kujenga ofisi za Mamlaka ya Mapato, ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Kasulu ambapo tumekuwa na mazungumzo na

Mheshimiwa Nsanzugwanko na yeye ametuahidi kwamba atatupatia hata kiwanja. Tumemuahidi kwamba tupo tayari sasa kujenga Ofisi ya *TRA* katika Mji wa Kasulu. Vivyo hivyo kwa Wilaya nyingine tunaendelea taratibu, tutaanza na zile ambazo gharama zetu za kupata mapato zinakuwa ni ndogo zaidi kulinganisha na mapato. Lakini dhamira yetu ni kuwa na Ofisi ya *TRA* katika nchi nzima. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: tunaendelea Waheshimiwa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani; swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Dimani Zanzibar naomba sasa swali la Mheshimiwa Yussuf 451 lijibiwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir umesema Chambani au Dimani?

MHE. ALI HAFIDH TAHIR: Nimesema Chambani

NAIBU SPIKA: *Hansard* iweke kumbukumbu sawa sawa.

Na. 451

Suala la Raia Kupigwa na Kuharibiwa Mali Zao

MHE. HAFIDH ALI TAHIR (K.n.y. MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN) aliuliza:-

Suala la raia kupigwa na kuharibiwa mali zao kwa upande wa Zanzibar limekuwa likiongezeka siku hadi siku;

Je, Serikali inatambua tatizo hili na kama inatambua inachukua hatua gani?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mbunge wa Chambani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba kila inapofika wakati wa Uchaguzi Mkuu hasa katika kisiwa cha Pemba baadhi ya watu hujichukulia sheria mkononi kwa kuwapiga wengine na kuharibu mali zao. Aidha, Serikali itaendelea kuongeza vikosi vya ulinzi na usalama katika maeneo

yote tete na kuhakikisha utii wa sheria bila shuruti unazingatiwa. Pia Serikali itaendelea kuelimisha wananchi madhara ya kujichukulia sheria mkononi dhidi ya wengine wasio na hatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nitoe wito kwa wananchi wote kuacha mihemko na itikadi za kisiasa wakati na kabla ya uchaguzi kwani hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, umedaiwa kodi nini na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango hapo kuhusu sauti? Nadhani uongeze sauti kidogo, Waheshimiwa hawajakusikia vizuri. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir swali la nyongeza.

MHE. HAFIDH ALI TAHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana pamoja ya kuwa sauti ilikuwa ndogo lakini nashukuru sana majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumzia suala la wakati wa kampeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kampeni ya uchaguzi na baada ya uchaguzi kule Zanzibar nyumba ya Kamishna wa Polisi ilichomwa moto, lakini mikarafuu mingi kule kisiwani Pemba ilikatwa, mazao machanga nayo yaliharibiwa.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na mambo yote yaliyotokea haya hivi sasa umechukua hatua gani ya kukomesha vitendo kama hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sababu hivi sasa kuna mambo mengi yanatokea na kwa kuitikia wito wa Rais Magufuli ambaye amesema sasa hivi uchaguzi umekwisha tunataka maendeleo.

Je, utawachukulia hatua gani wale ambao watatekeleza ukorofi katika siasa badala ya kuleta maendeleo ndani ya Tanzania? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir anataka kujua kwamba ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu ambao wamevunja sheria baada ya uchaguzi, akataja matukio mawili *specifically,* moja linahusu kurushwa bomu kwenye nyumba ya Kamishna na mambo ambayo yamekuwa yakijitokeza siku za karibuni ya ukataji mashamba ya mikarafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimjulishe tu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir kwamba mpaka sasa hivi Polisi imeshafanya kazi ya kuwakamata

watuhumiwa, mimi binafsi juzi nilifanya ziara na nilikuatana na Viongozi wa Polisi Zanzibar pamoja na Makamanda wa Polisi wa Mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba. Dhamira ya ziara ile ni kuweza baada ya kupata taarifa mbalimbali ambazo tumekuwa tukizipata kila siku juu ya hatua ambazo tunachukua, lakini kujionea wenyewe jinsi hatua hizo zilivyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema ni kwamba mpaka sasa hivi kuna watuhumiwa kadhaa wameshakamatwa na katika watuhumiwa waliokamatwa ni matukio mawili ambayo yamefikishwa Mahakamani, matukio mengine bado kesi zao zipo kwa *DPP*. Nilijaribu kutoa wito kwa *DPP* kuweza kufanya kazi kwa karibu kabisa na Polisi ili kuharakisha kesi hizo ili watu hao waweze kuchukuliwa hatua kali za kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili ambapo alitaka kujua kwamba baada ya kauli ambayo ameizungumza Mheshimiwa Rais, nataka nisisitize kwamba Jeshi la Polisi ndiyo chombo pekee chenye dhamana ya kuweza kutathmini hali ya usalama katika nchi yetu. Kama ambavyo imefanya kupitia Kamishna wake wa *operation* walitoa agizo kwamba kulingana na hali ya usalama nchini wamezuia mikutano ya kisiasa. Nataka nitoe wito tu kwamba wananchi ama vyama vya siasa vitii agizo hilo la Polisi, kama kuna yeyote ambaye hatii agizo hilo basi sheria ichukue mkono wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumewahi kuzungumza mara nyingi hapa kwamba hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria, kwa hiyo basi tunataka na mamlaka husika, kwa maana ya kwamba viongozi wa Jeshi la Polisi wa ngazi za chini wahakikishe kwamba wanatekeleza maelekezo ya ngazi za juu. Kwa hiyo, watu ambao wanahusika kutoka vyama vya siasa watii sheria hiyo, lakini watu ambao wanapaswa kuisimamia sheria hiyo waisimamie ipasavyo katika maeneo yote ya nchi yetu ikiwemo Pemba, Zanzibar na maeneo ya Tanzania Bara mpaka pale mamlaka husika ama Jeshi la Polisi watakapoamua vinginevyo kwa mujibu wa taarifa zao za ki-intelijensia na taratibu zao za kazi na utaalam ambao wanao.

MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba watachukuliwa hatua kali za kisheria wale wote walioshiriki vitendo hivi, lakini pia kuna wengine ambao tayari sasa hivi wameshakamatwa, yaani watuhumiwa wameshakamatwa, je, Serikali itakubaliana nami kwamba baada ya kugundulika watu hawa waliofanya vitendo hivi kwa raia wa Zanzibar, Serikali iko tayari pamoja na hatua kali zitakazochukuliwa za kisheria, iko tayari kuwataka walipe fidia kwa wale wote waliowafanyiwa vitendo hivi?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na uamuzi wa hatua gani za kuchukua baada ya kubainika na makosa ni maamuzi ya Mahakama. Kwa hiyo, pale ambapo Mahakama itaamua kulingana na sheria za nchi yetu basi nadhani ndivyo ambavyo inapaswa kutekelezwa. Siyo jukumu la Jeshi la Polisi kuamua hukumu gani ambayo watuhumiwa hawa wachukuliwe.

MHE. MUNIRA MUSTAFA KHATIBU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wanaoathirika zaidi ni wanachama wa CCM kwa kule Pemba; Je, Serikali haioni umuhimu wa chama hiki cha *CUF* kukifutia usajili na kuweza kupata amani ndani ya Tanzania yetu? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa upande wa Pemba matukio haya, wakati wa uchaguzi wa marudio na baada ya uchaguzi kumalizika, Pemba kulikuwa na amani, ambapo mpaka sasa hivi amani ipo. Matukio haya ya kihalifu ya kukatakata mikarafuu na kufanya mambo mengine ya hovyo zaidi yalijitokeza baada ya viongozi wa *CUF*, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alivyosema, kufanya ziara kule Pemba. Ndiyo maana nikasisitiza kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha kwamba wanachukua sheria kali kwa Kiongozi yeyote wa chama chochote kiwe cha *CUF* au chama kingine ambacho kinahatarisha ama kinachochea amani ya nchi yetu.

Kuhusiana na suala la kukifutia usajili chama hiki nadhani hayo ni mamlaka ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuona kama kuna haja hiyo kulingana na taratibu na sheria za nchi yetu zilivyo. Si jukumu la Serikali ama Jeshi la Polisi kuamua.

MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOSS NYIMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, toka tumalize Uchaguzi Mkuu Zanzibar imekuwa na baadhi ya watu wakitoa kauli za vitisho, hususan wakati huu wa sikukuu wanatoa kauli za vitisho kupitia mitandao ya kijamii;

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Zanzibar, hususan vijana na watoto ambao wanatarajia kusherehekea sikukuu ya Eid al-Fitr.*(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachoweza kuwaeleza wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla ni kwamba wasiwe na wasiwasi wowote, nchi yetu iko salama na itaendelea kuwa salama. Ninyi ni mashahidi kwa kazi nzuri ambayo imekuwa

ikifanywa na Jeshi la Polisi. Kwa matukio ya hivi karibuni jana na juzi mmejionea. Pia kwa upande wa Zanzibar juu ya hawa watu ambao wanajaribu kutaka kutuletea mrafaruku katika nchi yetu, tumewadhibiti. Nataka nitoe tu wito kwa wananchi kuacha kukubali kuchochewa na baadhi ya wanasiasa, wahakikishe kwamba wanaendelea kufuata sheria za nchi yetu, yeyote ambaye atakiuka sheria hiyo kama ambavyo tumekuwa tukizungumza kila siku, kwamba ikiwa ni mwanachama wa chama cha siasa, ikiwa ni kiongozi basi hatua kali za kisheria zitachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nisisitize tu kwamba wananchi wasiwe na wasiwasi, waendelee kusherehekea siku ya Eid-al-Fitr bila wasiwasi wowote. Serikali yao ipo itaendelea kuwalinda wao pamoja na mali zao.*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo.

Tangazo la kwanza ni la wageni waliotufikia asubuhi ya leo. Tunayo makundi mawili, wageni wa Waheshimiwa Wabunge, naona leo wageni wa mafunzo hawapo japokuwa tangazo limeonekana kama lina makundi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na mgeni wa Mheshimiwa Selemani Jafo, ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, na huyu ni Mwalimu Rashid Tebe kutoka Morogoro, karibu sana. Tunao pia wageni wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, ambao ni wanafunzi 18 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Edwin Mkumbo, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani ambaye ni Naibu Waziri wa Nishati na Madini, wakiongozwa na ndugu Bathlomeo Manunga ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, karibuni sana.

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni familia yake, na hawa wameongozwa na ndugu Neema Mlangi ambaye ni Dada wa Mheshimiwa, Dada ameongozana na watoto wa Mheshimiwa Allan Kiula ambao ni Joseph Allan, Joan Allan na Abraham Allan, hawa wote ni watoto wa Mheshimiwa Allan Kiula.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 28 wa Mheshimiwa Oran M. Njeza ambao ni Maafisa Elimu Kata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, hapa wameishia Mbeya lakini nadhani ni Mbeya Vijijini, wakiongozwa na ndugu Haroun Tende ambaye ni Mwenyekiti wa Maafisa hao, karibuni sana. Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Danstan Kitandula ambaye ni mtoto wake na huyu ni Luka Danstan Kitandula, karibu sana. Pia wageni wanne wa Mheshimiwa

Josephine Chagula ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana.*(Makofi)*

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambaye ni mwanariadha bingwa wa zamani wa Taifa, na huyu ni Ndugu Nzaeli Kiomo, karibu sana. Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud Ali Khamis ambao ni familia yake kutoka Zanzibar, Mkoa wa Magharibi, ambao ni wafuatao: Ndugu Abubakar Masoud Ali ambaye ni mtoto wake, Ndugu Fatma Masoud Ali na Ndugu Ibrahim Masoud Ali, hawa wote ni watoto wake, wameambatana na shemeji yake ambaye anaitwa Ndugu Rahma Hassan Said, karibuni sana.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 46 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao wapo kwenye makundi mawili kama ifuatavyo; wageni sita kutoka Mpanda wakiongozwa na Ndugu Stephano Asalile ambaye ni Mwenyekiti wa Vijana wa Wilaya ya Mpanda, karibuni sana. Tunao pia wageni 40 ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. Tunao pia wageni 40 wa Mheshimia Felista Bura ambao ni walimu watatu na wanafunzi 37 kutoka Shule ya Tumaini English Medium – Kisasa, ambayo iko Mkoani Dodoma, karibuni sana wageni wetu.*(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na matangazo mengine. Kuna tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa Ibada ambaye ni Mheshimiwa Anna Lupembe, na anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wa makanisa ya *CCT* kwamba, wanatakiwa kuhudhuria ibada katika jengo la Pius Msekwa leo siku ya Jumanne tarehe 28 Juni, 2016, mara baada ya kuahirishwa shughuli za Bunge. Aidha, Mtumishi Laizer wa Kanisa Kuu KKKT atashiriki ibada hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho ni mwaliko wa futari kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge wanawake. Leo tarehe 28 Juni, 2016, tangazo linatoka kwa Mheshimiwa Naibu Spika, ameandaa futari kwa ajili ya Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote katika hoteli ya Morena leo. *(Makofi/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, ubaguzi…

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ninawakumbusha kila siku, nikiwa nimesimama mtu mwingine asiongee. Sawa, nadhani mlikuwa mnashangilia lakini tangazo mmelisikia, Hoteli ya Morena leo baada ya kuahirisha shughuli za Bunge baada ya saa 12 jioni, Wabunge Wanawake. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo yetu kwa leo, tunaendelea, Katibu.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SIKA: Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mwongozo.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako chini ya kanuni ya 68 (7). Wakati Mheshimiwa Munira anauliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani juu ya vitendo ambavyo vinafanywa na Chama cha *CUF,* vitendo ambavyo vinaathiri maisha ya watu pamoja na mali, na akauliza ni kwa nini chama hicho, kutokana na vitendo hivyo kisifutiwe usajili. Mheshimiwa Naibu Waziri akasema kwamba suala hilo liko chini ya Msajiri wa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelazimika kuomba mwongozo huu kwa sababu kuna wakati ambapo sisi tunaamini Serikali yetu inawajibika kwa pamoja. Msajili wa Vyama vya Siasa hayuko humu ndani ambaye tunaamini sehemu ya Serikali. Kwa nini Wizara ambayo inahusika, ambayo huyu Msajili anafanya kazi chini ya Wizara hiyo hataki kusimama na kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Munira juu ya kufuta usajili wa Chama cha *CUF* ambao wanaendesha vitendo kule pemba, na hasa vinaathiri sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi kwa kusababisha mauaji pamoja na mali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wako, ni sahihi Bunge hili kutopata majibu wakati Serikali ya Chama cha Mapinduzi iko humu ndani, ni sahihi?

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo!

NAIBU SPIKA: Mwongozo, Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), sina haja ya kuisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata shida kidogo juu ya pale ambapo Waziri husika hayupo na maswali yanajibiwa kwa niaba ya Waziri mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, napata shida kwa sababu Kanuni ya 4(4) inatoa ruhusa ya maswali ya nyongeza matatu. Lakini limetokea tukio leo Naibu Waziri wa Wizara ya Afya akijibu maswali kwa niaba ya Wizara ya Ulinzi hatukuweza kuruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza na hata kipindi cha nyuma ilishatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 45(3) kiti chako kina mamlaka, kama majibu hayajaridhisha unaweza ukaelekeza majibu yakaletwa baadaye. Vilevile Kanuni ya 46(3) inaelekeza Waziri Mkuu, Mwanasheria Mkuu au Waziri

mwingine anaweza akaweka majibu ya nyongeza. Sasa naomba mwongozo wako, Je, tuboreshe Kanuni kwamba Waziri husika asipokuwepo basi maswali ya nyongeza yasiwepo, au la kwa Kanuni zilizopo Serikali iweze kujibu? Kwa sababu Mawaziri wako wengi hapa na wengine wamepitia Wizara mbalimbali wanaweza wakajibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miongozo miwili, mmoja Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, mwongozo mwingine umeombwa na Mheshimiwa Richard Mbogo. Nianze na Mwongozo wa Mheshimiwa Richard Mbogo.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka mwongozo huu ulipata kuombwa hapo nyuma, na uliombwa na Mheshimiwa Richard Mbogo, kuhusu maswali ya nyongeza pale ambapo mimi nilikuwa nimetoa maekezo kwamba Waziri anapokuwa anajibu kwa niaba ya Waziri wa Wizara nyingine kuhusu maswali kujibiwa kikamilifu. Waheshimiwa Wabunge tukaenda kwenye Kanuni ya 46, nikaeleza wakati huo kwamba mtakuwa mashahidi maswali mengi yamekuwa yakiulizwa hapa, hata ya Waziri mwenyewe mwenye dhamana hiyo, nikiombwa mwongozo na nikitoa mwongozo kwamba maswali hayo yajibiwe upya.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 44 niliitolea maelezo wakati huo, lakini kwa sababu wakati pengine sikuisoma na kwa hivyo pengine Waheshimiwa Wabunge hatukuelewana vizuri ilimaanisha nini. Kanuni ya 44(1) inasema, "maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mbunge yeyote kwa madhumuni ya kupata ufafanuzi zaidi juu ya jambo lolote lililotajwa katika jibu lililotolewa". Yanaweza kuulizwa.

Nadhani nilitoa maelezo marefu kipindi hicho, ambayo pengine sina haja ya kuyarudia kwa kirefu leo. Lakini kimsingi ni kwamba Kanuni ya 44(1) ambayo nimeisoma haijasema ni lazima.

Baada ya kusema hayo, fasili ya pili inasema hivi, "Mbunge anayeuliza swali la msingi ataruhusiwa kuuliza maswali ya nyongeza yasiyozidi mawili, na Mbunge mwingine yeyote atakayepewa nafasi ataruhusiwa kuuliza swali moja tu la nyongeza". Maana yake ni nini? Mbunge mwenye swali la msingi ataruhisiwa, maana yake lazima aruhusiwe, mwenye swali lake la msingi. Mbunge mwingine anategemea nafasi, lazima apewe nafasi ndipo aweze kuuliza swali la nyongeza. Maana yake ni kwamba ikiwa Spika au Kiti hakikutoa hiyo nafasi Mbunge ambaye hana swali la msingi hawezi kupewa nafasi hiyo.

Kwa hiyo Kanuni hii tuilewe tu vizuri. Ninapotoa yale maelezo ya ziada ningeweza pia kunyamaza na kusema Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Lakini katika ule ustaarabu tuliouanzisha humu ndani nalazimika kutoa maelezo hayo ili wote twende pamoja, usione kwa nini Waziri mwingine anaulizwa maswali mengi, mwingine haulizwi kabisa. Kwa hiyo ni mazingira hayo ili wote tuende vizuri, ndiyo maana nalazimika kutoa yale maelezo ya ziada. Lakini Kanuni ya 44 Waheshimiwa Wabunge, mtu ambaye Kiti kinalazimika kumpa maswali ya nyongeza ni mwenye swali lake la msingi.

Maswali ya nyongeza ni fursa ambayo Kiti kinatoa. Ndiyo maana katika Kanuni, fasili ya (2) inasema, "Mbunge mwingine atakayepewa nafasi." Maana yake ni kwamba, usipopewa nafasi, huwezi kuuliza na huwezi pia kushitaki kwa kutokupewa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ndiyo mwongozo wangu kuhusu maswali ya nyongeza. Kwa ujumla wake, maswali ya nyongeza, huu ndiyo mwongozo wangu.

Vile vile nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola kuhusu swali la nyongeza la Mheshimiwa Munira Mustafa Khatibu, ambaye alikuwa akimwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; na hoja yake ya msingi ilikuwa kuhusu Watanzania wanaoishi Pemba hasa wa Chama cha Mapinduzi kwamba wanapata taabu kwa vitendo wanavyofanyiwa na wananchi ambao ni wanachama wa Chama cha *Civic United Front, (CUF)*. Katika kuuliza swali lake wakati akijenga hoja, alionesha kana kwamba Chama hiki kwa nini kisifutiwe usajili kama kinaleta taabu? Kwa sababu ni Chama cha Siasa.

Mheshimiwa Waziri wakati akijibu swali hilo, alionesha kwamba Jeshi la Polisi linafanya juhudi katika matendo yale yanayoonesha ni ya uvunjifu wa amani, lakini katika jibu lake akaongeza maelezo kuhusu ufutaji wa Vyama na kwamba yeye asingeweza kufuta Chama ama kusema kuhusu kufuta Chama kwa sababu majukumu hayo amepewa Msajili wa Vyama.

Waheshimiwa Wabunge kwa mwongozo aliyouomba Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola anaonyesha kwamba Serikali ipo humu Bungeni na kwa namna nyingine pia hata Msajili wa Vyama vya Siasa na yeye ni sehemu ya Serikali. Kwa hiyo, Waziri yeyote hapa angeweza kutoa maelezo ni namna gani hili linaweza kufanywa.

Waheshimiwa Wabunge, niwasihi mnipe muda nikaipitie hiyo Sheria ya Vyama vya Siasa nione namna nzuri ya kuutoa huu mwongozo uliyoombwa na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola. Kwa maana hiyo, kwa mujibu wa Kanuni hiyo hiyo ya 68 (7) mwongozo unaweza kutolewa papo hapo au baadaye. Kwa

hiyo, mwongozo wa Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola nitautoa hapo badaye. *(Makofi)*

Katibu!

NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI: Miswada ya Sheria ya Serikali. Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016 *(The Public Procurement (Amendment) Bill, 2016),* kusomwa mara ya pili.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016
(The Public Procurement (Amendment) Bill, 2016)

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma *(The Public Procurement Amendment Act, 2016)* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Kamati ya Bunge ya Bajeti chini ya uwenyekiti wa Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo kwa kuchambua kwa kina na kutoa ushauri kuhusu namna ya kuuboresha Muswada huu ili kuboresha ununuzi katika Sekta ya Umma na kuwezesha Serikali kupata ubora wa thamani iliyokusudiwa, yaani *value for money*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekeozo mazuri ya Kamati. Hivyo, Serikali itaendelea kufanyia kazi mapendekezo mengine ya Kamati kwa lengo kusimamia kwa ufanisi ununuzi katika Sekta ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa maoni na ushauri waliotoa wakati wa semina ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu marekebisho ya Muswada yanayopendekezwa iliyofanyika hapa Dodoma terehe 18 Juni, 2016. Napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba ushauri na maoni yao kwa kiwango kikubwa yamezingatiwa na mengine yataendelea kufanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee namshukuru pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Mbunge kwa kuandaa Muswada huu pamoja na marekebiso yake, wadau mbalimbali katika Sekta binafisi, Taasisi za Serikali na wananchi kwa ujumla ambao kwa nyakati tofauti waliotoa ushauri wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ushauri na maoni ya Waheshimiwa Wabunge, Muswada huu kwa kiwango kikubwa umezingatia mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo wafanyabiashara ambao ni Wazabuni, Taasisi mbalimbali binafsi na Taasisi za Serikali. Baadhi ya Taasisi zilizowasilisha maoni ni pamoja na Tume ya Kurekebisha Sheria, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Wakala wa Barabara Nchini, Bodi ya Makandarasi Tanzania, *TANESCO, TCCIA* na *TANROADs*. Wadau hawa walishirikishwa katika hatua tatu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza Wiraza ya Fedha na Mipango iliandaa mkutano wa wadau ambao waliwasilisha mapendekezo mbalimbali ya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410. Pili, Tume ya Kurekebisha Sheria ilikusanya maoni ya wadau mbalimbali kwa njia ya maandishi na mahojiano ya ana kwa ana na kundaa taarifa. Taarifa husika iliwasilishwa kwa wadau kwa ajili ya kuboreshwa na hatimaye kukabidhiwa kwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye aliiwasilisha taarifa husika kwa Waziri Fedha na Mipango kwa ajili ya maandalizi ya Muswada huu. Tatu, Kamati ya Bunge ya Bajeti iliitisha mkutano wa wadau tarehe 26 Juni, 2016 ili kupata maoni yao ambapo Wizara ya Fedha na Mipango ilishiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi ya Umma wa mwaka 2016 una lengo la kuongeza ufanisi katika ununuzi wa Umma na kuondoa upungufu uliopo katika sheria ya sasa kwa kupunguza gharama na muda wa mchakato wa ununuzi, kutoa upendeleo kwa makampuni ya ndani, vikundi maalumu, malighafi na bidhaa zinazozalishwa nchini, kuweka viwango mahususi kwa bidhaa zitakazotumiwa na Serikali na kuruhusu ununuzi wa bidhaa na huduma moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Madhumuni ya Muswada; itakumbukwa kwamba, Sheria ya Ununuzi Umma Na. 7 ya mwaka 2011 ilianza kutumika rasmi mwezi Desemba, 2013 baada ya kufutwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Namba 21 ya mwaka 2004. Tangu kuanza kutumika kwa Sheria hii kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinoathiri usimamizi na ufanisi katika ununuzi wa Umma. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, bei ya bidhaa na huduma zinazonunuliwa na Serikali kuwa za juu ikilinganishwa na bei ya wastani wa soko

na hivyo kuongeza gharama za Serikali katika ununuzi. Hali hii inachangiwa na kuwepo kwa sharti linalozuia kufanyika kwa majadiliano hususan bei kati ya Taasisi nunuzi na mzabuni aliyeshinda zabuni hususan zabuni zinazohusisha mzabuni zaidi ya mmoja. Hali hii imeisababishia Serikali gharama kubwa ya ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni muda mrefu wa michakato ya ununuzi ambao unaathiri kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa miradi mbalimbali. Kwa mfano, zabuni za ushindani wa Kimataifa kwa ajili ya kupata mshauri mwelekezi huchukuwa takaribani siku 211 kukamilika wakati mchakato wa zabuni ya ushindani wa Kitaifa hutumia wastani wa siku 174. Vile vile, zabuni za ushindani wa Kimataifa kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa huchukuwa takribani siku 100 kukamilika wakati zabuni za ushindani Kitaifa hutumia siku 91.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, gharama kubwa zinazotokana na matangazo ya zabuni, michakato ya ufunguzi wa zabuni, tathimini ya zabuni, vikao vya Bodi ya Zabuni, majadiliano ya Zabuni na ukaguzi na upokeaji wa bidhaa zitokanazo na Zabuni, ambapo michakato hii huambatana na gharama za vikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni kutokuzingatiwa kwa viwango za bidhaa na huduma zinazopaswa kutumika katika Ofisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi nunuzi zimekuwa zikifanya ununuzi pasipo kuzingatia viwango vya mahitaji zilivyoidhinishwa na Serikali, yaani *approved standard,* mfano majengo, magari samani, vifaa vya ofisi na kadhalika. Hali hii imesababisha ugumu katika uratibu, ununuzi, usimamizi, udhibiti na matengenezo ya vifaa vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, ni kutokuwepo kwa upendeleo katika ushiriki wa Zabuni kwa makundi maalam katika jamii kama vile wanawake, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala muhimu yaliozingatiwa katika Muswada huu ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Kuondoa sharti la Kisheria linalozuia majadiliano ya bei katika zabuni kati ya Taasisi nunuzi na Mzabuni ili kupata unafuu wa bei, tofauti ilivyo hivi sasa ambapo kupitia Kifungu cha 76 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 7 ya mwaka 2011, majadiliano ya mkataba wa zabuni hayaruhusiwi kuhusisha masuala ya kupunguza bei katika Zabuni za Ununuzi au kuongeza bei katika Zabuni za Uuzaji wa mali za Serikali hususan endepo mchakato wa zabuni umehusisha mzabuni zaidi ya mmoja.

(b) Kupunguza muda wa michakato ya ununuzi kwa kurekebisha vifungu vya sheria na kanuni vinavyochangia urefu wa michakato ya ununuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kupunguza muda wa mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli kutoka siku 28 zilizobainishwa katika kifungu cha 96 (4) cha sheria ya sasa hadi siku saba zinazopendekezwa kwenye Muswada. Pamoja na kupunguza muda wa Afisa Masuuli kutoa uamuzi kuhusu malalamiko kutoka siku 14 zilizobainishwa katika Kifungu cha 96 (6) cha sheria, ambapo Muswada unapendekeza maamuzi kufanyika ndani ya siku saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kupunguza muda wa kuwasilisha rufaa kwa Mamlaka ya Rufaa ya Zabuni kutoka siku 14 zilizobainisha katika Kifungu cha 97 (2) cha sheria ilivyo hivi sasa hadi siku saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, aidha, baada ya Bunge kuupitisha Muswada huu, Waziri wa Fedha atarekebisha kanuni zilizopo hivi sasa kwa lengo la kupunguza muda wa mchakato wa Zabuni za Ununuzi wa Bidhaa, Kandarasi za ujenzi na huduma kutoka wastani wa siku 91 zilizobainishwa katika kanuni hadi siku 49 kwa zabuni za Kitaifa na kutoka wastani wa siku 100 hadi siku 56 kwa Zabuni za Kimataifa. Vile vile, muda wa Zabuni za Huduma za Ushauri utapungua kutoka wastani wa siku 174 hadi siku siku 126 kwa Zabuni za Kitaifa na wastani siku 211 hadi siku 146 kwa Zabuni za Kimataifa.

(c) Kupitia muundo na majukumu ya vyombo vinavyohusika na michakato ya ununuzi ndani ya Taasisi nunuzi kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi. Miongoni mwa mambo muhimu yatakayozingatiwa ni kupunguza idadi ya vikao vya Bodi ya Zabuni kwa kufuta sharti la kisheria linaloelekeza Taasisi nunuzi kufanya vikao vya zabuni siyo chini ya kikao kimoja kila mwezi kwa mwaka.

Muswada kupitia Ibara ya 39 unapendekeza Bodi kufanya kikao kimoja katika kila robo ya mwaka na vikao vya dharura vitafanyika pale Mwenyekiti atakapoona inafaa kufanyika. Marekebisho haya yanatokana na kupungua kwa kiwango kikubwa kwa shughuli za ununuzi za Taasisi nunuzi na kutokana na *GPSA* kupewa jukumu la ununuzi wa bidhaa na huduma mtambuka kwa Serikali na Taasisi zake.

Aidha, kupungua kwa idadi ya vikao kutapunguza gharama zinazotokana na posho ya vikao vya Bodi ya Zabuni, lakini vile vile, malipo ya posho na ada zinazolipwa kwa kamati mbalimbali zinazohusika na michakato ya zabuni, yatapitia upya kwa lengo la kuzifuta posho ambazo zinatokana na utekelezaji wa majukumu ya kazi ya kila siku ya washiriki wa vikao hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la hatua hii ni katika kutekeleza azma ya Serikali ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima ikiwemo posho za vikao kama nilivyobainisha katika hotuba ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2016 niliyoiwasilisha Bungeni tarehe 8 Juni, mwaka huu wa 2016.

(d) Kuweka sharti la kuzingatia viwango vilivyoidhiniswa na Serikali katika ununuzi wa mahitaji ya Taasisi kwa lengo la kudhibiti ubora, kurahisisha uratibu, ununuzi, usimamizi, udhibiti na matengenezo ya vifaa vinavyohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa kuweka viwango utahusisha aina ya bidhaa, sifa ya bidhaa, uimara wa bidhaa katika matumizi na unafuu wa bei. Hata hivyo, ili kuepuka kuweka viwango vitakavyofaidisha kampuni au bidhaa moja, utaratibu huu utajumuisha aina ya bidhaa zaidi ya moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mamlaka itakayosimamia uwekaji wa viwango vya bidhaa sitakazonunuliwa na Serikali, itaweka utaratibu wa namna ya kubadili viwango vya bidhaa pindi wazalishaji wa bidhaa husika watakapositisha uzalishaji, kubadili aina ya bidhaa, kubadili teknolojia, muundo au uimara wa bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ili Serikali iweze kufaidika katika utaratibu huo, mikataba ya ununuzi itakayoingiwa na Serikali na wazalishaji wa bidhaa hizo itazingatia masuala ya matengenezo vipuri na kadhalika ili kuhakikisha kwamba gharama zake zinakuwa nafuu. Hii ni kuweka mfumo utakaotoa upendeleo kwa makundi maalum kushiriki katika michakato ya zabuni kama vile wanawake, vijana, wazee na watu wenye mahitaji maalum kwa kuweka sharti kwa Taasisi nunuzi kutenga asilimia mahususi ya bajeti ya ununuzi kwa makundi hayo kama itakavyobainishwa kwenye kanuni.

(e) Kuweka upendeleo maalum kwa Wazabuni wanaotumia bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia malighafi za hapa nchini kwa kuweka sharti kwa taasisi nunuzi kutoa upendeleo wa angalau asilimia15 kama itakavyobainishwa kwenye kanuni.

(g) Kuweka sharti la kutumia mifumo ya kielektroniki katika ununuzi ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa Taasisi nunuzi kadri itavyowezekana kutumia mifumo ya kielektroniki wakati wa kuendesha michakato ya ununuzi au kuondoa mali za Umma pamoja na uandaaji na uwasilishaji wa ripoti kwa utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nieleze Mpangilo wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza yenye Ibara ya (1) inahusu masuala ya utangulizi, hususan jina la Sheria inayopendekezwa. Sehemu ya pili yenye Ibara ya (2) hadi 40 inaweka masharti

yanayopendekeza marekebisho katika vifungu mbalimbali vya sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (2) ya Muswada kama ilivyorekebishwa inapendekeza kurekebisha Kifungu cha (3) cha sheria kwa kufuta, kurekebisha na kuongeza tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya sheria ikiwemo *Defense and National Security, value for money* na *procurement* ili kuweka maana iliyokusudiwa na kuondoa ukinzani na tafsiri zilizopo katika sheria nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia jedwali la marekebisho, Ibara ya (2) ya Muswada imefanyiwa marekebisho ili kwanza kufuta tafsiri ya maneno *Budget Approving Authority* ili kuondoa utata wakati wa utekelezaji wa sheria na pili, kubainisha tafsiri ya maneno "*local firm*" kwamba ni kampuni ambayo asimilia kubwa ya hisa zake inamilikiwa na raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya (3) ya Muswada inapendekeza kuongeza kifungu kipya 4A ili kuweka misingi ya ujumla katika ununuzi na uondoaji wa mali ya Umma katika kuhakikisha usawa na haki kwa wazabuni wote kupata thamani halisi ya fedha katika ununuzi wa bidhaa na huduma katika misingi ya bei na ubora.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara za (4), (5), (6), (7), (8), (9) na (10) za Muswada zinapendekeza marekebisho ya vifungu vya 6 (2), (9), (10), (18), (20), (23) na (25) vya sheria ili kwanza kuondoa mwingiliano ya majukumu ya kiutendaji baina ya taasisi zinazosimamia ununuzi wa Umma nchini ambazo ni Idara ya Sera ya Ununuzi wa Umma, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma kupewa jukumu la kupata taarifa za bei ya bidhaa na huduma mtambuka zenye viwango vilivyothibitishwa kutoka kwa mamlaka zinazohusika ili kuendana bei ya soko na kuongeza wigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu, kupanua wigo wa sifa za mtu anayestahili kuteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma; na nne, Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma kupewa mamlaka ya kusimamia mchakato wa zabuni pindi inapofanya uchugnguzi kuhusu zabuni husika endapo itabaini kuendelea kwa mchakato kutaathiri uchunguzi unaofanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia jedwali la marekebisho Ibara ya (4) na (5A) za Muswada zimefanyiwa marekebisho ya kiuandishi ili kuleta maana

iliyokusudiwa na kuzihusisha Bodi za Wataalam katika kuandaa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 11 ya Muswada inayopendekeza marekebisho katika kifungu cha 31 (4) imefutwa ili kurejesha jukumu la Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri la kusimamia masuala ya ununuzi katika Halmashauri *(oversight functions)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 12 inapendekeza marekebisho katika Kifungu cha 35 (3) ili kuondoa sharti kwa Bodi za Zabuni kuridhia mikataba ya zabuni kabla ya kusainiwa. Lengo la marekebisho haya ni kufupisha muda wa mchakato wa zabuni kwa kuwa baada ya mkataba kuhakikiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mwanasheria wa Wizara au Taasisi kulingana na kiwango ni halali kisheria kusainiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 36 (1) cha sheria ili kwanza kuweka sharti kwa Afisa Masuuli kuwasilisha kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, taarifa kuhusu mikataba ya zabuni na mpango wa ununuzi wa mwaka wa fedha unaofuata kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi.

Pili, kuhakikisha kwamba taarifa zote za ununuzi zinasambazwa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki isipokuwa maeneo ambayo hayana miundombinu ya mifumo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 14 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kurekebisha kifungu cha 46A cha Muswada ili kisomeke kama Kifungu kipya cha 60A ili kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa kubainisha utaratibu utakaotumika na taasisi nunuzi katika kushuhudia mikataba ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza kufuta jina la Sehemu ya Tano na kuliandika upya ili kuweka mpangilio sahihi wa masharti ya sheria na hivyo kuleta maana iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 16 ya Muswada inapendekeza kufuta Kifungu cha 47 cha sheria kwa kuwa misingi iliyokuwa chini ya ibara hiyo imehamishiwa katika kifungu kipya cha 4A ili kuweka mpangilio mzuri wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 17 ya Muswada inapendekeza kurekebsiha kifungu cha 50 ili kwanza kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini *(GPSA)* na Wazabuni iliyofungamanishwa na bei ili kuondoa utaratibu wa kupanga bei elekezi na badala yake taasisi nunuzi zitafanya utaratibu wa ununuzi kwa kuzingatia bei ya

soko kwa wakati husika. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama ya ununuzi kupitia taasisi hii ambayo imekuwa ikilalamikiwa kwa kipindi kirefu. Pili, ni kufafanua tafsiri ya *open framework agreement* ili kubainisha kwamba mikataba ya aina hii baina ya *GPSA* na wazabuni haitahusisha bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 18 ya Muswada inapendekeza kuongeza vifungu vipya vya 55A, 55B, 55C na 55D ili kuweka masharti mbalimbali ya kutoa upendeleo maalum kwa kampuni za Kitanzania kushiriki katika zabuni za Serikali na kampuni zitakazotumia bidhaa zinazozalishwa Tanzania na kutenga zabuni kwa ajili ya Wazabuni wa Tanzania. Lengo la marekebisho haya ni kujenga uwezo wa makampuni ya wazawa katika ushiriki wa zabuni za Kitaifa na Kimataifa na kutoa upendeleo kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ili kuendeleza viwanda vya ndani.

Aidha, kupitia jedwali la marekebisho, Kifungu kipya cha 55A (2) (a) na (b) kimefanyiwa marekebisho ili kwanza kuweka sharti kwamba upendeleo utatolewa kwa kampuni ambayo imeshirikisha kampuni za Kitanzania kwa kiwango cha angalau asilimia 50. Pili, kuweka sharti kwamba upendeleo utatolewa kwa kampuni ambayo itathibitisha kuwa na wafanyakazi wa Kitanzania angalau asilimia 50. Vilevile, kupitia jedwali la marekebisho, Kifungu cha 55D kimefanyiwa marekebisho ya kiuandishi kwa kuondoa neno "*may*" na kuweka "*shall*" ili kuweka sharti la ulazima kwa taasisi ununuzi kutenga kazi kwa ajili ya kampuni za hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 19 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 59 cha sheria kwa kufuta kifungu kidogo cha (6) ili kuondoa sharti la kupata idhini ya kufuta mchakato wa zabuni kutoka kwa Mamlaka ya Udhibiti na Ununuzi wa Umma. Lengo la hatua hii ni kupunguza muda wa mchakato wa zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 20 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 60 cha sheria ili kwanza kupunguza muda wa kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli pindi Wazabuni wanapopokea kusudio la Afisa Masuuli kumpa tuzo *(award)* Mzabuni aliyeshinda kutoka siku 14 hadi siku saba.

Aidha, marekebisho ya kiuandishi yamefanyika kupitia jedwali la marekebisho ili kubainisha kwamba siku saba zinahusu siku za kazi pekee. Pili, ni kuondoa sharti kwa Afisa Masuuli wa Halmashauri, kuwasilisha uamuzi wa kumpa tuzo mzabuni kwenye Kamati ya Fedha na Mipango ya Halmashauri kwa uchambuzi na ridhaa kabla ya kumjulisha mzabuni aliyeshinda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho haya ni kuondoa jukumu hili kwa kuwa siyo jukumu la Kamati hii kwa mujibu wa Kifungu cha 31 (4) cha

Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 kama ilivyofafanuliwa katika kanuni zinazosimamia ununuzi kwenye Halmashauri *(The Local Government Authorities Tender Boards Establishment and Proceedings Regulations 2014)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza kufuta Kifungu cha 63 ili kwanza kuhamisha maudhui yaliyopo kwenye kifungu hiki kwenye kifungu kipya cha 4A ili kuweka mtiririko mzuri wa sheria.

Pili, kuweka sharti kwa taasisi nunuzi kwamba ununuzi na uondoaji wa bidhaa utatekelezwa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki *(e-procurement)* ili kuongeza uwazi, ufanisi na uwajibikaji. Aidha, maeneo ambayo hayana mifumo ya kielektroniki, utaratibu wa kawaida *(manual)* utatumika.

Aidha, marekebisho yamefanyika katika Ibara ya 21 kupitia jedwali la marekebisho kwa kufuta Kifungu kidogo cha (2) kinachohusu kuandaa kanuni kwa kuwa tayari kuna Kifungu cha 105 (2)(w) ambacho kimeweka sharti kwa Waziri wa Fedha kuandaa kanuni kwa ajili ya masuala ya ununuzi wa kutumia mifumo ya kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 64 cha sheria kwa kuweka sharti kwa taasisi nunuzi kutenga asilimia mahsusi *(specific percentage)* ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya vikundi mbalimbali vikiwemo wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 65 ili kwanza kufanya marekebisho ya kiuandishi ili kuleta maana iliyokusudiwa na pili kuondoa sharti la kupata idhini ya *GPSA* kabla ya kufanya ununuzi wa dharura ili kupunguza muda na kuongeza ufanisi kwenye mchakato wa ununuzi wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 24 ya Muswada inapendekeza kuongeza Kifungu kipya 65A. Kupitia kifungu hiki, taasisi nunuzi zimepewa uwezo wa kufanya ununuzi moja kwa moja kwa wazalishaji, wauzaji wa jumla au watoa huduma ili kupata thamani halisi ya fedha kulingana na bidhaa au huduma itolewayo. Muswada pia unapendekeza kifungu kipya cha 65B kinachobainisha masharti ya kuzingatia viwango vitakavyowekwa kwa ajili ya bidhaa zitakazotumiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 25 ya Muswada kama ilivyorekebishwa inapendekeza kufanya marekebisho ya kiuandishi kwenye Kifungu cha 73 (5) ili kuleta maana iliyokusudiwa. Aidha, Ibara ya 26 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 76 (2) kwa kufuta Kifungu kidogo cha (c) na (d). Marekebisho haya yanalenga kuruhusu taasisi nunuzi kufanya majadiliano ya

bei wakati wa mchakato wa zabuni kwa lengo la kupunguza bei ya ununuzi na kuongeza bei ya kuuza mali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 27 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho madogo ya kiuandishi katika Kifungu cha 77 (1) (b) cha sheria hii wakati ambapo Ibara ya 28 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho inapendekeza kurekebisha vifungu vidogo vya (3), (4) na (5) vya Kifungu cha 83 cha sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Marekebisho haya yana lengo la kuifanya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kuwa chombo pekee chenye mamlaka ya kufungia *(debarment)* Wakurugenzi wa Kampuni na kampuni ambayo imethibitishwa na Mahakama au Mamlaka ya Rufani za Zabuni kujihusisha na vitendo vya rushwa, udanganyifu na ushawishi wakati wa mchakato wa zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara 29 hadi ya 31 ya Muswada zinapendekeza kufanya marekebisho ya vifungu vya 88, 89 na 91 ili kutenganisha majukumu ya msingi ya Wajumbe wa Mamlaka za Rufani za Zabuni na shughuli za kiutawala katika Mamlaka ya Rufaa za Zabuni.

Aidha, marekebisho haya yanaweka utaratibu kwa Mamlaka ya Rufani za Zabuni kuwasilisha bajeti yake kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuidhinishwa badala ya utaratibu wa hivi sasa ambapo jukumu hili linatekelezwa na Wajumbe wa Mamlaka ya Rufani za Zabuni ambao kimsingi hawapaswi kufanya shughuli za kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 32 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 93 ili kuweka hitaji la kisheria kuwasilisha taarifa za mpango wa utekelezaji wa bajeti ya Mamlaka ya Rufani kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 33 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho kwa kufuta Kifungu cha 95 (3) cha sheria. Marekebisho haya yana lengo la kuondoa ukinzani wa masharti mbalimbali ndani ya kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 34 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho kwenye Kifungu cha 96 (4) na (6) cha sheria ili kupunguza muda wa kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli kutoka siku 28 mpaka siku saba za kazi *(working days)*. Aidha, kifungu hiki pia kimeweka sharti kwa Afisa Masuuli kutoa maamuzi dhidi ya malalamiko yaliyowasilishwa ndani ya siku saba za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 35 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 97 cha sheria ili kupunguza muda wa kuwasilisha rufaa kutoka siku 14 hadi siku saba za kazi. Lengo la marekebisho haya ni kupunguza muda wa mchakato wa kushughulikia malalamiko ya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 36 ya Muswada kama ilivyorekebishwa kupitia jedwali la marekebisho, inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 99 ili kupunguza muda na gharama zinazotokana na malalamiko yanayoweza kuwasilishwa na wazabuni walioshindwa zabuni. Aidha, kupitia jedwali la marekebisho, Afisa Masuuli au Mamlaka ya Rufaa za Zabuni, anapaswa kuwasilisha uamuzi wake kwa mzabuni ndani ya siku saba za kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 37 ya Muswada inapendekeza kurekebisha Kifungu cha 101 ili kuboresha taratibu za kuomba marejeo Mahakama Kuu unaofanywa na mashirika au taasisi za Serikali. Aidha, kupitia jedwali la marekebisho, imebainishwa kwamba maombi ya marejeo yatawasilishwa Mahakama Kuu baada ya kupata idhini ya Mahakama husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 38 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Kifungu cha 105 cha sheria ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya ununuzi kuandaa kanuni kwa ajili ya utaratibu wa ununuzi kwa taasisi za Umma zinazojiendesha kibiashara na ununuzi wa dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 39 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya jedwali la pili la sheria kwa kurekebisha aya ya tano ili kupunguza vikao vya Bodi kutoka vikao 12 kwa mwaka hadi vikao vinne kwa mwaka. Aidha, vikao vya dharura vitafanyika pale Mwenyekiti atakapoona inafaa. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama zinazotokana na wingi wa vikao vya zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 40 ya Muswada inapendekeza marekebisho ya jedwali la tatu la sheria kwa kufuta aya ya tatu na ya nane ili kwanza kuondoa Kamati za Bodi ambazo hivi sasa hazipo kwenye muundo wa Mamlaka ya Rufani za Zabuni; na pili, kuondoa ndani ya sheria taratibu za kiutawala kuhusu uandishi wa kumbukumbu za vikao vya Mamlaka za Zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge muujadili Muswada huu na hatimaye mkubali kuupitisha kuwa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, kwa hiyo, tutaendelea na hatua zinazofuata. Waheshimiwa Wabunge, tulipaswa sasa hivi kuisikia Kamati ya Bajeti ikileta maoni yake kuhusu hili, lakini ndiyo wanakamilisha taarifa yao. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo, nitasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni ili wao waweze kuleta sasa taarifa yao halafu tuanze na mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa maelezo hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

(Saa 5.35 Asubuhi Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 jioni)

(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)

NAIBU SPIKA: Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti

MHE. HAWA A. GHASIA- MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania toleo la Januari, 2016, napenda kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016, ambao unafanya marekebisho kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2011 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ununuzi wa Umma kwa kuondoa upungufu uliopo katika sheria ya sasa kwa kupunguza gharama na muda wa michakato ya manunuzi, kutoa upendeleo maalumu kwa kampuni za ndani za Watanzania pamoja na vikundi maalumu kwenye masuala ya ununuzi, kutumia malighafi na bidhaa zinazozalishwa nchini, kuweka viwango mahsusi kwa bidhaa zitakazotumiwa na Serikali na kuruhusu ununuzi wa bidhaa na huduma moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji kulingana na bei halisi ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** tarehe 27 Juni, 2016 Kamati yangu ilifanya Mkutano na Wadau mbalimbali *(Public hearing)* ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki walitoka Shirika la Simu Tanzania *(TTCL),* Bodi ya Taifa ya Uhasibu na Wakaguzi *(National Board of Accountants and Auditors),* Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *(CRB),* Asasi ya Kijamii ya SIKIKA pamoja na Taasisi ya Maendeleo ya Afya Tanzania *(Health Promotion)* na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali *(LAPF)*.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha, Watendaji wa Wizara yake, Taasisi zinazoratibu Ununuzi wa Umma pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kujadili kwa kupitia vifungu vyote kwenye Muswada huu. Kamati imeridhika na marekebisho yaliyofanyika ambayo kimsingi yamejumuisha maoni na ushauri wa muda mrefu uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wadau wa manunuzi katika upande wa muda mrefu wa mchakato wa ununuzi, gharama kubwa za zabuni, pamoja na kupunguza matumizi ya Serikali kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kushauriana na Serikali na kupitia vifungu vyote vya Muswada huu, ina maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuweka sharti la kutenga kazi kwa ajili ya Wakandarasi wa ndani, Kamati ilishauri Serikali kutumia neno *"shall"* badala ya *"may"* kwa ajili ya kuyataka mamlaka ya kutenga kazi kwa ajili ya kuweka Wakandarasi wa ndani. Serikali ilikubaliana na wazo hili na imefanyia mabadiliko haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoa ufafanuzi wa neno "*local Firm*," Serikali inakusudia kufanya mabadiliko kwa kuongeza kifungu cha 55A, 55B, 55C na 55D ili kutoa upendeleo kwa Makampuni ya Watanzania kushiriki katika ununuzi wa bidhaa na huduma. Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha kwamba inaweka Tafsiri ya neno *"local firm"* ili kuhakikisha kwamba kampuni zinazolengwa ni zile ambazo zinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100. Serikali imechukua wazo hili na imeahidi kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika mabadiliko ya jumla yanayopendekezwa katika Sehemu ya Pili, katika Kifungu cha (2) cha Muswada ni kuongeza tafsiri ya maneno *"Budget Approving Authority*." Kamati ilishauri Serikali kutoa tafsiri sahihi ya *maneno "Budget Approving Authority,"* kwa sababu Sheria hii inatumika kwa Taasisi na Mashirika mbalimbali ya Umma ambayo yana utaratibu tofauti wa kupitisha Bajeti zao. Kwa mfano, mifuko ya jamii ikiwemo *LAPF*, bajeti inapitishwa na Bodi na baadaye kwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara husika. Serikali imekubali kuondoa tafsiri ya maneno hayo ili kuondoa mkanganyiko huo na hivyo tulikuwa tunaomba iletwe *schedule of amendment* kwa sababu ilikuwa bado haijaletwa.

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika Kifungu cha 11 cha Muswada ambapo ilikuwa inapendekeza kufuta Kifungu cha 65 (4) cha Sheria ya Manunuzi ambacho kilikuwa kinatoa fursa kwa Waheshimiwa Madiwani kushiriki katika mchakato wa manunuzi. Baada ya majadiliano ya kina, imekubaliana na pendekezo la Kamati la kuacha kifungu hicho kama ilivyo kwenye sheria ya sasa. Kwa sababu ilikuwa inapendekeza kwamba hata ile taarifa ambayo ilikuwa inapelekwa kwenye Kamati ya Fedha isipelekwe. Hata hivyo, katika

mabadiliko yaliyowasilishwa na Serikali hayaonyeshi kutekelezwa kwa makubaliano hayo, japo Mheshimiwa Waziri amekubaliana na Mapendekezo ya Kamati lakini tulikuwa tunaomba alete *schedule of amendment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatambua kwamba huwezi kuwa na orodha inayojitosheleza ya huduma na bidhaa maalumu. Hata hivyo, Kamati ilishauri Serikali kutoa tafsiri ya maneno "*specialized equipment,*" ili kuondoa utata ambao unaweza kujitokeza wakati wa ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo Serikali imekusudia. Serikali imekubali pendekezo hili na italitolea ufafanuzi pamoja na maboresho ikiwa ni pamoja na *schedule of amendment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyopo kwenye Kifungu cha 38 cha Muswada ili kwa kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 105 (2) cha Sheria ya Manunuzi ili kutoa fursa kwa Taasisi na Makampuni ya Umma yanayofanya kazi kibiashara kuwa na utaratibu wake wa kufanya maamuzi. Hatua hii itawezesha makampuni hayo kujiendesha Kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu marekebisho ya kifungu cha 24 cha Muswada kwa kuongeza Kifungu kidogo cha 65A na 65B yenye lengo la kuweka sharti ya kufanya manunuzi kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa bidhaa mbalimbali zitakazotumika Serikalini ikiwemo ununuzi wa magari. Kwa muda mrefu Bunge limekuwa likishauri Serikali kupunguza gharama kubwa inayotumiwa na Serikali katika ununuzi wa mafuta, magari na matengenezo ya magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya bajeti inaendelea kusisitiza kuwa Serikali isimamie na kuhakikisha kuwa sasa Watumishi wa Umma ambao hawastahili kupewa magari, watumie magari yao binafsi na wale ambao wanastahili kukopeshwa magari na Serikali na kupewa posho kidogo kwa ajili ya mafuta na matengenezo isipokuwa kwa baadhi ya viongozi kulingana na stahili zao.

Mfano, Wakuu wa nchi, Viongozi Wakuu wa mihimili, Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waendelee kupewa magari lakini wale ambao stahili zao ni kukopeshwa, basi wakopeshwe na wapewe posho ya kuendesha vifaa vyao. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kununua magari kwa pamoja, yaani *bulk procurement* yasiyokuwa na gharama kubwa kulingana na bei ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Muswada kwenye Kifungu cha 18 na 22 yametoa fursa muhimu ya kuhusisha wazabuni wa ndani katika manunuzi hasa kwa upande wa kuwajumuisha kushiriki kwenye shughuli hizo pamoja na wazabuni wa nje. Kamati inaona kuwa hatua hii ni ya kupongezwa

na itatoa fursa kwa Wataalamu wa Kitanzania katika nyanja mbalimbali na kampuni za ndani hasa zile zinazohusu Wakandarasi kujifunza na kujiongezea uwezo kwa kushirikiana na kampuni ya nje hasa kwa upande wa kuongeza ujuzi na matumizi ya teknolojia mpya.

Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa uwezeshaji wa wakandarasi *(Local Contractors and supplies Empowerment Fund)* ili waweze kumudu utoaji wa huduma mbalimbali zinazohusisha gharama kwa mfano, ukandarasi wa barabara. Mfuko huu unaweza kutumika kutoa dhamana *(bond)* wakati wa kuomba kazi. Mfano mzuri tunauona kwa nchi ya China ambayo ina mfumo maalumu wa kusaidia makampuni yao ya ndani kupata kazi nje ya mipaka ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** bado kuna changamoto kubwa katika Halmashauri zetu kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri. Mara nyingi uteuzi huu umekuwa ukifanywa na Watendaji Wakuu wa Halmashauri, yaani Wakurugenzi kulingana na matakwa yao binafsi na si kwa mahitaji ya zabuni husika. Kamati inashauri Serikali kutunga kanuni zitakazosaidia kutoa vigezo na maelekezo ya uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Zabuni za Halmashauri ili kutoa usawa na utendaji wa haki katika maamuzi ya zabuni husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika**,** katika majadiliano ya Kamati na Wizara ya Fedha, Serikali ilikuja na mabadiliko ambayo yanapendekeza kuongeza kifungu kipya 102A ambacho kingebeba vifungu vipya vifuatavyo; 55A, 55B, 55C, 55D, 64, 65A, 65B na 105B ambavyo hivyo vimebeba roho ya marekebisho ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vifungu hivyo, Serikali inapendekeza Sheria hii kutoanza kutumika mpaka Waziri atakapotangaza rasmi kwenye gazeti la Serikali. Katika orodha ya marekebisho mapya ambayo yamewasilishwa na Waziri wa Fedha, Pendekezo hilo la kuwa na Kifungu cha 102A halipo katika *Schedule of Amendment*. Kamati inaomba kujua na inamwomba Waziri wa Fedha atuambie, ni lini marekebisho haya yataanza kutumika baada ya kupitishwa na Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika**,** Kamati imebaini kwamba kuna upungufu mkubwa katika manunuzi ya Umma hasa katika kipindi cha uchaguzi ambapo Kamati ya Fedha pamoja na Baraza la Madiwani linakuwa limevunjwa. Aidha, Kanuni za uendeshaji wa Halmashauri haziruhusu Baraza la Madiwani kujadili Taarifa ya Manunuzi na taarifa nyingine pindi Baraza jipya la Madiwani linapoingia madarakani. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalumu kwenye kanuni ili kuruhusu baraza jipya kupewa taarifa ya mchakato wa

manunuzi kwa kipindi chote wakati ambapo Baraza halikuwepo na wao kupata fursa ya kushauri. *(Makofi)*

Kamati inaipongeza serikali kwa kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi wa Serikali *(GPSA)* na wazabuni iliyofungamanishwa na bei. Utaratibu huu umekuwa ukilalamikiwa kwa muda mrefu kati ya wadau wa manunuzi ya Umma, kuwa ulikuwa unaongeza urasimu na gharama ya bidhaa za kutoa huduma tofauti na bei ya soko. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa haraka wa huduma husika pamoja na kupunguza urasimu na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa kubainisha utaratibu utakaotumika kupata huduma hizo kulingana na bei husika.

Kamati inaishauri Serikali wakati wa kuandaa Kanuni kuzingatia mazingira wezeshi, yaani mazingira maalumu yatakayowasaidia wahisani wanaochangia miradi ya maendeleo pale itakapohitajika Serikali kuwasaidia kugharamia baadhi ya michango au huduma za haraka ambazo zitasaidia utekelezaji wa mradi husika. Mfano, wahisani wanaweza kutoa msaada wa vifaa vya hospitali kwa masharti kwamba Serikali itahitaji kuchangia Bima na Usafirishaji. Fursa hizi zionyeshwe kwenye kanuni hasa kwa upande wa miradi ya ubia, yaani *PPP* itakayohusu ujenzi wa madarasa, barabara na miundombinu mingine katika Halmashauri na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yanayotoa huduma kwa bei za juu kuliko bei za soko. Mfano, kufanya matengenezo ya magari kwa upande wa *TEMESA*, inakuwa ni gharama kubwa sana ukilinganisha na maeneo mengine, mfano, inagharimu takribani Shilingi milioni tatu hadi tano kulingana na aina ya gari. Kiasi hiki ni kikubwa kuliko kiasi kinachotozwa kwenye baadhi ya karakana za watu binafsi ambao wanatoa huduma kama hiyo. Hivyo ni vyema Taasisi hizo za Serikali zikatoza bei ya soko ili ziweze kushindana katika soko la kupata wateja zaidi ya wateja wanaowapata sasa hivi ambazo nyingi ni Taasisi za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imepitia na kujadili kwa kina marekebisho ya Muswada huu na kuona kuwa kuna baadhi ya maeneo muhimu Serikali imejitahidi kuyafanyia kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kuondoa sharti la kisheria linalozuia majadiliano ya bei katika zabuni kati ya taasisi nunuzi na zabuni ili kupata unafuu wa bei tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Hii itasaidia kufikia makubaliano kulingana na mazingira halisi ya huduma inayotakiwa kutolewa. Pia kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi pamoja na muda wa mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa Maafisa Masuuli kutoka siku 28 hadi siku saba. Hii itasaidia kuharakisha manunuzi. Hata hivyo, Kamati inapendekeza

kwamba badala ya kusema tu siku saba, basi isomeke kwamba ni siku saba za kazi.

Pia suala la kurekebisha kanuni ili kupunguza muda wa mchakato wa zabuni za ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma kutoka wastani wa siku 91 zilizobainishwa katika Kanuni hadi siku 49 kwa zabuni za Kitaifa na kutoka wastani wa siku 100 hadi siku 56 kwa zabuni za Kimataifa. Hatua hii itaharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo tunayokusudiwa kutekeleza hasa pamoja na kuhakikisha malipo ya Wakandarasi pale wanapotoa huduma.Pia kufanya marekebisho ya muundo na majukumu ya vyombo vinavyohusika na michakato ya manunuzi ndani ya taasisi ya nunuzi ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi. Hatua hii itapunguza pia urasimu na kuharakisha manunuzi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa wakati na hivyo kuongeza ufanisi na uwazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilikuwa inaiomba Serikali iangalie pale ambapo Wakandarasi wametoa huduma katika Serikali na Serikali ikachelewa kuwalipa na pale ambapo pia wakandarasi wamechukua mikopo kutoka mabenki mbalimbali ambayo yana riba kubwa. Kwa hiyo iangalie jinsi gani ambavyo itawasaidia kuwafidia wakandarasi pale ambapo dhamana zao zinachukuliwa katika mabenki, lakini kutokana tu na ucheleweshaji wa ulipaji kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa tunaomba kwa kuanzisha ule mfuko ambao una wawezesha na kuwapa bondi Wakandarasi nadhani tatizo hilo lingekuwa linaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, naomba nitumie fursa hii niombe washiriki wote watambuliwe na *Hansard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Ashatu Kijaji, Mbunge, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, Makamishina wa Bajeti, pamoja na wataalam wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu. Pia tunapenda kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimalizie kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Mheshimiwa Spika, Katibu wa Bunge na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutokana na uharaka wa kuandaa taarifa hii, kuna *schedule* za *amendment* ambazo zitaletwa katika Bunge hili ili ziweze kufanyiwa marekebisho, pamoja na marekebisho ambayo yataletwa na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda nimshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti, ndugu Lina Kitosi, Mkurugenzi Msaidizi Mathew Kileo, ndugu Michael Kadebe, pamoja sekretarieti ambayo ni pamoja na ndugu Godfrey Godwin, Emmanuel F. Robby, Ruva Tunze, Maombi Kakosi, Lilian Masabala na Wilson E. Machaine kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

TAARIFA YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA MAREKEBISHO YA SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA WA MWAKA 2016 (THE PUBLIC PROCUREMENT (AMENDMENT) ACT 2016) KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la Januari 2016 napenda kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Bajeti kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016 (*The Public Procurement (Amendment) Act, 2016*).

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2016, ambao unafanya marekebisho kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ununuzi wa Umma kwa kuondoa upungufu uliopo katika Sheria ya sasa kwa kupunguza gharama na muda wa michakato ya ununuzi, kutoa upendeleo maalumu kwa kampuni za ndani za Watanzania pamoja na vikundi maalum kwenye masuala ya ununuzi, kutumia malighafi na bidhaa zinazozalishwa nchini, kuweka viwango mahsusi (standards) kwa bidhaa zitakazotumiwa na Serikali na kuruhusu ununuzi wa bidhaa na huduma moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji kulingana na bei halisi ya soko.

Mheshimiwa Spika, tarehe 27 Juni, 2016 Kamati yangu ilifanya Mkutano na Wadau mbalimbali *(Public hearing)* ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu kabla ya kuanza majadiliano na Serikali. Wadau walioshiriki walitoka Shirika la Simu Tanzania *Tanzania Telecommunication Company Limited (TTCL),* Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi *National Board of Accountants and Auditors (NBAA),* Bodi ya Usajili wa Wakandarasi *Contactors Registration Board (CRB),*

Asasi ya Kijamii ya *TWAWEZA* Taasisi ya Maendeleo ya Afya Tanzania *Health Promotion Tanzania (HDT)* na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa *(LAPF)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha, watendaji wa Wizara yake, Taasisi zinazoratibu Ununuzi wa Umma pamoja na Wanasheria kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kujadili kwa kupitia vifungu vyote kwenye Muswada huu. Kamati imeridhika na marekebisho yaliyofanyika ambayo kimsingi yamejumuisha maoni na ushauri wa muda mrefu uliotolewa na Wabunge pamoja na wadau wa manunuzi hasa katika upande wa muda mrefu wa mchakato wa ununuzi, gharama kubwa ya zabuni, pamoja na kupunguza matumizi ya Serikali kwenye ununuzi wa bidhaa na huduma.

2.0. MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika baada ya Kamati kushauriana na Serikali na kupitia vifungu vyote vya Muswada ina maoni na ushauri ufuatao;

2.1. Maoni Kuhusu Vifungu mbalimbali ya Muswada.

2.11. Kuweka Sharti ya Kutenga kazi kwa ajili ya Wakandarasi wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishauri Serikali kutumia neno "Shall" badala ya "may" kwa ajili ya kuyataka mamlaka ya kutenga kazi kwa ajili kuweka makandarasi wa ndani. Serikali ilikubaliana na Wazo hili na imefanya mabadiliko.

2.12. Kutoa ufafanuzi wa neo *"Local Firm"*

Mheshimiwa Spika, Serikali inakusudia kufanya mapadiliko kwa kuongeza kifungu cha 55A,55B,55C na 55D ili kutoa upendeleo kwa Makampuni ya Watanzania kushiriki katika ununuzi wa bidhaa na huduma. Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha inaweka Tafsiri ya neno "Local firm" ili kuhakikisha kwamba kampuni zinazolengwa ni zile ambazo zinamilikiwa na Watanzania kwa asilimia 100. Serikali imelichukua wazo hili na imelifanyia kazi.

2.13. Kutoa Tafsiri ya maneno *"Budget Approving Authority"*

Mheshimiwa Spika, Katika mabadiliko ya ujumla yanayopendekezwa katika Sehemu ya pili kifungu cha 2 cha musada ni kuongeza tafsiri ya maneno *Budget Approving Authority*" .Kamati ilishauri Serikali kutoa tafsiri sahihi ya *maneno "Budget Approving Authority"* kwasababu Sheria hii inatumika kwa Taasisi na Mashirika mbalimbali ya umma ambayo yana utaratibu tofauti wa kupitisha Bajeti zao. Mfano Mifuko ya jamii bajeti inapitishwa na Bodi na baadae kwa

Waziri mwenye dhamana ya Wizara husika. Serikali imekubali kuondoa Tafsiri ya maneno hayo ili kuondoa mkanganyiko.

2.14. Kuwaondoa Madiwani katika Mchakato wa Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, Katika kifungu cha 11 cha Muswada ambayo ilikuwa inapendekeza kufuta kifungu cha 65 (4) cha Sheria ya Manunuzi ambacho kilikuwa inatoa fursa kwa Waheshiwa Madiwani kushirki katika mchakato wa manunuzi. Baada ya majadiliano ya Kina Serikali imekubaliana na pendekezo la Kamati la kuacha kifungu hicho kama kilivyo kwenye Sheria ya sasa. Hata hivyo katika mabadiliko yaliyowasilishwa na Serikali hayaonyeshi kutekeleza kwa makubaliano hayo.

2.15. Kutoa Tafsiri ya maneno "*Specialized good and equipment*"

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua kwamba huwezi kuwa na orodha inayojitosheleza ya huduma na bidaa maalumu**.** Hata hivyo, Kamati ilishauri Serikali kutoa Tafsiri ya maneno "*Specialized equipment*" ili kuondoa utata utata ambao unaweza kujitokeza wakati wa ununuzi wa vifaa hivyo ambavyo Serikali imekusudia. Serikali imekubali pendekezo hilo na italitolea ufafanuzi.

2.16. Ununuzi katika Mashirika na Taasisi za Umma ambayo yanafanya Biashara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekubaliana na Mapendekezo ya muswada yaliyopo kwenye kifungu cha 38 cha Muswada, ili kwa kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 105 (2) cha Sheria ya manunuzi ili kutoa fursa kwa Taasisi na Makampuni ya umma yanayofanya biashara kuwa na utaratibu wake wa kufanya maamuzi. Hatua hii itayawezesha makampuni hayo kujiendesha Kibiashara.

2.2. Maoni ya Ujumla Kuhusu Sheria ya Manunuzi.

2.21. Manunuzi kulingana na thamani ya fedha

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na Serikali kuhusu marekebisho ya kifungu cha 24 cha Muswada kwa kuongeza kifungu kidogo cha 65A na 65B vyenye lengo la kuweka masharti ya kufanya manunuzi kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa bidhaa mbalimbali zitakazotumika Serikalini ikiwemo ununuzi wa magari. Kwa muda mrefu Bunge limekuwa likishauri Serikali kupunguza gharama kubwa inayotumiwa na Serikali katika ununuzi wa mafuta, magari na matengenezo ya magari. Kamati ya bajeti inaendelea kusisitiza kuwa Serikali isimamie na kuhakikisha kuwa sasa watumishi wa umma ambao hawastahili kupewa magari watumie magari yao binafsi na wale ambao wanastahili wakopeshwe magari na Serikali na kupewa posho kidogo kwa ajili ya mafuta na matengenezo isipokuwa kwa baadhi ya viongozi kulingana na stahili zao (Mfano Viongozi wakuu wa nchi, Viongozi wakuu wa Mihimili, Wakuu wa

Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya). Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kununua magari kwa pamoja (***bulk procurement***) yasiyo na gharama kubwa kulingana na bei ya soko.

2.22. Uhusishwaji wa wazabuni wa ndani katika manunuzi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho ya muswada kwenye kifungu cha 18 na 22 yametoa fursa muhimu ya kuhusisha wazabuni wa ndani katika manunuzi hasa kwa upande wa kuwajumuisha kushiriki kwenye shughuli hizo pamoja na wazabuni wa nje. Kamati inaona kuwa hatua hii ni ya kupongezwa na itatoa fursa kwa Wataalmu wa Kitanzania katika nyanja na kampuni za ndani hasa zile zinazohusu wakandarasi kujifunza na kujiongezea uwezo kwa kushirikiana na kampuni za nje hasa kwa upande wa kuongeza ujuzi na matumizi ya teknolojia mpya. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuanzisha mfuko wa uwezeshaji wa wakandarasi *(Local Contractors and supplies Empowerment Fund)* ili waweze kumudu utoaji wa huduma mbalimbali zinazohusisha gharama kubwa mfano ukandarasi wa barabara. Mfuko huu unaweza kutumika kutoa dhamana *(Bond)* wakati wa kuomba kazi *(Tender)*. Mfano mzuri tunauona kwa Nchi ya China ambayo ina mfumo maalumu wa kusaidia makampuni yao ya ndani kupata kazi nje ya mipaka ya nchi yao.

2.23. Uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, bado kuna changamoto kubwa katika Halmashauri zetu kuhusu uteuzi wa wajumbe wa Bodi za Zabuni za Halmashauri. Mara nyingi uteuzi huu umekuwa ukifanywa na Watendaji Wakuu wa Halmashauri (Wakurugenzi) kulingana na matakwa yao binafsi na si kwa mahitaji ya zabuni husika. Kamati inashauri Serikali kutunga kanuni zitakazo saidia kutoa vigezo na maelekezo ya uteuzi wa wajumbe wa Bodi ya Zabuni za Halmashauri ili kutoa usawa na utendaji haki katika manaumuzi ya zabuni husika.

2.24. Kuanza kwa Kutumika kwa Mapendekezo yaliyoletwa kwenye Muswada wa Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Spika, Katika majadiliano ya Kamati naWaziri wa Fedha, Serkali ilikuja na mabadiliko ambayo yanapendekeza kuongeza kifungu kipya 102A ambacho kingebeba vifungu vipya vifuatavyo: 55A, 55B, 55C, 55D, 64, 65A, 65B na 105 (2). Ambavyo hivyo vimebeba roho ya marekebisho ya muswada huu, katika vifungu hivi Serikali inapendekeza Sheria hii kutoanza kutumika mpaka watakavyokamilisha uandaaji wa kanuni za utekelezaji. Katika orodha ya marekebisho mapya ambayo imewasilishwa na Waziri wa Fedha Pendekezo hilo la kuwa na kifungu cha 102A halipo katika schedule of Amdment. Kamati inajiuliza ukimya huu wa Serikali maandlizi yatakayowezesha Sharia hii kutumika yatakamilika lini.

2.25. Utaratibu wa Manunuzi kipindi cha Uchaguzi Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba kuna mapungufu makubwa katika manunuzi ya umma hasa katika kipindi cha uchaguzi ambapo Kamati ya Fedha pamoja na Baraza la Madiwani linakuwa limevunjwa (Kipindi wa uchaguzi). Aidha, Kanuni za uendeshaji wa Halmashauri haziruhusu Baraza la Madiwani kujadili Taarifa ya manunuzi na Taarifa nyingine pindi Baraza jipya la madiwani linapoingia madarakani. Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu maalumu kwenye kanuni ili kuruhusu baraza jipya kupewa taarifa ya mchakato wa manunuzi kwa kipindi chote wakati baraza halikuwepo na wao wapate fursa ya kushauri.

2.26. Kuondoa upangaji wa bei elekezi na watoa zabuni

Mheshimiwa Spika, kamati inaipongeza serikali kwa kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na wazabuni iliyofungamanishwa na bei. Utaratibu huu umekuwa ukilalamikiwa kwa muda mrefu kati ya wadau wa manunuzi ya umma, kuwa ulikuwa unaongeza urasimu na gharama ya bidhaa na huduma tofauti na bei ya soko. Hatua hii itasaidia upatikanaji wa haraka wa huduma na husika pamoja na kupunguza urasimu na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa kubainisha utaratibu utakaotumika kupata huduma hizo kulingana na bei husika.

2.27. Ushirikiano baina ya Halmashauri na Wahisani katika utekelezaji wa Miradi ya Ubia *(PPP)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali wakati wa uandaaji wa Kanuni kuzingatia mazingira wezeshi (maalumu) yatakayosaidia wahisani wanaochangia miradi ya maendeleo pale watakapohitaji Serikali iwasaidia kugharamia baadhi ya michango au huduma za haraka ambazo zitasaidia utekelezaji wa mradi husika. Mfano wahisani wanaweza kutoa msaada wa vifaa vya hospitali kwa masharti kwamba Serikali itahitajika kuchangia Bima na Usafirishaji *(Insurance and Freight)*. Fursa hizi zionyeshwe kwenye kanuni hasa kwa upande wa miradi ya ubia (PPP) itakayohusu ujenzi wa madarasa, barabara na miundombinu mingine katika Halmashauri na Serikali kuu.

2.28. Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutoa Huduma kwa Bei ya juu kuliko Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kuna baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yanatoa huduma kwa bei ya juu kuliko bei ya soko. Mfano kufanya matengenezo madogo kwenye magari (Service) kwa TEMESA inagaharimu takribani Shilingi 3,000,000 hadi 5,000,000 kulingana na aina ya gari. Kiasi hiki ni kikubwa kuliko kiasi kinachotozwa kwenye baadhi ya karakana za watu binafsi ambao

wanatoa huduma kama hiyo. Hivyo ni vyema Taasisi hizo za Serikali zikatoza bei ya soko ili ziweze kushindana katika soko la kupata wateja zaidi ya wateja wanaowapata hivi sasa ambazo nyingi ni Taasisi za Umma tu.

2.29. Maeneo mengine muhimu ya muswada huu

Mheshimiwa Spika, kamati imepitia na kujadili kwa kina marekebisho ya Muswada huu na kuona kuwa kuna baadhi ya maeneo muhimu Serikali imejitahidi kuyafanyia kazi kama ifuatavyo:-

a) Kamati inaipongeza Serikali kuondoa sharti la kisheria linalozuia majadiliano ya bei katika zabuni kati ya taasisi nunuzi na mzabuni ili kupata unafuu wa bei tofauti na ilivyokuwa hapo awali. Hii itasaidia kufikia makubaliano kulingana na mazingira halisi ya huduma inayotakiwa kutolewa;

b) Kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi pamoja na muda wa mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli kutoka siku 28 hadi siku 7; hii itasaidia kuharakisha manunuzi. Hata hivyo, Serikali ijirekebisha na ucheleweshaji unaojitokeza wakati wa uandaaji wa nyaraka za Zabuni (*bid documents)* na uidhinishaji (*approval*); uharaka katika tathmini ya tenda; muda wa kusubiri kusaini Mikataba/Zabuni na mabadiliko yatokanayo na mabadiliko ya viwango vya gharama mara zabuni zinapopitishwa *(limit negotiations of contract variations)*.

c) Kurekebisha kanuni ili kupunguza muda wa mchakato kwa zabuni za ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma kutoka wastani wa siku 91 zilizobainishwa katika Kanuni hadi siku 49 kwa zabuni za kitaifa na kutoka wastani wa siku 100 hadi siku 56 zabuni za kimataifa.Hatua hii itaharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo tunayokusudia kutekeleza sasa pamoja na kuharakisha malipo ya wakandarasi pale wanapotoa huduma.

d) Kufanya marekebisho ya muundo na majukumu ya vyombo vinavyohusika na michakato ya ununuzi ndani ya taasisi nunuzi ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi. Hatua hii itapunguza urasimu na uharakishaji wa maamuzi na hivyo kurahisha upatikanaji wa bidhaa na huduma kwa wakati na hivyo kuongeza ufanisi wa kazi.

3.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati, ambao wametoa maoni na mapendekezo mbalimbali yaliyowezesha kuboresha taarifa hii hatimaye kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Susana Chogidasi Mgonukulima, Mb
16. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb
17. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
18. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
19. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
23. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb
24. Mhe.Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
25. Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb
26. Mhe. Albart Obama Ntabaliba, Mb
27. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb

Aidha, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Fedha na Mipango Mhe. Dkt Philip Mpango Mb, Naibu Waziri Mhe. Dkt Ashatu K. Kijaji Mb, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu, Kamishna wa Bajeti pamoja na wataalamu wao kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati yangu wakati wote wa mjadala wa Muswaada. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) pamoja na Wakala wa Huduma ya Ununuzi wa Umma (GPSA) kwa mchango wao katika muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kukushukuru wewe binafsi, Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Lina Kitosi, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo Ndg. Michael Kadebe, pamoja na Sekretarieti ya Kamati Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel F Rhobi, Ndg. Ruva Tunze, Ndg. Maombi Kakozi, Ndg. Lilian Masabala, na Ndg. Wilson E

Machaine kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na hatimaye kuweza kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa Abdulrahman Ghasia (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
28 Juni, 2016

NAIBU SPIKA: Ahsante Mwenyekiti.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa mawasilisho wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango na tumeshaisikia Kamati, nimeletewa majina hapa tunaanza uchangiaji mchana huu. Kwa hiyo, tutaendelea na uchangiaji mpaka tutakapofikia hatua nyingine kwa mujibu wa Kanuni zetu.

Katika wachangiaji tulionao mchana wa leo, tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Diodurus Kamala, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Martha Moses Mlata ajiandae.

MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA: Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la hoja mbalimbali za kwamba fedha za Serikali zinatumika nyingi pasipokuwa na sababu, mara nyingi tumekuwa tukisikia viongozi mbalimbali wakisema huu ni mfano tu, kwamba *pen* ingweza kununuliwa shilingi 100 au 200, lakini kwa sababu ya Sheria ya *Procurement* tunalazimika kununua *pen* hiyo kwa shilingi 1000, 2000, 3000 au hata 10,000. Sasa chimbuko la tatizo hilo ni kifungu namba 50 na 56 kilichoanzisha Mamlaka ya *GPSA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko yote haya tunayoyafanya kwa lengo la kuhakikisha tunaokoa fedha ya Serikali isitumike pasipokuwa ya lazima, bila kufanya marekebisho ya makusudi kuhusu utaratibu unaotumiwa na *GPSA* tutakuwa hatujafanya lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana wale wachache wanaofanikiwa kuingia kwenye *GPSA;* Taasisi mbalimbali na hasa kwa hizi *items* ambazo zinatumika kununua kwa utaratibu wa *GPSA* ni zile *items* zinazotumika kila siku, *computer*, masuala ya *pen*, uchapishaji na mambo mengine madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa kuwa *GPSA* inakuwa imeshaweka orodha kwamba hawa ndio wanahusika nchi nzima, na Taasisi kama iko Kagera ikijikuta kwamba kati ya wote waliobanishwa ndani ya orodha ya *GPSA* hakuna anayetoka eneo hilo, maana lazima watalazimika kufuata ile bei ambayo imewekwa na *GPSA*. Hili ni tatizo kubwa ambalo kama hatutaligusia katika mabadiliko haya huenda tukaendelea na matatizo kama tuliyokuwa tukiyazungumzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia katika kifungu cha 4A(1) ambapo inasema; *all public procurement and disposal by tender shall be*, lakini neno *by tender* nashauri liondolewe kwa sababu njia ya manunuzi *by tender* ni njia mojawapo, zipo njia nyingine nyingi tu, ambazo sheria inazitambua. Zipo taratibu kama vile *restricted system, shopping, single source, direct contracting, minor value* sasa zote hizi zinatambulika. Ukisema *by tender* maana yake hizi nyingine zote zinazotambuliwa na sheria umeziweka pembeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo ningependa iangaliwe, ukienda katika kifungu cha 6(c) *replace monitor and evaluate with advice with on performance,* sheria inashauri tuweke maneno *advice on performance* na tuondoe *monitor and evaluate* katika kifungu 6(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho ningependa kusema hapa ni kwamba hiki kifungu nashauri chote kifutwe, kwa sababu masuala ya *advice and performance* tayari sheria inatambua yako kwenye sheria na yanasimamiwa na *PPRA*. Sasa masuala ya *advice and performance* tayari tumeshaweka utaratibu mzuri wa kuyashughulikia na sheria inatambua kuwepo kwa *PPRA*; kwa hiyo tutakuwa tunarejesha kazi ambazo tayari tulishawapa *PPRA* zinarejeshwa kwenye taasisi zingine jamba ambalo litaleta mgongano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma ukurasa namba 3 wa Mheshimiwa Waziri alipokuwa akiwasilisha hoja ya mapendekezo, nikaangalia wadau wakubwa waliokutana na Wizara nikaona kuna *TANESCO, TANROADS* na taasisi zingine, lakini kwa masikitiko makubwa sikuona *National Board of Materials Management* watu ambao ndio muhimu, ndio wataalamu wanaotakiwa kuongoza katika masuala ya *procurement*. Sasa sijui ni kwa bahati mbaya Mheshimiwa Waziri alisahau au hawakuwa *consulted* au wao wenyewe walishindwa kutoa ushauri wao. Lakini sababu hiyo iliyosababisha hawa *National Board of Materials Management* wasio *consulted*, inapelekea wanaopanza kutaja sifa za Mkurugenzi Mkuu wa *PPRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kifungu 23 kinataja sifa za Mkurugenzi Mkuu wa *PPRA*. Lazima tukubali katika dunia hii, kwa mfano mimi kama mchumi siwezi kuomba hata siku moja kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *PPRA*. Waliosomea mambo hayo watanishangaa na watanidharau.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hiki kifungu kinachopendekezwa kinasema mwanasheria, mchumi, mwanamuziki anaweza kuwa. Sasa hii sikubaliani nayo ushauri wangu ni kwamba lazima tuheshimu *profession* za wataalam. Tunayo *Board* ya *Materials Management*i na wataalam walio bobea katika masuala ya *procurement*, basi ni vizuri sifa hizi hata tunapozitaja, tuanze kutaja. Hapa Tanzania tuna bodi nyingi, kwa mfano tuna *Professional Board* ya Madaktari, huwezi ukakuta kule mwanasheria eti ndio anakuwa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, ukienda kwa wakandarasi, utakuta kuwa Mwenyekiti wa hiyo Bodi au Mtendaji Mkuu lazima awe mkadarasi aliyesomea, ukienda kwa wahasibu kule, ili uweze ku-*add* ile *professional body* lazima uwe mtaalamu wa Uhasibu. Lakini unapokuja kwenye *Materials Management* inakuwa tofauti; naomba niseme tunalo tatizo katika nchi hii ambapo kila mtu anafikiri anaweza kufanya kazi za *procurement* hiyo siyo sawa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia haraka haraka kuna utaratibu wa kuweka *lots* unapo-*advertise tender*, kama *tender* ni bilioni 40, 50 ni vizuri kuweka *lots* ili upate watu wengi wanaoweza kufanya kazi hiyo na ifanyike kwa haraka. Najua hapa Tanzania kuna taasisi moja ilijaribu kufanya hivyo, tulipongeza kwa hatua hizo lakini tulikuwa tunapongeza hatua ambazo walifanya kwa ubunifu wa watu waliokuwepo wakati huo siyo utaratibu ambao sheria ilikuwa inaruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo ningependa nishauri ukienda kifungu kinachozungumzia suala la kwamba *tender board* ikutane mara moja kwa *quarterly*. Lakini Sheria ya Manunuzi ukiiangalia inaitaka *Procurement Management Unit (PMU)* wakutane kila mwezi na taarifa yao waiande kwaajili ya kuiwasilisha kwenye *tender board* na *PMU* lazima wakutane na wanashughuli nyingi za kufanya, lakini wakati huo huo tumeamua sasa kwamba *tender board* ikutane mara moja kwa miezi minne ili kubana matumizi. Maana yake ni kwamba ule urasimu tunaoukwepa tunarejea kwenye urasimu huo huo kwa sababu *PMU* itakaa kulingana sheria inavyotaka, lakini haitaweza ku-*reporti* kwenye *tender board* mpaka baada ya miezi minne ambapo sasa *tender board* ndipo inapokaa. Kwa hiyo tunaondoa urasimu mmoja, tunarejesha urasimu wa aina nyingine

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa hili ni la kisheria zaidi, nitaomba Serikali ilitizame tunawataja katika sheria hii kwamba kifungu cha 83, tunapendekeza kufungua kampuni itakayojihusisha na rushwa si chini ya miaka kumi; ukishasema itapewa adhabu si chini ya miaka kumi maana yake itategemea siku hiyo Hakimu ameamkaje, anaweza akatoa hata miaka 50, hata 100. Sasa hilo kwangu ni changamoto. Lakini pia nchi hii, tunazo sheria nyingine zinazoshughulikia masuala ya rushwa, juzi tumepitisha mabadiliko hapa, tumeanzisha na mahakama ya kushughulikia masuala ya uhujumu uchumi. Kama kuna sheria nyingine zinazoshughulika na masuala ya rushwa

kwa nini basi tusiache sheria hizo zikafanya kazi kuliko kufanya mabadiliko hapa, ambayo tunampa Hakimu uamuzi ambao ni *pendulous box* huwezi kujua anachukua hatua zipi? Lakini kwa sisi ambao siyo wanasheria tunajua kwamba pale inapotokea kuna sheria iliyotungwa awali inashughulikia jambo hilo hilo; unapokuwa unatunga sheria mpya lazima uhakikishe sheria hiyo unayotunga isigongane na zile sheria nyingine ambazo tayari zipo. Mimi nadhani wanasheria wanalielewa hili na wataweza kulifanya kazi kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, la mwisho kabisa ni dogo tu, ukiangalia *corruption mult-practice* ni ipi kuna sehemu wametoa *definition* hawakuweka *comma* wamesema *giving receiving* sasa nimejaribu kutafuta kwenye *dictionary* zote za kiingereza nini maana ya *giving receiving* nimekuta hana maana, kwa hiyo ninashauri koma iongezwe pale, *giving* ni jambo moja na *receiving* ni jambo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Dkt. Kamala natumaini baadhi ya marekebisho yako umepeleka jedwali la marekebisho. Tunaendelea Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika huu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwapongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuleta marekebisho haya ya sheria hii ambayo imekuwa ni kikwazo kikubwa katika majukumu mbalimbali ya Serikali huko nyuma. Kwa kweli nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza niipongeze Serikali kwa kuamua kuleta vifungu vya kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi. Tumekuwa tunatumia muda mrefu sana katika mchakato wa manunuzi. Na wakati mwingine katika baadhi ya taasisi kama huna wataalam, kama wale wa *PMU* hawajajiandaa inaweza ikafika mpaka mwisho wa mwaka bado mko kwenye mchakato wa manunuzi, kwa hiyo hii ya kupunguza muda, kwa kweli naipongeza sana Serikali ni kitu kizuri sana tulichokuwa tunakisubiri; hili ni suala la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nimefurahishwa sana katika muswada huu, ni hii ya kuiondoa wakala wa ununuzi wa bidhaa za umma yaani *GPSA* kuiondoa katika kupanga bei. Hili lilikuwa ni tatizo kubwa, *GPSA* ilikuwa inalalamikiwa kila mahali na bei ambazo zilikuwa zinawekwa

katika mikataba zilikuwa ni kubwa sana haziendani na hali halisi. Sasa kuiondoa kwamba wasipange bei nadhani hii inakwenda vizuri sana na sheria ya sasa ambayo kwa marekebisho haya yanataka taasisi zitumie bei ya soko; kitu ambacho ni muhimu sana. Hii ilikuwa ni changamoto kubwa sana lazima tutumie bei ya soko, unakuta mfuko simenti unauzwa shilingi 15,000 bei ya soko, kwenye mikataba shilingi 20,000, 30,000 hii haikubaliki. Kwa hiyo marekebisho haya ni ya muhimu sana lazima tuyaunge mkono, mimi nafikiri ni suala la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na *GPSA* kuna tatizo lingine lipo *TEMESA*. *TEMESA* haijazungumzwa kwenye hii sheria nayo imekuwa ni matatizo kwenye utengenezaji wa magari na vipuri, bei ambazo zimekuwa zinawekwa na *TEMESA* ukienda mitaani ziko tofauti kabisa. Sasa hilo halikubaliki, lazima Serikali itazame hapo ifanye nini ili kuweza kurekebisha kusudi tuweze kutengeneza magari katika bei ambazo zinakubalika kwenye soko. Siyo zile ambazo zinawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho nilitaka kuchangia kwenye hii nimefurahishwa sana na hii sheria kwa kuleta sasa upendeleo maalum kwa kampuni za kizalendo, zinazomilikiwa na Watanzania. Hii ni suala la msingi sana kwa sababu mara nyingi kwenye upande wa *construction* makampuni mengi yaliyokuwa yanafanya kazi nyingi yalikuwa ni ya kigeni, na makampuni ya ndani yamekuwa hayapewi kazi kwa sababu ya kukosa mambo fulani fulani. Sasa hii ambayo imewekwa kwenye sheria ya kuwapa upendeleo wa makusudi, maalum nadhani ni suala la msingi sana ambalo limewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini haijaishia hapo na wataalam wa ndani kwamba tutumie wataalam wa ndani ili kuwajengea uwezo waweze kuchangia katika maendeleo ya nchi; hii nafikiri itatuletea maendeleo endelevu. Hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu tukiendelea kutegemea wataalam kutoka nje, hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu tukiendelea kutegemea makampuni yanayotoka nje, lazima tuyajengee uwezo makampuni ya ndani, haya ndio yatakayoweza kuleta maendeleo endelevu. Hili nafikiri ni suala la msingi sana ambalo naliunga mkono.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu ununuzi katika Serikali za Mitaa, tumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye Serikali za Mitaa na huku ndio kuna matatizo mengi sana, mara nyingi kampuni nyingi ambazo zimekuwa zikifanya kazi kwenye Serikali za Mitaa zimekuwa zikiwa na matatizo mengi, nadhani kuna haja sasa ya kurekebisha vizuri, kulikuwa na kanuni zile zinazohusu manunuzi kwenye Serikali za Mitaa na kanuni za hii, mimi namwomba Mheshimiwa Waziri, hizi kanuni ziwe *harmonized* tuwe na kanuni moja inayo-*apply* sehemu zote; hizi kanuni ambazo mara nyingine ziko huku, nyingine huku zina toa *loopholes* kwa watu kutumia zile

nafasi vibaya na kufanya fedha za umma zipotee kwa kiwango kikubwa. Hili ni suala la msingi ambalo lazima tulizingatie katika kuweza kuhakikisha kwamba mambo yetu haya yanakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kwenye Halmashauri kuna tatizo lingine, mimi nilikuwa nafikiri mwelekeo mzuri Halmashauri zingeshauriwa pale zinapoweza kununua baadhi ya vifaa zinunue zenyewe halafu zifanye kazi ziajiri vibarua wa kufanya kazi; ingekuwa ina maana sana. Mimi sielewi kwa nini ni lazima kama Halmashauri inaweza kununua *grader* kwa nini tumpe *contractor,* kwa nini sheria ilazimeshe kwamba lazima ipewe *tender?* Mimi nilikuwa nafikiri ni lazima sasa kama tuna *grader* tuajiri vibarua wa kuweza kufanya hizo kazi na tulime barabara kwa wingi hilo lingekuwa ni la msingi sana. Kwa hiyo ningeomba sheria iliangalie hilo, na ione namna gani tutakavyoweza kulitekeleza iatusaidia sana katika kuweza kusaidia kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi sheria ilivyo inataka kila kitu kiende kwenye *tender* hatuwezi kuweka kila kitu kiende kwenye *tender,* haiwezekani hilo ni la msingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo nilitaka kuchangia ambalo naliona sasa lilikuwa ni tatizo la mfumo huu wa ununuzi ni suala la bei, sheria ilikuwa imeweka kigezo kwamba bei huwezi uka-*negotiate*, huwezi uka-*bargain* bei ikapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mtu ameweka bei za ajabu; nataka kweli afanye kazi au yupo peke yake au wapo wangapi kwa nini tusiruhusiwe, sheria hii sasa inaruhusu kuanza ka-*bargain* bei mimi ninadhani hili ndio suala la msingi sana, lazima tu-*bargain* bei, iendane na hali halisi pale tunapoona kwamba bidhaa ambazo mzabuni ameweka haziendani na hali halisi, tumwambie bei ya soko sio hiyo rekebisha kama unataka kazi na irekebishwe ili kazi ziweze kwenda na tuweze ku-*save* hela za umma na tuweze kupata thamani halisi ya fedha za umma.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa nilichangie ni kuhusu *value for money,* ni kitu muhimu sana, haiwezekani katika hali ya kawaida mimi nikienda dukani nanunua kitu kwa shilingi 500 ukisema unatoka kwenye taasisi ya umma wanakwambia shilingi 5,000 hii haikubaliki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haikubaliki kwa sababu; sababu nyingine ambazo wanazitoa nyingine zina maana lile suala la kusema kwamba eti malipo ya Serikalini yanachukua muda mrefu sana kwa hiyo zile bei zinakuwa na *interest* hii nadhani ni *message* inafika kwenye Serikali mliangalie hilo. Hakuna sababu ya kuchelewesha sana malipo walipwe kwa wakati na hili

tuachane nalo. Lakini bei lazima tuzingatie bei ya soko na tuzingatie thamani halisi ya bidhaa tulizonunua, sasa hivi vitu vingi unakuta haviendani na hali halisi *value for money* haiwi-*considered* hasa hili ni tatizo kubwa ambalo ninaamini kabisa katika hii sheria ni muhimu sana ikalitekeleza na ikaliangalia, naamini Wizara wataliangalia kwa undani zaidi ili tuone ni namna gani tunaweza kulitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa nirudie kwenye lile suala la kanuni za ununuzi wa umma, kuna baadhi ya vipengele vilikuwa vinakinzana na sheria kuu.

Mheshimiwa Waziri naomba ukaviangalie vizuri vile vipengele vinavyokinzana, vipengele vingine vilikuwa vinaweka utaratibu huku tofauti unakuta kwenye kanuni zinakuwa ni tofauti. Hasa naomba hizi ukaziangalie vizuri ili ziwe *harmonize* ziendane na sheria inavyotaka. Lakini zaidi ya hapo hizi kanuni zisichelewe, sheria hii inatakiwa ianze kufanya kazi; mimi niliamini inaanza kufanya kazi tarehe 1 mwezi wa 7, kesho kutwa. Lakini sasa kama kanuni zitachelewa zitasababisha hii sheria iendee kutumika na tuzidi kuchelewa zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba muliangalie hili muziharakishe hizi kanuni zije kwa wakati ili haya marekebisho ambayo yamepitishwa na hii sheria yaweze kufanya kazi ile ambayo tunaitarajia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo napenda niseme naunga mkono hoja, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Martha Moses Mlata na Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati ajiandae.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na mimi pia kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu alipolihutubia Bunge letu aliona udhaifu na mapungufu ya sheria hii ya manunuzi na ndio maana leo nashukuru Mawaziri wetu wametuletea ili tuweze kuirekebisha kwa manufaa ya Taifa letu. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa nia yake njema ya kuokoa na kuondoa vichaka maana yake sheria hii ilikuwa ni vichaka kwa watu ambao sio waadilifu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini baada ya pongezi hizo mimi sitakuwa na mengi sana kwenye sheria hii kwa sababu sio mtaalamu sana kwenye mambo ya sheria ya manunuzi lakini kuna maeneo mengine ambayo ninaona nitoe ushauri hasa kwenye upande wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukachanganya hii Sheria ya Manunuzi pamoja na manunuzi ya dawa za binadamu, huwezi ukalinganisha *tender* ya pembejeo za kilimo au *tender* ya kutengeneza barabara au *tender* ya kuagiza vipuli na dawa ambazo zinatumiwa na binadamu. Ninazungumza hivyo kwa sababu sheria hii imekuwa ikichukua muda mrefu sana katika masuala ya uagizaji wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaongea haya labda ni*declare interest* kwa sababu mimi nilikuwa mjumbe wa Bodi ya *MSD,* ninafahamu matatizo makubwa ambayo *MSD* wanayapata namna ya kuagiza dawa kwa kufuata Sheria hii ya Manunuzi. *Tender* itatangazwa mwezi wa tatu lakini mpaka sasa ukienda bado hata wale ambao wamepata *award* kwa ajili ya kuleta labda dawa bado kabisa mlolongo ni mrefu, apate zile *awarded letter*,aje aende apate mkataba, aende kwa *AG* maana yake na zile kanuni naona walizirekebisha lakini bado hazisaidii aende kwa *AG,* atoke pale afanyiwe *vetting,* akitoka kwenye kufanyiwa *vetting* arudi sasa aende kutoa *order* na akitoa *order* dawa ile ikatengenezwe kule kiwandani ni miezi mitatu, kwa sababu *MSD* wana nembo yao kwa hiyo ni lazima watoe *order* kiwandani ili zile dawa zitengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri hili mliangalie msichanganye hii Sheria ya Manunuzi ya dawa za binadamu na manunuzi ya vitu vingine, ninaomba sana hili mliangalie. Mnaweza mkawa mmeliweka kama mlivyoliweka, lakini hebu mtakapokwenda nendeni mkaangalie na kama mkiona kuna uzito wala msisite lileteni tena hapa ndani ili tuokoe maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninazungumza hayo kwa sababu mimi ninaelewa kwanza kabisa dawa asilimia 80 zinatoka nje, lakini makampuni mengine yanatoka nje yanakuja ku-*register* dawa hapa, yanapo- *register* dawa yanasubiri *MSD* atangaze *tender, MSD* anapotangaza *tender* wao kazi yao ni kuvizia na unakuta wana- *tender* kwa bei ya chini lakini huwezi kujua hata hizo dawa wanakwenda kuzinunua wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa ninaomba sana tuliangalie suala hili na ushauri wangu ni kwamba kuwe na utaratibu kwanza ninashukuru kwamba makampuni ya ndani yanapewa kipaumbele, mimi kwa kweli ninashukuru. Lakini utekelezaji wake, mimi ninawaamini sana Waheshimiwa Mawaziri na watendaji wenu na ninaamini kupitia ile kauli mbiu ya hapa kazi tu. Lakini ninaamini pia kwa kauli mbiu ya kutumbuliwa majipu, nilikuwa ninaomba sana kauli ya utumbuaji majipu uendelee kuangalia ni namna gani makampuni ya Kitanzania hayanyanyaswi. Kwa sababu makampuni ya Kitanzania yananyanyaswa na makampuni ya nje wanakuja na bei za chini kwa kisingizio

kwamba Watanzania wananunua vitu vya bei ya chini. Lakini matokeo yake dawa zinazoletwa zinakuwa ni *fake* wala sio bora kwa Watanzania.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilikuwa naomba sana tuangalie bei, lakini lazima uangalie na ubora wa kile kitu unachompelekea Mtanzania hasa kwa afya yake. Kwa hiyo hilo ninaomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa sababu hatuna viwanda vya kutosha vya madawa tunategemea viwanda vya nje, nilikuwa naomba makampuni ambayo yanakuwa *registered* hapa Tanzania ya wazawa au ya nje, wao wawe ni mawakala au ma-*agent* wa viwanda fulani kule nje ili *MSD* anapotoa tenda kwa kampuni ile bado atoe *copy* kwenye kiwanda ambacho yule mtu amesema atatoa zile dawa. Kwa sababu walio wengi wana *cheat,* watasema kwamba dawa zile wanaenda kuzitoa labda tuseme Malaysia, India au *whatever,* lakini bado unaweza ukakuta wapo Keko pale wanatengeneza dawa pale, wanaziingiza *MSD* wakijifanya wamezitoa nje kumbe zile dawa ni *fake*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba kuwe na mahusiano kati ya viwanda ambavyo vimetambuliwa na nchi yetu ambavyo vinatu-*supply* dawa ili wale ma-*agent,* wale *bidders* watuambie zile dawa wakipata *tender* watakwenda kununua wapi lakini bado *copy* iende ili tupate bei iliyo sahihi ambayo sio ya kudanganya.Kwa hiyo, mimi niliona nizungumze tu kwenye eneo hili wala sikutaka kuzungumzia sana maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Kingi, Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hii *Procurement Act*.

Kwanza kabisa na mimi nianze kumpongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kuleta hii sheria kwa sababu tumekuwa tukiipigania muda mrefu sana na tunaamini sasa uletwaji wa hii sheria itatusaidia pia hata Serikali kuongeza pato la Serikali na watu ambao walikuwa wanakwepa kulipa kodi na wale ambao walikuwa wanafanya *tender* kwa upendeleo hasa angalau itasaidia hii sheria kuleta haki sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niwapongeze Kamati ya Bajeti kwa sababu kwa kipindi tu kifupi wameweza kutuletea hotuba yao nzuri japokuwa tumechelewa kuisoma, lakini ninaimani kwamba sheria hii sasa inaenda

kutendewa haki. Pia nimpongeze Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa sababu siku zote huwa anakuwa anatuletea sheria nyingi, lakini tunakuwa hatumpongezi, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kupongeza Serikali kwa kuiondoa *GPSA* kupanga bei kwa sababu kwa kweli ilikuwa ni tatizo kubwa sana kwa kutupangia bei kwa wazabuni.

Mheshimiwa NAibu Spika, jambo la pili, nilikuwa nataka kujua hii *GPSA* bado ilikuwa inachagua wazabuni wachache ili waweze ku-*tender* hizo zabuni. Sasa je, katika sheria hii inasemaje maana yake zamani wakati *GPSA* haipo hizi *tender* zilikuwa zinatangazwa magazetini na kila mtu anatendewa haki, ku-*tender* hizo zabuni. Sasa labda sheria ituambie je, *GPSA* wameondolewa na ile kuchagua wazabuni wachache katika ku- *tender* hizi zabuni?

La pili pia hii *GPSA* ilikuwa inatoza ile asilimia mbili ya gharama ya mkataba je, na hii asilimia mbili imeondolewa? Nilikuwa nataka nipatiwe majibu ya hilo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, ukisoma hotuba ya Waziri ukurasa wa saba namba "E", niipongeze kwa sababu imeweka mfumo utakaotoa upendeleo kwa makundi maalum kwa akinamama, vijana, wazee na makundi maalum ya walemavu. Lakini nilikuwa naomba labda sheria hii ingeweka wazi, je, ni asilimila ngapi sasa hayo makundi yatapatiwa? Labda nitoe mfano, kama watatoa asilimia 30, kwa sababu kina mama wengi sana wamekuwa wakifanya biashara tunaona kabisa tofauti labda na vijana na haya makundi mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kama itatoa asilimia 30, ingetamka kwamba asilimia 15 basi wapatiwe akina mama na asilimia 15 yagawane haya makundi mengine. Hili litawasaidia akina mama wengi sasa hivi wamekuwa wakifanya biashara lakini wanaona kwamba hawapatiwi huo upendeleo ambao watapatiwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukisoma pia kipengele "G" namba hiyo saba inasema kwamba; kuweka sharti la kutumia mfumo wa *electronic* katika ununuzi na kuongeza uwazi na uwajibikaji. Labda kanuni zingeeleza jinsi ya kuelimisha kutumia hizi mashine za *EFDs* kwa sababu itasaidia kama wangewekewa uwezo wa kujua hizi mashine, kwa sababu utawakuta akina mama wengine wako huko vijijini, hakuna umeme, hakuna nini, sasa labda wangetoa elimu na kuwajengea uwezo ili waweze kuzitumia hizi mashine kuliko ilivyo, haijaeleza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilikuwa naomba labda katika sheria hii tungeona kipaumbele cha Serikali kuwalipa wazabuni kwa wakati. Kwa sababu utakuta kwamba zamani wazabuni Serikali ilikuwa haiwalipi kwa wakati, wanaweza wakapewa *tender* labda kwenye mashirika au taasisi za umma, lakini malipo yao yanachukua muda mrefu sana. Je, hii sheria sasa itaibana Serikali kuweza kuwalipa hawa wazabuni kwa wakati? Kwa sababu utakuta wazabuni wanadaiwa na wazabuni wanatakiwa sasa waki-*issue invoice*, wanatakiwa pia watoe risiti na *TRA* wanatakiwa sasa wakusanye kodi kwa hao wazabuni. Lakini wazabuni hawajalipwa, *TRA* wanawadai, na *TRA* usipolipa wao wanatakiwa wakupige *penalt*. Sasa je, sheria hii inamlindaje mzabuni?*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo, naomba tu kuunga mkono sheria hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Asante, Mheshimiwa Ali Hassan King, atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola ajiandae.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwanza na mimi napenda nimshukuru Mwenyenzi Mungu, ambaye ametujalia uhai na uzima katika siku ya leo kuja kujadili sheria hii ambayo ya mapendekezo iko mbele yetu ya *procurement,* ambayo imelenga kuokoa gharama na fedha nyingi za Serikali ambazo zinakwenda katika matumizi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Waziri wa Fedha na timu yake kwa kuleta muswada huu kwa wakati ili kuokoa fedha hizo, lakini pia napenda kuishukuru Kamati ya Bajeti nayo kwa kufanya uchambuzi na kupendekeza mambo tofauti ambayo yameboresha sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekusudia kuongea mambo mawili katika kuchangia muswada huu wa sheria, jambo la kwanzani matumizi ya *health commodities,* au manunuzi ya *health commodities,* vifaa tiba ambalo aliongelea kwa upana zaidi Mheshimiwa Martha Mlata, ameongelea kiundani zaidi. Sasa mimi mapendekezo yangu yanakuja hapa, kwa sababu hivi vifaa tiba kikawaida vina sifa ya kwamba vinaokoa maisha ya mwanadamu na hasa hasa katika afya za mama na mtoto ndio usiseme. Zitaokoa maisha ya watanzania kwa ujumla, kwa hiyo kuna uharaka wa kufanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu la kwanza, kungekuwepo na kifungu maalum ambacho kinaelezea hivi vifaa tiba. Lakini kama hilo halikuwezekana la kuwa na kifungu maalum cha kuelezea vifaa tiba, katika mapendekezo ya sheria kifungu cha 24 kimeeleza kwamba kitaongeza ibara ya 65A, ambapo hapo kutatajwa *specialized goods,* zimetajwa *all services* ambapo labda hapa inawezekana vikaingia hivi vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili neno la *specialized goods or services* kwamba bado halijawa maalum sana au liko *general.* Kwa hiyo, labda katika uchambuzi wake lingechambuliwa tukaelewa ni vifaa vya aina gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine katika kifungu hicho hicho ambacho kimeelezea habari hiyo ya *specializes goods* cha 65A(2) ambacho kimependekezwa kimempa mamlaka Waziri kutunga kanuni, katika kanuni hizo ambazo atataja hivyo vitu kwa undani wake, basi ndani ya hizo kanuni tulikuwa tunamuomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia hizi *health commodities* au vifaa tiba kwa lugha ya kikwetu, ili viweze kwenda sambamba. Kwa hiyo, vifaa tiba hivi vitakapopatikana vitaweza kutuongezea thamani ya maisha ya wanadamu katika nchi yetu. Lakini pia ili iweze kwenda sambamba na azimio la Wizara ya Afya, sasa hivi katika manunuzi tumewasikia wamejipanga kivingine, kwa hiyo iweze kuboreshwa katika hivyo vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mchango ilikuwa ni katika masuala hayo ya vifaa tiba, ambayo pia katika sheria kuna kifungu cha 67 cha sheria mama, ambacho kiongezwe, wafanye marekebisho katika kifungu hicho ili kiweze kukaa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika suala lingine, ambalo lilikuwa lina changamoto kubwa ya kutokuwepo kwa vigezo vya mahitaji ya sekta ya umma yaani *standards,* ilikuwa hakuna *standards.* Kwa hiyo, sheria iliyoongezwa 65B katika kifungu cha 24 cha mapendekezo ya sheria kimeeleza kwamba zitatumika hizo *specialized standards.*Kwa hiyo hizo *standards* zitakazotumika bado haijaelezwa ni za aina gani, bado iko *general*. Kwa hiyo itolewe ufafanuzi, itakapotolewa ufafanuzi inaweza ikaleta maana zaidi. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ambacho kwa ajili ya kuboresha sheria hii pia Waziri amepewa mamlaka katika kifungu kinachofuata cha 65B(2) Mheshimiwa Waziri amepewa mamlaka tena ya kutunga *regulations.* Basi atakapotunga *regulations* kwa sababu unapoweka *standards* wakati mwingine kuna watu wanaweka *standard* kwa sababu wameshajua kwamba anaenda kununua kwa nani.

Mheshimiwa Naibu Spika,kwahiyo zinawekwa standard kama zina m**-***lead* yule mnunuzi kwamba aelekee kwenda kununua kwa mtu gani. Kwa hiyo hii nayo itakuwa inafanyika uongo, sasa uongo huu ili uweze kuwa *covered.* Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri katika kanuni ambayo umepewa nguvu na Kifungu hicho cha pili cha 65B basi aweze kuweka kifungu cha adhabu kwa watakaofanya makosa katika kuweka *standard*. Kwa sababu wengine wanaweza wakaweka *standard* za makusudi, za uongo ili kuweza kupotosha, kwahiyo naishauri Serikali katika suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine mambo niliyokusudia mawili ni haya ambayo nimeongea lakini jingine nikupongeze wewe mwenyewe kwa kusimama madhubuti katika kiti chako na kusimamia kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana ya kanuni ni sheria na waswahili tunasema sheria ni msumeno, kwa hiyo na msumeno Al Marhumu Issa Matona alisema kwamba; hukata mbele na nyuma msumeno kazi yake. Usiutie lawama ufanyapo kazi yake. Kwa hiyo na wewe unatumia kanuni naamini unakata mbele, unakata nyuma kwa sababu unatumia kanuni. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini aliendelea Al Marhumu Issa akasema kwamba, usitumie mkono kutaka kujiharibia, utakutoka mguno tayari umeshaumia, ukileta mabishano bure utakujalia. Kwa hiyo wenzetu wametumia mkono kutaka kujiharibia hizi kanuni na tayari umeshatoka mguno wameshaumia hawamo ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kukupongeza huku, pongezi ambazo zimewafanya watu wanune wasikae humu ndani, maana yake kwamba, wameambiwa wasikae humu ndani lakini pia wamepewa sharti kwamba wasitusemeshe, wasitusalimie.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilimsamilimia mwanaume mwenzangu akanitikisikia mabega hivi, kanijibu kwa mabega. Kwa hiyo mimisikumfahamu vizuri lakini kule kwetu kuna msemo mmoja au kuna kanuni moja kwamba mtu ambaye anaweza akamwambia bwana usimsemeshe fulani, fulani akikusalimia usimuitikie mara nyingi mume huwa anamuambia mke kwamba akikusalimie fulani usimsemeshe wala usimuitikie. Kwa hiyo na wao hiyo amri sijui wamepewa na nani maana hawatusemeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kushangaza ambayo misemo yakiswahili ipo, kama mzazi ameenda hospitali kujifungua kwa bahati mbaya mtoto akapita tunasema yule mtoto sio riziki kapita, na pia akiolewa dada yetu yeyote akipata mume lakini mume hatimizi majukumu ya nyumbani watasema kaolewa lakini mume sio riziki. Kwa hiyo na majimbo yale meupe kweli yana Wabunge lakini wale Wabunge sio riziki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naunga mkono hoja mia kwa mia na tunamuomba Mheshimiwa Waziri achukue marekebisho ambayo tumeyapendekeza, ahsante nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni atafuatiwa na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mheshimiwa John Kadutu ajiandae.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba nichukue fursa hii kwanza kuipongeza Serikali kwa kuleta hii Sheria ya Manunuzi. Mimi kwangu na ninaamini kwa Wabunge wote hii sheria ndiyo sheria muhimu kuliko sheria zote kwa sababu manunuzi yote ndiyo yanaenda kufanywa huko. Hii ndiyo sheria ambayo italeta taswira kwamba uchumi wetu utakua au hautakua, kwa hiyo nawapongeze kwa hilo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba Waziri wakati mnaandaa kanuni, mjitahidi sana kuhakikisha mnaweka dirisha. Moja, kwenye suala la *PPP* kwa sababu ile Sheria ya *PPP* bado inafanyiwa marekebisho ili isije ikawa kwamba mahali ambako Serikali sasa inataka kuingia ubia na *private sector* acha kwenye hii miradi mikubwa mimi nazungumzia hasa hizi za kwetu za ngazi ya Halmashauri/ngazi za chini ambapo 80% ya maendeleo inaenda huko pawe na dirisha ambapo Halmashauri ikitakiwa kuchangia na sekta binafsi kwamba, wale wadau wa maendeleo pawe na fursa kwamba, Halmashauri ichangie kiasi fulani, wadau wanachangia kama ni vifaa ili kazi zionekane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niendelee kushauri kwamba huko ngazi ya Halmashauri tunakuwaga na*suppliers* kwamba, mwanzo wa mwaka tunachagua wale watu ambao watakuwa wanatoa huduma kumi ambao watakuwa wana-*supply* kwenye Serikali, naomba hiko kifungu kiondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila *tender* inapotoka au kila tunapotaka kufanya iwe wazi yeyote yule ambaye anataka kuingia kwenye huo mfumo wa kuomba kutoa huduma au kufanya kazi waruhusiwe kwa sababu inawezekana kipindi fulani Januari mnachagua watu kumi mwezi Machi tayari sasa dira au yule mtengenezaji akaweka *godown* yake pale kwamba unaweza kununua moja kwa moja kwa bei ya kiwandani kwa mfano kwa *cement* yaani *agent* wake akawa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ni vizuri kwenye vikundi vidogo vidogo ambavyo havijasajiliwa kuwe na dirisha sisi tutaenda kuhamasisha vikundi vijisajili hata kama ni wale wamama wanaouza sokoni basi wawe na mashine yao moja ya *EFD*. Yeyote anaye-*supply* pale risiti ikitoka pale sokoni ili zile *supplies* na wale wapate riziki ambayo wanastahili kupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo hii wanao-*supply* chakula, wanao-*supply* bidhaa ndogo ndogo katika hizi *tender* ndogo ndogo unakuta gharama ni kubwa sana wakati tungeweza kupata kwa bei ya chini. Yule mtu wa chini hapati kwa sababu hajasajiliwa, ni muhimu sasa twende kuwashawishi waendelee kusajiliwa ili na wao wapate fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini muhimu nyingine kwenye suala la *standards;* kila Wizara unakuta inakuwa na*standards* zake, Wizara ya Mambo ya Ndani inaruhusu kujenga majengo yao kwa *hydraform blocks,* lakini Wizara ya Elimu ukitaka kujenga darasa kwa *hydraform blocks* hairuhusiwi wanakuwa na *standards* zao. Sasa tungekuwa na *uniform standards* kwamba *standard* moja kwenye Serikali ikikubalika kote basi iendelee kukubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, nilikuwa nashauri yale maoni yote ya Kamati ya Bajeti basi pia yachukuliwe kwa uzito wake na pawe na *special provisions* kwa zile *public entities* ambazo zinafanya biashara *competitive business* kwa mfano *TTCL* na nini muiwekee *special provision* kwamba wao pia wakitaka kufanya manunuzi basi wasifate ule mlolongo wa kawaida ni ili taasisi zetu zifanye kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye *life saving health commodities and equipment* nilikuwa naomba hiyo iwekwe. Lakini pia kwenye kile kifungu cha kununua vifaa vilivyotumika ambapo tuna ndege, meli na reli lakini viongezwe vifaa vya afya hizi *life saving health commodities.* Kwa sababu kuna vifaa vingi vya tiba ambavyo ni *used* kwa mfano vitanda vya akina mama kujifungulia. Hata ingekuwa kimetumika mara ngapi bado ile kwetu kijijini itaweza kuokoa maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya vifaa ambavyo sio *electronic* basi vile vifaa baada ya kupitishwa na Waziri husika viruhusiwe kununuliwa ikiwa *used* pamoja na vifaa vya kilimo. Kuna vifaa vingi sana vya kilimo ambavyo Serikali kwenye mashamba yake ambayo tunataka kuanzisha uzalishaji wa mbegu.Wanaweza kununua vifaa vingi ambavyo ni *used* kwa mfano ma-*rippers* na nini. Bei yake mpya ni dola 65000 ya *used* unapata hata dola 10,000; sasa pawe na dirisha kwa vifaa vile ambavyo havina mwisho katika maisha yake basi viruhusiwe kununuliwa vifaa ambavyo vimetumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ningeshauri kwamba tuangalie katika kanuni, muhimu kuliko yote manunuzi yote nimeona katika sheria hii ya Halmashauri zetu zinaenda kule kwenye kanuni. Sasa wakati wa kanuni tutaendelea kumuomba Waziri, sisi tutaendelea kuleta *input* zetu ili ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ninaomba ombi lingine kwa Serikali, naomba hii sheria tukiipitisha mwakani muirudishe ili ndani ya huu mwaka mmoja haya majaribio yote tunaenda kufanya, mapungufu yote ndani yamwaka mmoja tuje tuzibe ile mianya yote, tusije tukakaa miaka minne kama tulivyofanya 2011, tukarudia mwaka 2014 mwishoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kila wakati tukiweza kurekebisha ninaamini huku tunakotarajia kufika tutaweza kufika. Muhimu kuliko yote pia ni kuangalia namna wakandarasi yaani Watanzania wanaweza kushiriki katika manunuzi iwe katika nanii kubwa au ndogo. Ninashukuru kwamba Serikali imekubali kwamba, hata katika ukandarasi mahali ambapo wanatakiwa kwenda kufanya tathmini na nini kuna namna ambapo watu wetu wa ndani wakishiriki basi na wao watakuwa wanapata fursa ya kupata ile elimu na fursa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye Halmashauri naomba muendelee kuangalia kwa mfano kama *TEMESA* magari yetu yanatakiwa tupeleke pale kutengeneza. Kama tunaweza kutengeneza kwa bei nafuu hapo hapo ndani ya mji huo sisi tufanye *quotation TEMESA* ikiwa juu kuliko hao basi turuhusiwe kupeleka kwingine ili na *TEMESA* wafanye kazi yao iwe *competitive*. Nanii yoyote isiwe kama tunapeleka kwenye taasisi ya Serikali basi watu-*charge* bei yeyote na wao pia waingine kwenye *tender* kama mtu yeyote mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama bei zao zikiwa nafuu tupeleke huko kama sio nafuu basi tupeleke mahali ambapo sisi kama Halmashauri au taasisi ya Serikali itaona kwamba inapata unafuu na inaweza ikaokoa fedha nyingi. Lengo kubwa hapa ni kuokoa fedha lakini sio kupunguza ubora wa kazi na huduma ambayo inatakiwa. Tupate huduma na ubora wa kazi ile ile tunayotakiwa kwa *standards* zinazotakiwa lakini kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *procurement* zingine zote kwa mfano kwenye ununuzi wa tiketi na nini yote hayo Serikali iangalie mifumo ambayo serikali itaendelea kufaidi na itapata *discount* kwa sababu unapofanya *bulk procurement* kwenye jambo lolote bado unaendelea kupata *discount*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niendelee kushukuru na niendelee kuipongeza Serikali kwa kuleta sheria hii. Tunaomba Waziri wakati wa kuandaa kanuni basi maoni ya Wabunge wengi ambapo tutaendelea kusimamia kule kwenye Halmashauri zetu uyapokee na uyafanyie kazi, kwa sababu kila Halmashauri inakuwa ina jambo lake la kipekee tofauti na Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ambayo yako Dar es Salaam tofauti na Babati, mazingira ambayo yako Kigoma au kwingine yanaweza kuwa tofauti. Pia wakati wa kuweka *standards* ya bei kwa mfano jengo la darasa linalojengwa Dar es Salaam na Babati na nyingine ambayo iko Mwanza au kule Kigoma ni tofauti.

Kwa hiyo mtakapoweka wastani wa bei pia katika Mkoa huo basi wao wamekaa na waangalie kwamba ndani ya Mkoa wetu wastani wa bei itakuwa ni jambo fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tukishaweza kufanya hivyo na mahali ambapo wadau wengine wa maendeleo wanaweza kuchangia. Pawe na dirisha ambapo pesa za Serikali, pesa za umma ziweze kutumika kwa kibali maalum. Nasema tusivunje kanuni, tusivunje sheria lakini pawe na vibali, pawe na *authority* ambayo itatoa hiko kibali. Lakini ili tuweze kuokoa fedha na tuweze kufanya shughuli ambayo italeta manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu kila Mkoa na kila Wilaya kabla ya kutoa kazi basi wawe wanaangalia bei ambazo ziko sokoni. Bei kama ni barabara, nyumba, ujenzi, kama ni *supplies* za vitu wawe wanatoa. Lakini muhimu wanasemaga pesa za Serikali zinachelewa bei inakuwa mara mbili, hapana! Hata kama umekopa benki basi ile bei ipande kutokana na *interest rate*. Umekopa *CRDB* kwa 21% basi weka asilimia 25 kwamba wewe umekopa hizo pesa ukicheleweshewa wewe utalipa riba ya benki iwe ni kiasi hicho sio bei iwe mara mbili au mara tatu alafu unasema kwamba pesa za Serikali huwa zinachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukiwa na uwazi katika shughuli hizi zote mimi naamini tutaokoa fedha nyingi sana na ubora wa kazi utaendelea kuwepo. Lakini Wizara ya Fedha naomba kile kitengo chenu ambacho siku zote tunaendelea kuomba kwamba *Planning and Development* kitengo hiki kiweze kutoa elimu lakini pia waweze kuwa wanapita kila wakati kuangalia mazingira ya eneo moja na eneo lingine ili shughuli hizi zote basi ziweze zikafanikiwa na tukapata manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba nishukuru na niipongeze Serikali kwa kuleta sheria hii, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mheshimiwa John Kadutu ajiandae atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye huu Muswada wa Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Yanga inacheza TP Mazembe pale Dar es Salaam na haya marekebisho tunayoyafanya leo ya sheria hii nina imani kama Yanga itashinda na marekebisho haya yatakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kulikumbusha Bunge lako tukufu kwamba, katika Bunge la Kumi Serikali iliwasilisha Muswada wa Sheria ya Ununuzi na tukatunga Sheria Namba 7, 2011 kwa kufuta kabisa Sheria Namba 21 ya mwaka 2004. Ilionekana ile sheria tulioifuta ilikuwa na mapungufu makubwa sana na hivyo Wabunge tukajiridhisha kwamba sheria tuliyoitunga kwenye Bunge la Kumi ingeweza kuondoa matatizo katika sekta ya ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni kwa bahati mbaya leo Serikali inawasilisha tena Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na marekebisho ambayo tunaenda kuyafanya leo. Nilikuwa naangalia muswada wenyewe, tunakwenda kubadilisha vifungu 40 na vifungu 40 ni vingi sana, ni vifungu ambavyo tunaenda kuvibadilisha katika hati ya dharura, kwa hiyo ninayo mambo ambayo ningependa niitahadhalishe Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwenye ukurasa wa 11 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Tulipotunga Sheria Namba 7 ya 2011 tuliangalia kwamba sekta ya ununuzi wa umma kwenye Halmashauri zetu lazima tuweke sharti ambalo linamtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kuwasilisha mbele ya Kamati ya Fedha na Mipango maamuzi yaliyofanywa na Bodi ya Zabuni ili Kamati ile iweze kuchambua na kuridhia juu ya utoaji wa tuzo kwa mzabuni aliyeshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanya vile kwa sababu ndipo sasa dhana ya *D by D* (ugatuaji wa madaraka) kwenda vijijini ulikuwa unajidhihirisha. Kamati ya Mipango na Fedha ndiyo inayofanya ziara kwenye eneo lao la Halmashauri na kukagua miradi yote ya maendeleo ambako wazabuni hawa wanakuwa wanatekeleza zile zabuni walizoshinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa, leo muswada unaoletwa mbele ya Bunge lako tukufu. Mheshimiwa Waziri anapendekeza kwa lugha ya kusema kuboresha kwa kufuta kabisa na kuondoa sharti la Kamati ya Fedha na Mipango kutopokea tena taarifa ya maamuzi ya utoaji wa zabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli kamati hii kupitia na kuchambua uamuzi huu ni kasoro na ni upungufu? Mimi nilidhani kuendelea kuwapa lungu zaidi Kamati ya Mipango na Fedha.Ndipo pale ambapo watahakikisha fedha za wananchi katika manunuzi ya umma kwenye miradi inatumika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana kamati hii inapokuwa inapokea taarifa hii na kuichambua.Wao hawaiambii bodi kwamba mpeni huyu zabuni, hapana! Wao jukumu lao ni kuangalia inawezekana katika kaguzi walizofanya za miradi wakakuta kuna mzabuni. Kampuni ya ukandarasi imechakachua mradi, imejenga mradi chini ya kiwango, wanayo mamlaka ya kuiambia bodi

kwamba huyu mkandarasi ana matatizo ili waweze kuiangalia upya zabuni ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ninamtahadhalisha sana Waziri wa Fedha na Mipango alitazame hili ili tuhakikishe kwamba sharti hili la kuipa Kamati ya Fedha na Mipango liendelee kama lilivyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala hili la bei ya soko. Sababu nyingi zinazotolewa na hasa katika muswada huu za kwamba Serikali imekuwa ikiingia hasara kwa sababu zabuni hizi wanaweka bei ya juu tofauti na bei ya soko. Na hivyo leo tufanye marekebisho kwa kutazama kwamba wazabuni hawa wawe wanaleta zabuni zao kwa kuangalia bei ya soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimtahadhalishe Mheshimiwa Waziri amejipanga vipi kuhakikisha kwamba yale mambo yaliyokuwa yanawafanya ghawa wazuni kuweka bei ya juu Serikali inayatazama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza wazabuni hawa wanapokuwa wanaleta bei zao Serikali hii imekuwa haiwalipi kwa wakati! Na hivyo wamekuwa wakiingia hasara, wanafuatilia madai yao miaka nenda rudi Serikali haiwalipi na matokeo yake hata zile fedha wanazofatilia zinakuwa haziwasaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni nyingi zimefilisika, watu wanalisha shule, wanalisha magereza lakini malipo kutoka Serikali inakuwa ni kizungumkuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, leo mnaposema kwamba walete bei za soko na wakati ninyi Serikali hamjabeba jukumu katika sheria hii hii kwamba na ninyi muwalipe kwa wakati, nina imani kwamba sheria hii tunayoibadilisha leo haitaleta mafanikio, wazabuni hawa hawa mtaendelea kupata bei za juu na vinginevyo hamtawapata wazabuni mtarudi kule kule kuanza kufanya manunuzi nyinyi wenyewe. Ndiyo maana leo hii Mkurugenzi ambaye ana *cash money* ukimtuma kwenda kwenye duka ana uwezo wa kununua bei ya soko lakini Mkurugenzi huyo huyo akienda kwa kauli ya kukopa alipe baadaye bei ile lazima haitakuwa hiyo ambayo mnaiita ni bei ya soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine Serikali imejipangaje kwenye suala la rushwa kwenye hizi tenda za zabuni? Kwa sababu rushwa ndiyo husababisha wazabuni hawa wanaleta bei ambazo ziko juu na wamekuwa wakifanya mawasiliano na wazabuni kwamba katika kujenga barabara hii au katika kuleta jenereta, katika kuleta *fridge*, katika kulisha shule ndizi moja lazima ulete bei fulani kwa ajili ya kushindana na hao wengine. Wanafanya hivyo kwa sababu wazabuni hawa au wakandarasi ili waweze kulipa ile *10 percent* ambayo ni ya *corruption* lazima waweke bei za juu, hawawezi wakatumia hela zao za mfukoni

katika kulipa hawa kwa njia ya rushwa. Kwa hiyo, nilitaka kujua Serikali imejipangaje, haya mambo ya kuwaambia wazabuni wanapoleta zabuni zao wawe wameandika kwamba hawatajihusisha na rushwa, yale yamekuwa ni maandishi tu ni makaratasi lakini bado kumekuwa na matatizo kwenye zile zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo namtahadharisha ambalo inabidi pia walichukue kwa makini, katika masuala haya ambayo tumesema kwamba tujaribu kupunguza muda wa hizi tenda ambapo mwanzoni walikuwa wanatumia muda mwingi sana, lazima ule muda tungeuoanisha na huu muda ambao tunataka kuboresha wa manunuzi ya dharura. Tusipooanisha muda huu na yale manunuzi ya dharura, nina uhakika lazima Bodi ya Zabuni watakuwa hawatengenezi ule mpango wa manunuzi kwa mwaka, watakuwa wanasubiri wajifanye kila kitu wananunua kwa dharura na watakuwa wanasubiri pia waweze kuzigawa zile tenda. Kwa sababu kwenye Sheria ya Manunuzi kuna kile kiwango ambacho hawaruhusiwi katika tenda moja Mkurugenzi kutoa maamuzi kwa ajili ya manunuzi lazima waende kwenye tenda. Kwa hiyo, ule muda tusipouoanisha vizuri na hizi zabuni za kawaida pamoja na haya manunuzi ya dharura, tunaweza tukarudi kule kule tukasema kwamba sheria tuliyoipitisha lazima tuirekebishe tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho. Leo tunakwenda kufanya maboresho 40 kwa Sheria ya Manunuzi na tunafanya maboresho haya…

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kangi, naomba umalizie sekunde 10 muda wako umekwisha.

MHE. KANGI A. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, haya, naunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa John Kadutu atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi hii kuchangia jioni ya leo juu ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ambayo imekuwa ni tatizo. Leo niipongeze Serikali kwa kuleta mabadiliko haya na kwa kusikia kilio cha Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla, Serikali imekuwa na *speed* nzuri na mimi nimeshawishika kuipongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuingia hapa mjengoni nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri kwa hiyo najua madhara na madhira ambayo halmashauri zinapitia. Ni shida sana kuitekeleza lakini mkafanikiwa, muda mwingi mnatekeleza sheria lakini upande wa pili mnaingia gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni lile alilosema Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Hawa Ghasia, sina hakika kama ni kanuni au ni waraka lakini mimi nadhani ni waraka. Serikali iufute ule waraka uliokataza Waheshimiwa Madiwani kujadili mambo yaliyokuwa yamefanyika wakati Waheshimiwa Madiwani wako kwenye mchakato wa uchaguzi, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza mengi yamepitisha mambo haraka haraka hasa ya manunuzi haya kwa kujua Waheshimiwa Madiwani wangekuja na kuchambuachambua. Kwa hiyo, jambo hili lazima Serikali iwe inasikia kama ilivyosikia kuleta mabadiliko, sioni tatizo kama Serikali inaweza kufuta waraka uliotolewa na Katibu Mkuu wa TAMISEMI wakati huo. Jambo hili litaturahisishia sana kuondoa ugomvi kati ya Madiwani na Watendaji wetu wa Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la Bodi za Zabuni. Mimi niishauri sana Serikali na hasa viongozi wa Serikali Mikoani kutokuziingilia Bodi za Zabuni. Mara nyingi bodi hizi ni za wafanyakazi ambao ni Wakuu wa Idara, zinaundwa pale kwenye halmashauri lakini viongozi wa mikoa wengi wanaziingilia, wanaingilia maamuzi, sana tu, jambo ambalo linasababisha shida lakini inapokuja habari ya TAKUKURU watu wanaruka. Watu wakisikia tu kuna kubanwa na TAKUKURU wanasema hapana ulipaswa kutekeleza yale ambayo unapaswa kutekeleza. Kwa hiyo, nadhani Serikali iko hapa viongozi wa mikoa na sekretarieti za mikoa waambiwe waziache Bodi za Zabuni ziwe huru kufanya mambo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ucheleweshaji wa michakato ya manunuzi. Sheria hii inasaidia, itapunguza muda kwa sababu muda ulikuwa mrefu na matokeo yake gharama ilikuwa inaongezeka. Ni wakati sasa Serikali ihakikishe sheria hii inasaidia kupunguza huo mchakato na watu wajikite kwenye manunuzi kwa *speed* na kazi ifanyike bila kuchelewesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la wataalam amelizungumzia Mheshimiwa Dkt. Kamala. Maafisa Ugavi ni wachache sana. Pamoja na uchache wao lakini taaluma hii inaoonekana kama kutokuheshimika kama ambavyo Mheshimiwa Dkt. Kamala amesema ukilnganisha na fani zingine za uhasibu, udaktari na uanasheria kwani bodi au taaluma hizo zinaheshimika sana tofauti kabisa na hawa. Maafisa Ugavi hawaheshimiki na wanasakamwa sana kwa kudhani kwamba wao ndiyo sehemu ya ulaji wa rushwa kumbe wanahitaji na wenyewe waheshimike na labda chombo chao kiweze kuwa *strong* kuweza kusimamia mambo haya ya manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la madeni, nililizungumza wakati wa mjadala wa bajeti kuu. Madeni ni mengi mno katika magereza, hospitalini, kwenye shule, watu wametoa huduma kwa nini Serikali inasuasua kuwalipa watu hawa? Maana yake ku-*supply* ni kuisaidia Serikali, ni kwamba wameikopesha Serikali, Serikali ifanye kila inaloweza kulipa madeni haya tuondokane na shida zilizoko. Maana kila siku Mbunge ukifika au Mwenyekiti wa Halmashauri ukifika lazima watu wanakufuata kwa ajili kukusisitiza madeni yao yaweze kulipwa. Siyo wao tu, wakandarasi hawalipwi kwa wakati na matokeo yake miradi hii inakwenda kwa kusuasua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sikuwa na mengi sana kwa sababu kama nilivyosema leo niko sambamba na Serikali, ingekuwa tofauti mimi napasua pale pale. Leo naipongeza Serikali, Mheshimiwa Waziri hongera sana kwa kuwasikia Waheshimiwa Wabunge na kwa ku-*react* kwa *speed* na Serikali nzima ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Kadutu au wewe ni sehemu ya ile timu inayocheza leo? Tuendelee Waheshimiwa, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo ajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ambayo imeletwa na Waziri wa Fedha. Kwanza, nampongeza kwa kuleta mabadiliko ya hoja hii ambayo ni muhimu sana. Suala la manunuzi ya umma Serikalini ni kitu cha msingi na muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ununuzi wa umma ni kipimo cha namna Serikali inavyoendesha shughuli zake, inavyofuata sharia, uwazi na namna ambavyo inadhibiti vitendo vyovyote vya rushwa kwenye zabuni. Zabuni ni eneo ambalo linaleta rushwa sana. Zile rushwa kubwa kubwa zinazozungumzwa zinatoka kwenye zabuni kubwa, mikataba mikubwa, yote inatokea hapa kwenye hii kitu inaitwa zabuni na ndiyo maana asilimia 70 ya bajeti inakwenda huko kwenye suala la mchakato wa zabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria yetu ya *Public Procurement, Cap 410* ina historia ambayo imeanzia tangu 1990, tukaja kwenye ya 2011 pamoja na *regulations* zake lakini pamoja na sheria zote hizo utaona kwamba bado haijakidhi matakwa yale ambayo yanatakiwa ili sheria hii iweze kuwa nzuri na itekelezeke vizuri. Kwa hiyo, mabadiliko yanatokea na ndiyo maana sheria hii sasa hivi imeletwa hapa kufanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sheria hii ambayo bado haijafanyiwa marekebisho imesaidia kwa kiwango kikubwa hasa kwenye udhibiti wa

corruption. Imedhibiti rushwa kwa sababu imekuwa na Kamati nyingi sana pamoja na changamoto ya urasimu na muda lakini kwa njia moja au nyingine imesaidia kuweka *transparency* kwenye suala zima la mchakato wa hizo zabuni. Pia sheria hii ambayo tunataka kuibadilisha imesaidia sana kutoa *opportunities* za kutoa zabuni za kimataifa ambazo sasa hivi tunazifanyia mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sheria ambayo sasa hivi imeletwa hapa ina umuhimu sana kwa sababu imeingiza kitu ambacho kinaitwa *value for money* ambacho ni muhimu sana na kimewekwa mpaka kwenye hii *preamble* ambayo ipo kwenye haya mabadiliko. Ukiangalia kifungu cha 3 au cha 2 kimeweka hiyo *preamble* ambayo inaonyesha kwamba sasa sheria hii itaangalia *value for money* na sasa hivi ndiyo sheria nyingi za zabuni zinakwenda kwenye mwelekeo huo. Nilikuwa naangalia Sheria ya Manunuzi ya *World Bank* pamoja na *EU* zote hizo zimeingiza kitu kinaitwa *value for money*. Pia imejaribu kuondoa mlolongo mzima wa michakato hii na kupunguza hizi Kamati ambapo kila Kamati ikikaa inapewa hela, sasa mlolongo wote huo umeondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kimoja kimewekwa ambacho wenzetu pia wamekiweka badala ya kulenga tu *bidder* yule ambaye ana bei ya chini inaangalia huyu mzabuni pamoja na kuwa na bei ya chini, je, vitu vyake vina ubora kiasi gani? Sasa hicho ni kitu muhimu, kuangalia ubora na siyo kuangalia tu thamani kwamba hii ni thamani ndogo basi huyu mpe kwa sababu thamani ndogo ameshinda hiyo tenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha msingi ambacho nimekitafuta kwenye marekebisho haya sikukiona ni suala la *negotiations* kwamba huyu ameshinda, je, kuna utaratibu gani umewekwa ambapo wanaacha mambo ya kwenda kwenye bei ndogo wanaingia kwenye majadiliano na wazabuni kuweza kuangalia ubora *irrespective* ya bei ambayo ameitenda? Kwa hiyo, ni kitu cha msingi naomba Mheshimiwa Waziri aeleze amekiweka wapi kwenye hizi *provisions* ambazo zipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na-*support* kabisa suala ambalo limewekwa kuanzia kifungu cha 55A, 55B, 55C na 55D ambapo inawakata makali wageni na kuwaruhusu wazawa kushiriki kwenye zabuni hizi. Suala hili limekuwa likiathiri sana zabuni nyingi kwa sababu utakuta wanapewa watu wa nje na wanaleta wataalamu wao na wengine hata hawana utaalam wanajaa kwenye hizo zabuni wanafanya kazi na watu wetu wanakosa kazi za kufanya. Hii itasaidia sana kwa sababu watu wetu watapata nafasi ya kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la ushindani wa zabuni, kwenye zabuni lazima pawepo na ushindani lakini pawepo pia na zabuni ambazo hazina ushindani (*single source)* lakini hizi *single source* pia ni lazima zirekebishwe

ziendane na wakati. Nimeangalia kwenye kifungu cha 65A na 65C na nimeona ushindani huu wa *single source* ameachiwa Waziri kutengeneza hizo *regulations*. Hapa ni lazima tuwe waangalifu sana vinginevyo tunaweza tukarudi kwenye suala lile lile ambalo liko chini. *Single source* ni muhimu na lazima tui-*encourage* kwa sababu kuna mifano mingi ambapo zabuni unaweza ukanunua moja kwa moja kutoka kiwandani na ikaanza kufanya kazi. Kwa hiyo, ningeshukuru kama suala hili litapewa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna suala la zabuni maalum wakati wa athari au panapotokea chochote kile ambacho ni cha dharura hapo tena huwezi ukasema kwamba unaanza mambo ya tenda itachukua mlolongo mrefu. Ni lazima sheria iruhusu vitu vya wakati huo kwamba sasa hivi vitu vya dharura viruhusiwe mtu aweze kwenda moja kwa moja kwenye *single source* na kuanza kufanya manunuzi. Hiyo *special provision* lazima iwepo na ionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala kubwa ambalo linatakiwa kwenye zabuni ni uaminifu na uadilifu na namna watumishi wa Serikali watakavyofanya kazi hiyo. Naunga mkono hoja hii kwa sababu imejaribu kutaja mambo mengi ambayo ni muhimu. Cha msingi hasa ambacho sijakiona na napenda Waziri atuthibitishie, wakati wazabuni wanaingia kwenye majadiliano, suala la kui-*inflate rate* ni kitu cha muhimu sana. Watumishi wengi wa Serikali wanaongeza bei pale kwenye zabuni na ile kuongeza bei inawapa tabu sana hata wapelelezi namna ya kuchunguza na kujua hii kitu bei yake ni shilingi ngapi. Kwa hiyo, ni vizuri wakati wa zabuni tuwe na *assessment* ya kujua kwamba chombo hiki ambacho tunataka kiingie kwenye zabuni au gharama ya kutengeneza hii barabara inaweza kuwa shilingi ngapi? A*tleast* tukiwa na *maximum evaluation* itasaidia kuondoa hii *thinking* ya kuongeza bei jinsi anavyotaka mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii na nashukuru kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Amina Saleh Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo kama bado tutakuwa na muda Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba atamalizia.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia mawili matatu katika Sheria hii ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuleta Muswada huu. Nampongeza pia Waziri mwenye dhamana,

Waziri Mpango kwa mipango mizuri ambayo ninaamini kabisa inatupeleka kwenye uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwanza kwa kuunga mkono hoja lakini vilevile niipongeze tena Serikali kwa sababu imeona umuhimu wa kuleta sheria hii na hasa kwangu mimi nafurahia sana kwa kuona ni kwa jinsi gani makundi maalum yameainishwa katika sheria hii. Vilevile niombe tuangalie, je, katika makundi haya maalum ni utaratibu upi mzuri utakaoandaliwa ili kuhakikisha kwamba makundi haya na yenyewe yanapata nafasi hii na kuweza kushiriki katika mchakato huu mzima pasipo kuachwa nyuma na tunapoelekea katika uchumi wa kati tuhakikishe kwamba hakuna anayeachwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende sasa katika ukurasa wa 13 katika kipengele cha 27 ambapo kinasema kwamba marekebisho haya yana lengo la kuifanya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma kuwa chombo pekee chenye mamlaka ya kufungia. Naomba tu nishauri hapo kwa sababu kama ni kampuni, kwa mfano kampuni 'A' ikifungiwa inaweza kuanzisha kampuni nyingine na wakaendeleza kufanya mchakato huu au kuendelea na kazi. Vilevile kama ni Wakurugenzi hawa wakifungiwa wanaweza pia kutumia wenza wao au ndugu zao kuhakikisha kwamba wanaendeleza suala hili. Hapa niiulize Serikali itadhibiti vipi jambo hili lisiweze kujitokeza. Naomba sana Serikali izingatie suala hili ili kuhakikisha kwamba kama kweli kampuni imefungiwa au kama kweli Wakurugenzi fulani wamefungiwa basi wasipate nafasi tena ya kutumia mlango wa nyuma kushiriki katika kuweza kupata hiyo tenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile sheria hii itapunguza zile 10% zilizokuwa zikitumiwa na ofisi za Serikali na mfano mzuri tu ni katika matangazo. Matangazo mengi ambayo yanatoka Serikalini au katika Wizara mbalimbali unakuta yamechajiwa gharama kubwa na hii ni kwa sababu ya wale watu ambao wanaweka zile 10% au kwa wale wafanyakazi/watumishi wa umma ambao siyo waaminifu wanatumia hii 10% kuhakikisha kwamba wanavyopeleka matangazo na cha kwao kinarudi ili waweze kujipatia. Kwa hiyo, mimi naona hii ni faraja kubwa sana na niiombe tu Serikali kuhakikisha kwamba sheria hii kweli inakuwa ni msumeno ambao unakula pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile sheria hii itasaidia pia kuhakikisha kwamba vitu vingi vinakuwa vya viwango. Wakati mwingine wakandarasi hawa wamekuwa wakikubali kuingia makubaliano lakini katika makubaliano hayo kunakuwa na zile 10% ambazo zinasababisha washindwe kutimiza wajibu wao mfano ni katika ujenzi wa barabara mbalimbali. Barabara mojawapo katika Jiji la Dar es Salaam ni ya Baracuda ambayo imetengenezwa hivi karibuni tu lakini tayari hivi sasa imekwishakuwa na mashimo mengi tu. Siyo hiyo tu lakini barabara ya Tabata ambayo inapita katika Shule ya St. Marys ilitengenezwa

kwa muda mfupi na ikaharibika na hii ni kutokana na hizo hizo 10% ambazo zinaiingizia gharama kubwa Serikali. Pamoja na mabadiliko haya ya sheria niiombe Serikali iweke adhabu kali kwa wale wakandarasi ambao kwa namna moja au nyingine watapewa tenda hizo na matokeo yake wakafanya kile kitu katika kiwango ambacho hakikubaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niungane na maoni ya Kamati ya Bajeti na nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, tuzungumzie hili ambapo katika ofisi nyingi za Serikali ambapo unakuta kuna idara takriban nne/tano na idara hizo zote zina Wakurugenzi Wasaidizi na hawa wasaidizi wamekuwa wakitumia magari ya Serikali na mafuta ya Serikali lakini cha kusikitisha mwisho wa mwezi pia utakuta wana posho kwa ajili ya mafuta. Sasa hapa niulize tu kama mtu kapewa gari, dereva yupo bado mwisho wa mwezi ana posho ya mafuta, haya mafuta ni ya nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile baadhi ya watumishi ambao siyo waaminifu wamekuwa wakiyatumia vibaya na pengine hili pia litawapunguzia adha baadhi ya madereva mfano wale wa Jiji la Dar es Salaam. Dereva huyo analazimika kuamka saa kumi alfajiri kwa ajili ya kumfuata bosi na wakati mwingine bosi huyu inawezekana anakaa mbali Bunju, amfikishe ofisini. Gari hilo ni la Serikali, mafuta ya Serikali, mwisho wa mwezi kuna posho ya mafuta. Kwa hiyo, naipongeza kwa kweli Serikali yangu na nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri Mpango kwa mipango mizuri ambayo naamini kabisa ina lengo la kututoa hapa tulipo kutupeleka katika uchumi wa kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana naunga mkono hoja 100%. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo na kama muda utabaki tutamalizia na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hotuba hii iliyopo mbele yetu juu la Sheria ya Manunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingi ni ushauri lakini katika ushauri huu nadhani ni vizuri sana tukajaribu kuangalia namna gani tunazisaidia halmashauri zetu kwa mfano katika suala la usafi. Suala la usafi ni gumu sana katika halmashauri zetu. Tunapoweka utaratibu huu wa manunuzi kwenye usafi ina maana kwamba tenda zetu zinafuata mwaka wa fedha na inakuwa ni muda wa mwaka mmoja. Sasa tujiulize kwamba ni nani ana uwezo wa kuwekeza vifaa vya usafi kwenye mji halafu akavitumia kwa mwaka mmoja halafu baada ya hapo mwaka unaofuata anakosa ile tenda! Jiulize hata kama ungekuwa wewe umenunua lori la kusomba takataka, umewekeza kwenye

mradi wa kusomba takataka katika mji na umeshinda tenda lakini mwaka unaofuata bahati mbaya umekosa hiyo tenda, hilo gari utalipeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo kama hili liliwahi kutokea pale Dar es Salaam miaka ya nyuma. Imetangazwa tenda ya kukusanya ushuru wa maegesho, mtu kawekeza, kafunga mashine za kisasa kabisa kukusanya ile ada ya *parking* mwaka uliofuata kakosa tenda mashine zile inabidi ang'oe akaweke nyumbani, hazina kazi nyingine zaidi ya kuuza tiketi za *parking*. Kwa hiyo, nashauri kwamba ziko tenda ambazo lazima tuziwekee kipengele maalum kwa mfano kama ni suala la vifaa vya usafi ama usafi wa miji basi ni lazima Serikali ione kwamba hapa mwekezaji wake awe tofauti au anayeiomba hii tenda awe tofauti na tenda nyingine za kawaida. Kwa sababu mtu hawezi kununua magari kwa ajili ya kufanya usafi katika mji, ameshinda tenda, ame-*operate* kwa mwaka mmoja, mwaka unaofuata amekosa ile tenda. Sheria inawafanya halmashauri watangaze tenda kwa mtu mwingine na wewe unaikosa, sasa yale magari utafanya nayo nini, utakuwa huna kazi ya kufanyia yale magari. Kwa hiyo, naomba sana Serikali iangalie hilo na ione ni kwa namna gani inaweza ikasaidia halmashauri zetu kuwa safi. Miji yetu inashindwa kuwa misafi kwa sababu ya utaratibu wa kuwapata wakandarasi wa kufanya usafi katika miji. Hilo suala la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni la ujenzi katika halmashauri zetu. Ziko halmashauri zina vifaa vya ujenzi lakini havina sifa ya kufanya kazi ya ujenzi ndani ya halmashauri kwa kutumia fedha ambayo Serikali inaitoa ili kusudi barabara zitengenezwe na miradi mbalimbali ya ujenzi ifanyike. Naomba niishauri Serikali hapa, kwa zile halmashauri ambazo zimekamilisha seti ya vifaa kwenye kanuni ioneshwe kwamba wapate kibali kutoka kwa Waziri wa TAMISEMI kuwaruhusu kutengeneza angalau barabara moja ili kusudi halmashauri na yenyewe iweze kupata ile fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, halmashauri ina wataalam, unakuta ina injinia na ndiye anayesimamia barabara zote kwa hiyo uzoefu anao. Matokeo yake tunakuja kutoa tenda ya mamilioni ya kujenga barabara zetu kwa mkandarasi aliyekuja na begi na *jeans* tu, anaanza kukodi vifaa vilevile vya halmashauri halafu anaanza tena kuwasumbua kulipa na anaanza kuhangaika kutafuta vifaa mahali pengine. Niombe sana Serikali iangalie hili kwa sababu halmashauri zimetumia fedha nyingi sana kununua vile vifaa vya ujenzi na vimekamilika. Kwa hiyo, angalau 25% kwenye miradi ya ujenzi ndani ya halmashauri, halmashauri iruhusiwe kuijenga na Serikali iwalipe kama inavyowalipa wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la Kamati ya Fedha kutokupitia wakandarasi waliopitishwa na Bodi ya Manunuzi. Naomba Serikali iangalie, jambo hili kwanza halicheleweshi mchakato wa aina yoyote kwa sababu vikao vile vya *finance* viko kila mwezi na vina ratiba yake. Suala la kupitisha au kuwapitia wakandarasi hawa linakuja pengine kwenye halmashauri mara moja au mbili tu katika mwaka, wala haihusiki kabisa kumchelewesha mkandarasi wala kuzuia shughuli ya aina yoyote ya mkandarasi lakini ile inasaidia kujiridhisha na kupanua maarifa. Kwa sababu ndani ya halmashauri wale Madiwani wanaoshiriki katika vikao vile vya *finance* wanauelewa mbalimbali, wanaweza wakasaidia kuishauri halmashauri namna gani mkandarasi huyu yupo na wanamfahamu namna gani. Sioni kama kuna haja ya kuiondoa hii Kamati ya Fedha ya Halmashauri kutokushiriki katika mchakato wa kuwa-*award* tenda. Niombe sana Serikali ilione hilo kwa sababu lenyewe lilikuwa halipunguzi chochote kwenye halmashauri badala yake lilikuwa linajaribu kuongeza ubora wa kazi ambayo Kamati ile ya tenda imefanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, nimefurahi sana sheria hii imekuja na utaratibu sasa wa kubishania bei kwamba mnajadiliana bei na *supplier* ili kusudi halmashauri iweze kupata huduma. Niiombe sasa Serikali, vinginevyo hapa tutasababisha matatizo kwa watendaji kwa sababu watatumia nafasi hii, watabishania bei, watapata bei nzuri lakini inapokuja kwenye malipo sasa, tutasababisha tatizo kubwa sana kama hatutalipa kwa wakati. Tukumbuke kwamba walikuwa wanaweka bei ya juu na ilikuwa inawasaidia kwa sababu fedha yao ilikuwa inakaa Serikalini. Leo hii tukijaribu kuangalia unaweza ukakuta kuna watu huko Magereza na kwenye Shule za Sekondari hawajalipwa. Kwa hiyo, niombe sana tunapofikia mahali pa kuanza kuitumia sheria hii malipo kwa *suppliers* yaweze kutolewa kwa wakati kwa sababu unapobishania bei ina maana kwamba utapata bei ya soko halafu unachelewesha malipo zaidi ya miezi sita maana yake hutaki huyo *supplier* aendelee kukuhudumia ndiyo unamuua kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazingira ambayo *supplier* ana-*supply* chakula cha wanafunzi, akikataa kuleta chakula kwa sababu wewe hujamlipa maana yake watoto wale watalala njaa. Ukitaka kujua kichaa cha watoto wa shule wanyime chakula, watachoma shule, watapiga walimu, wao hawatajua kama ni *supplier* hajaleta chakula. Kwa hiyo, niombe sana suala hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna kundi lingine ambalo ni dhaifu sana, kundi la wafungwa. Tusipoangalia utaratibu tunaouweka hawa wafungwa ndiyo tunaenda kuwapa adhabu ya mara ya pili ya kulala na njaa. Kwa sababu huyu *supplier* atasema naleta leo mnilipe pesa kesho, mtasema sawa, ataleta hakupewa fedha miezi inakwenda, siku nyingine haleti, wafungwa wanalala njaa na wafungwa kwa sababu hawana pa kulalamika maana yake

sasa tutakuwa tunasababisha adhabu mara mbili ya adhabu waliyohukumiwa. Kwa hiyo, niombe sana, kama tunakubaliana sheria hii ni nzuri ipite basi niiombe Serikali ihakikishe kwamba kweli kila mmoja anatimiza wajibu wake, anahakikisha kwamba fedha inakuwepo, huyu *supplier* anatoa hiyo huduma na Serikali inamlipa kwa wakati. Hivi ndivyo tutaweza kusaidia hii sheria ifanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie tena kuomba, tafadhali sana halmashauri zenye vifaa vya ujenzi zipewe angalau zile kazi zilizoko kwenye mpango wa kazi kwa 25% ili kusudi na zenyewe ziweze kujijenga zaidi. Kwa sababu tunategemea miaka ijayo halmashauri ziweze kujitegemea zenyewe kwa kila jambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja sheria hii iweze kutusaidia kupunguza gharama kwa Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, muda uliobaki unaweza tu kuchangia kwa dakika tano. Sasa uchaguzi ni wako, uchangie kwa dakika tano au uchangie kesho dakika zako zilizo kamili.

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia kesho.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji wa hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa jioni ya leo, tutaendelea tena kesho. Ninalo tangazo kwenu la kuwakumbusha wanawake wote kwenda kwenye futari hoteli ya Morena leo Jumanne tarehe 28, Juni, 2016, saa 12.00 jioni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Jumatano tarehe 29 Juni, 2016, saa tatu kamili asubuhi.

(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,
Tarehe 29 Juni 2016, Saa Tatu Asubuhi)